TATHMINI YA HADITHI FUPI ZILIZOWASILISHWA KATIKA *BRITISH BROADCASTING CORPORATION*: MTAZAMO WA EDGAR ALLAN POE NA LEECH (1969)

FRANCIS MAINA MACHARIA
C50/30827/2015

TASNIFU YA UTAFITI ILIYOWASILISHWA KWA IDARA YA KISWAHILI CHUO KIKUU CHA KENYATTA KWA MINAJILI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI

MEI, 2021

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu na haijafanywa na mtahiniwa yeyote kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu kingine chochote ila mimi tu.

Sahihi:..... Tarehe: 6/5/2021

Jina: FRANCIS MAINA MACHARIA

C50/30827/2015

Wasimamizi:

Tasnifu hii imewasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa utafiti huu katika chuo kikuu cha Kenyatta.

Sahihi:..... Tarehe:.....

Jina: DKT. RICHARD M. WAFULA

Chuo Kikuu Cha Kenyatta

Idara ya Kiswahili

Sahihi:..... Tarehe:.....

Jina: DKT. PAMELA M. Y. NGUGI

Chuo Kikuu Cha Kenyatta

Idara ya Kiswahili

TABARUKU

Ninaitabaruku tasnifu hii wazazi wangu: Jane Mugure Oldikir Macharia na Evanson Macharia Maina. Isitoshe, ndugu yangu Benson Kiruri Macharia na dadangu Eunice Wangechi Macharia. Vilevile, mjombangu Julius Olaibon. Bila kusahau, ndugu zangu wa tangu utotoni Awadh Basheikh Ahmed na Ally Hemed Mtawa. Mwisho, rafiki yangu Wesley Ongige Abaya ambaye tuliajiriwa pamoja na Tume ya Kuwaajiri Walimu (TSC) Shule ya Upili ya *Sacred Heart Mwakiwiwi Girls* mnamo mwaka wa 2018.

SHUKURANI

Mwenyezi ulotukuka, mja wako nashukuru,
Ni mema yalonifika, mwanao naona nuru,
Joho jipya menivika, abadani sikufuru,
Shahada nimeipata, Ya Rabbi nanyenyekea.

Asante wangu walezi, wasimamizi tajika,
Ni mengi nimemaizi, yasoweza hesabika,
Singaupata ujuzi, mkono singawashika,
Asanteni daktari, Wafula nawe Pamela.

Wahadhiri idarani, sijui niseme nini?
Mtasalia moyoni, si haba nawathamini,
Shahada i mikononi, mlinilinda ndiyani,
Mola mwingi wa rehema, azidi kuwabariki.

Bwana Simiyu na Lawi, tulifaana chuoni,
Kwa raha na yalo mawi, tukazama masomoni,
Hivi leo twasitawi, tabasamu zi nyusoni,
Akufaaye kwa dhiki, hakika ndiye rafiki.

Wazazi nipulikani, wa maisha maridhia,
Sina la kuwalipani, malipo yangu ni dua,
Sichoki washukuruni, elimu nimepokea,
Upendo wenu wa dhati, upendo ulo adhimu.

Tamati hapa natua, beti sita sendi mbali,
Nimesogea hatua, kufikia uzamili,
Uzamifu nawazia, nishishiyelo ni hili,
Nguzo yangu ni Rabuka, Maina ndo langu jina.

IKISIRI

Utafiti huu umetathmini hadithi fupi zilizowasilishwa katika BBC kwa kuzingatia mtazamo wa Edgar Allan Poe. Katika kufanya hivyo, mtafiti amejihusisha na uhakiki wa mikusanyiko: *Mapenzi ni Kikohozi* (1970), *Vituko Duniani* (1970), *Pavumapo Palilie* (1971) na *Kinywa Jumba la Maneno* (1977) za kipindi kati ya 1970 hadi 1977 maarufu kama "Hekaya za Kuburudisha" zilizochapishwa na shirika la Longman Kenya wakishirikiana na BBC. Mikusanyiko hii inajumuisha hadithi ambazo zilitokea kuwa bora na hivyo zikasomwa hewani na shirika la utangazaji la BBC na hatimaye zikachapishwa kwanzia 1970 hadi 1977. Mtafiti amezingatia mtazamo wa Edgar Allan Poe (1842; 1846) na kipengele cha uhakiki cha mtindo katika kutalii hadithi hizi na kukadiria usanii wa watunzi wa hadithi fupi teule. Kwa kufanya hivyo, ametathmini hadithi fupi zilizowasilishwa katika BBC. Nadharia ya uhakiki ya mtindo pamoja na misingi ya hadithi fupi iliyowekwa na Poe (1842; 1846) imetumika katika kufanikisha utafiti huu. Leech na Short (1981) wanafafanua mtindo kama namna mwandishi anavyotumia lugha kuzingatia muktadha maalumu na kwa lengo mahsusi. Mtindo ni ule upekee wa kujieleza katika maandishi au mazungumzo. Poe (1842; 1846) anaweka misingi ya hadithi fupi kwa kuorodhesha vigezo muhimu ambavyo vinafaa kuzingatiwa ili kufanya hadithi fupi kuvutia na kuwa bora. Nadharia ya mtindo na misingi iliyowekwa na Poe imesaidia katika kutathmini hadithi fupi zilizoko katika mikusanyiko hii ya awali zaidi. Mbinu ya utafiti iliyotumika ni ya kimaelezo ikirutubishwa kwa kiasi fulani na mbinu ya kitakwimu. Mbinu ya kimaelezo imetumika pale ambapo mtafiti amedondoa sentensi au matukio ya kimaelezo na kuchanganua hadithi teule. Aidha, mbinu ya kitakwimu imetumika wakati wa kuteua hadithi mbalimbali kutoka mikusanyiko ya hadithi fupi tuliyoorodhesha. Sampuli imeteuliwa kimaksudi. Utafiti umekuwa wa maktabani. Inatarajiwa utafiti huu utakuwa na mchango hasa kwa upande wa muundo, maudhui na usawiri wa wahusika katika mtindo kwa kuonyesha namna hadithi fupi inastahili kusukwa ili kuwafaa waandishi chipukizi katika kusanii kazi zenye ubora wa muundo, mtindo na maudhui.

ABSTRACT

This research seeks to evaluate the short stories that were aired by BBC using Edgar Allan Poe's view on short stories. The researcher has developed a critique on some of the short stories in the collections: *Mapenzi ni Kikohozi* (1970), *Vituko Duniani* (1970), *Pavumapo Palilie* (1971) and *Kinywa Jumba la Maneno* (1977). These collections are commonly known *as "Hekaya za Kuburudisha"* which were published by Longman Kenya and BBC. The above mentioned collections have short stories that were aired by BBC and later published between 1970 and 1977 due to their high literary standards. The researcher has based his literary analysis on both style and Poe's view on short stories to understand what made the stories appealing to the listeners and finally be published. In doing so, we have evaluated the standards of the short stories using Edgar Allan Poe's view on short stories. The research has been guided by stylistic theory and Poe (1842; 1846) view on short stories. Leech and Short (1981) explain style as how a writer uses language in a particular context for a specific reason. Style is an individuals uniqueness in writing or speaking. Poe (1842; 1846) gives his view on short stories by highlighting what a writer ought to consider to make his story appealing. We have used both qualitative and quantitative methods of research. Qualitative method has been of importance when writing down our criticism on the selected texts whereas quantitative method has been used when identifying the number of stories that need to be analysed from each collection. Moreover, the research is library oriented. It is hoped that the findings of this research will be of benefit to upcoming authors in showing factors to consider while writing a short story.

ISTILAHI ZILIZOTUMIWA

Ukiushi: Matumizi ya sifa za kimtindo zisizo za kawaida na zinazoonekana kwenda kinyume na matarajio au sifa za kimatumizi za lugha zilizo katika jamii fulani wakati fulani maalumu.

Uchimuzi: Ni mbinu ya kutilia mkazo mambo fulani yanayopewa uzito mwingi katika kazi ya fasihi. Hutumiwa kurejelea sifa za kiisimu pamoja na kimtindo zinazomsaidia msomaji kuona jambo fulani kwa uwazi zaidi.

Ujumi: Kanuni za uzuri au ubaya wa kazi yoyote ile ya fasihi.

Mtindo: Ni upekee wa kujieleza katika maandishi au mazungumzo.

Hadithi fupi: Ni masimulizi yanayojikita na idadi ndogo ya wahusika katika kueleza tukio moja maalum.

ORODHA YA VIFUPISHO

BBC:	British Broadcasting Corporation
HF:	Hadithi fupi
AM:	Afrika Mashariki
TEKNOHAMA:	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
FS:	Fasihi Simulizi
FA:	Fasihi Andishi
Uk:	Ukurasa
Kur:	Kurasa
Mhr:	Mhariri
Wahr:	Wahariri
Juz:	Juzuu

YALIYOMO

UNGAMO.....ii
TABARUKU iii
SHUKURANI.....iv
IKISIRI v
ABSTRACT.....vi
ISTILAHI ZILIZOTUMIWA.....vii
ORODHA YA VIFUPISHO..... viii
YALIYOMO.....ix
SURA YA KWANZA 1
UTANGULIZI.....1
1.1 Usuli wa Mada 1
1.2 Suala la Utafiti 4
1.3 Maswali ya Utafiti.....6
1.4 Malengo ya Utafiti 6
1.5 Sababu za Kuchagua Mada.....6
1.6 Upeo na Mipaka.....8
1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada.....9
1.8 Misingi ya Nadharia.....17
1.8.1 Misingi ya Nadharia ya Hadithi Fupi kwa Mtazamo wa Poe (1842; 1846).....17
1.8.2 Nadharia ya Mtindo kwa Ujumla.....19
1.8.2.1 Dhana ya Wahusika na Uhusika katika Uhakiki wa Kimtindo.....22
1.8.2.2 Aina ya Wahusika katika Hadithi Fupi 23
1.9 Mbinu za Utafiti.....25
1.9.1 Mahali pa Utafiti 26
1.9.2 Muundo wa Utafiti.....26
1.9.3 Uteuzi wa Sampuli.....27
1.9.4 Ukusanyaji wa Data 27
1.9.5 Uchanganuzi wa Data 28

1.9.6 Uwasilishaji wa Matokeo....28
1.9.7 Hitimisho....29
SURA YA PILI....30
TATHMINI YA MIUNDO YA HADITHI FUPI TEULE....30
2.1 Utangulizi....30
2.2 Mtiririko wa Mawazo katika Hadithi Fupi Teule....30
2.2.1 Mtiririko wa Mawazo katika Hadithi, "Siku ya Arobaini" (Mohamed, 1970)....31
2.2.2 Mtiririko wa Mawazo katika Hadithi, "Kusoma na Kupenda" (Salim, 1970)....32
2.2.3 Mtiririko wa Mawazo katika Hadithi, "Ajuta Majuto ya Mjukuu" (Somba, 1970)....34
2.2.4 Mtiririko wa Mawazo katika Hadithi, "Maisha Yalimwendea Kombo" (Isaakwisa, 1970)....36
2.2.5 Mtiririko wa Mawazo katika Hadithi, "Mzee Khamis, Leo Wapi?" (Mohamed, 1971)....38
2.2.6 Mtiririko wa Mawazo katika Hadithi, "Malipo Duniani, Hesabu Ahera" (Said, 1971)....42
2.2.7 Mtiririko wa Mawazo katika Hadithi, "Sina Rafiki" (Wahab, 1977)....44
2.2.8 Mtiririko wa Mawazo katika Hadithi, "Mke Wangu" (Muhammed, 1977)....50
2.3 Ujenzi wa Tukio Moja katika Hadithi Fupi Teule....55
2.3.1 Ujenzi wa Tukio Moja katika Hadithi, "Siku ya Arobaini" (Mohamed, 1970)....56
2.3.2 Ujenzi wa Tukio Moja katika Hadithi, "Kusoma na Kupenda" (Salim, 1970)....56
2.3.3 Ujenzi wa Tukio Moja katika Hadithi, "Ajuta Majuto ya Mjukuu" (Somba, 1970)....57
2.3.4 Ujenzi wa Tukio Moja katika Hadithi, "Maisha Yalimwendea Kombo" (Isaakwisa, 1970)....58
2.3.5 Ujenzi wa Tukio Moja katika Hadithi, "Mzee Khamis, Leo wapi?" (Mohamed, 1971)....59
2.3.6 Ujenzi wa Tukio Moja katika Hadithi, "Malipo Duniani, Hesabu Ahera" (Said, 1971)....59

2.3.7 Ujenzi wa Tukio Moja katika Hadithi, “Sina Rafiki” (Wahab, 1977)....60
2.3.8 Ujenzi wa Tukio Moja katika Hadithi, “Mke Wangu” (Muhammed, 1977) 61
2.4 Aina ya Migogoro na Utatuzi wa Migogoro katika Hadithi Fupi Teule....62
2.4.1 Aina ya Migogoro na Utatuzi Wake katika Hadithi, “Siku ya Arobaini” (Mohamed, 1970)....62
2.4.2 Aina ya Migogoro na Utatuzi Wake katika Hadithi, “Kusoma na Kupenda” (Salim, 1970) 63
2.4.3 Aina ya Migogoro na Utatuzi Wake katika Hadithi, “Ajuta Majuto ya Mjukuu” (Somba, 1970) 64
2.4.4 Aina ya Migogoro na Utatuzi Wake katika Hadithi, “Maisha Yalimwendea Kombo” (Isaakwisa, 1970) 65
2.4.5 Aina ya Migogoro na Utatuzi Wake katika Hadithi, “Mzee Khamis, Leo Wapi?” (Mohamed, 1971) 66
2.4.6 Aina ya Migogoro na Utatuzi Wake katika Hadithi, “Malipo Duniani, Hesabu Ahera” (Said, 1971) 67
2.4.7 Aina ya Mgogoro na Utatuzi Wake katika Hadithi, “Sina Rafiki” (Wahab, 1977)....68
2.4.8 Aina ya Mgogoro na Utatuzi Wake katika Hadithi, “Mke Wangu” (Muhammed, 1977)....69
2.5 Matumizi ya Lugha katika Hadithi Fupi Teule....70
2.5.1 Taswira....71
2.5.2 Chuku....71
2.5.3 Msemo....72
2.5.4 Lakabu....72
2.5.5 Methali....73
2.5.6 Nahau....74
2.5.7 Sadfa....74
2.5.8 Uzungumzinafsi....75
2.5.9 Nidaa....75
2.5.10 Tabaini....76
2.5.11 Balagha....76
2.5.12 Kinaya....77

2.6 Hitimisho....78
SURA YA TATU....79
USAWIRI WA WAHUSIKA KATIKA HADITHI FUPI TEULE....79
3.1 Utangulizi....79
3.2 Aina ya Wahusika....79
3.2.1 Wahusika Wakuu katika Hadithi Fupi Teule....80
3.2.2 Wahusika Wasaidizi katika Hadithi Fupi Teule....83
3.2.3 Wahusika Wadogo katika Hadithi Fupi Teule....86
3.2.4 Wahusika Bapa katika Hadithi Fupi Teule....89
3.2.5 Wahusika Mviringo au Duara katika Hadithi Fupi Teule....92
3.2.6 Wahusika Foili katika Hadithi Fupi Teule....95
3.3 Idadi ya Wahusika na Jukumu la Wahusika katika Hadithi Fupi Teule....98
3.3.1 Idadi ya Wahusika na Jukumu lao katika Hadithi, "Siku ya Arobaini" (Mohamed, 1970)....98
3.3.2 Idadi ya Wahusika na Jukumu lao katika Hadithi, "Kusoma na Kupenda" (Salim, 1970)....101
3.3.3 Idadi ya Wahusika na Jukumu lao katika Hadithi, "Ajuta Majuto ya Mjukuu" (Somba, 1970)....104
3.3.4 Idadi ya Wahusika na Jukumu lao katika Hadithi, "Maisha Yalimwendea Kombo" (Isaakwisa, 1970)....107
3.3.5 Idadi ya Wahusika na Jukumu lao katika Hadithi, "Mzee Khamis, Leo Wapi?" (Mohamed, 1971)....111
3.3.6 Idadi ya Wahusika na Jukumu lao katika Hadithi, "Malipo Duniani, Hesabu Ahera" (Said, 1971)....114
3.3.7 Idadi ya Wahusika na Jukumu lao katika Hadithi, "Sina Rafiki" (Wahab, 1977)....118
3.3.8 Idadi ya Wahusika na Jukumu lao katika Hadithi, "Mke Wangu" (Muhammed, 1977)....121
3.4 Uthabiti wa Wahusika Wakuu katika Hadithi Teule....124
3.5 Mshabaha wa Lugha ya Wahusika Wakuu na Lugha ya Hadhira Lengwa katika Hadithi Teule....130
3.6 Kusadikika kwa Wahusika Wakuu na Uwazi wa Sababu za Matendo yao katika Hadithi Teule....134

3.7 Hitimisho.....140
SURA YA NNE 141
TATHMINI YA MAUDHUI YA HADITHI FUPI TEULE 141
4.1 Utangulizi.....141
4.2 Umuhimu wa Elimu.....142
4.3 Changamoto katika Ndoa.....144
4.4 Athari za Mapenzi na Uzinzi 146
4.5 Athari za Tamaa.....148
4.6 Nafasi ya Mwanamke katika Jamii 150
4.7 Athari ya Utabaka 151
4.8 Mila na Desturi katika Utamaduni.....153
4.9 Umuhimu wa Bidii.....155
4.10 Ukatili katika Jamii 158
4.11 Athari ya Utamaushi 159
4.12 Athari za Kisasi.....160
4.13 Nafasi ya Dini katika Jamii.....161
4.14 Hitimisho.....162
SURA YA TANO 164
HITIMISHO.....164
5.1 Utangulizi.....164
5.2 Muhtasari wa Utafiti 164
5.3 Matokeo ya Utafiti 166
5.4 Mchango wa Utafiti 167
5.5 Matatizo ya Utafiti 169
5.6 Mapendekezo 170
5.7 Hitimisho.....171
MAREJELEO 172

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli wa Mada

Shirika la utangazaji la BBC (*British Broadcasting Corporation*) ni shirika lenye makao makuu nchini Uingereza. Shirika hili la habari ndilo kubwa zaidi duniani na hutoa habari na taarifa mbalimbali kwa njia ya runinga, redio na intaneti (BBC, 2017). Baadhi ya malengo ya shirika hili ni kutoa habari, kuelimisha na kuburudisha. Kwa mujibu wa Potter (2012), lilianzishwa kama shirika la kibinafsi 1922 likijulikana kama *British Broadcasting Company Limited*. Kufikia mwaka wa 1927 lilibadilishwa na kuwa shirika la umma. Aidha, idhaa ya Kiswahili ilizinduliwa tarehe 27 Juni 1957 na matangazo yake yaliegemea habari kuhusu ukombozi wa mataifa ya Afrika na sherehe za baada ya kujipatia uhuru za nchi nyingi za Afrika kama vile: Tanganyika, Uganda, Kenya, Jamhuri ya kidemokrasia ya Congo, Rwanda na Burundi (BBC, 2017).

Kuanzia mwaka wa 1967 BBC ilianzisha mashindano ya hadithi fupi na zile zilizotokea kuwa bora zilisomwa hewani na hatimaye zikachapishwa katika mikusanyiko minne ambayo ni: *Mapenzi ni Kikohozi* (1970), *Vituko Duniani* (1970), *Pavumapo Palilie* (1971) na *Kinywa Jumba la Maneno* (1977). Hadithi hizi zilikuwa za waandishi mashuhuri kama vile: Said Ahmed Mohamed, Mohamed Suleiman Mohamed na Muhammed Said Abdulla mtawalia. Kwa mujibu wa Mazrui (2007), idhaa hii imechangia katika ukuzaji wa hadithi fupi ya Kiswahili Afrika Mashariki. Uchapishaji huu uliweka

msingi wa uandishi wa hadithi fupi za baadaye katika Kiswahili kwa sababu baadhi ya waandishi hawa kama vile: Said Ahmed Mohamed, Mohamed Suleiman Mohamed na Muhammed Said Abdulla bado wanachapisha kazi zao hadi sasa.

Mohamed (2002) anatoa shukrani kwa Idhaa ya Kiswahili ya BBC London na anakiri kuwa ndiyo ilichangia katika kukuza kipawa chake cha utunzi wa hadithi fupi baada ya baadhi ya hadithi zake kushinda, kusomwa hewani na hatimaye kuchapishwa. Anaongeza kuwa BBC hawakutambua kuwa walizidi kumtia hamu ya utunzi wa hadithi fupi aliyokuwa nayo tangu utotoni mwake. Hata hivyo, katika miaka ya 1970 kipindi cha mashindano ya hadithi fupi cha BBC kilisitishwa na kwa bahati nzuri anasema kuwa alipata nafuu ya kutovunjika moyo pale Idhaa ya Kiswahili ya redio ya Ujerumani ilipoanzisha mashindano kama yale ya BBC ya hadithi fupi.

Bertoncini (1998) anasema kwamba hadithi zilizoko katika mikusanyiko hii minne maarufu kama *Hekaya za Kuburudisha* ni hadithi zenye mvuto mkubwa ambazo zilichapishwa na shirika la uchapishaji la Longman likishirikiana na BBC kuanzia 1970 hadi 1977. Kwa maoni yake, hadithi ya Mohamed Suleiman Mohamed yenye mada “Siku ya Arobaini” kutoka mkusanyiko wa *Mapenzi ni Kikohozi* (1970) ndiyo yenye mvuto mkubwa zaidi. Anaendelea kusema kuwa Mohamed Suleiman katika hadithi hii amedhihirisha utajiri wa lugha alionao unaomsukuma kusanii kazi safi. Hakueleza vipengele vya kifasihi vilivyomfanya kufikia uamuzi wa kusifu hadithi “Siku ya Arobaini”

kutoka mkusanyiko wa *Mapenzi ni Kikohozi* (1970) ndiposa utafiti huu unakusudia kutathmini hadithi fupi zilizowasilishwa katika BBC kwa mtazamo wa Edgar Allan Poe (1842; 1846) na Leech (1969).

Msokile (1992) anaeleza kwamba ubora wa hadithi fupi utokana na: Kwanza, kuwepo kwa tukio moja lililopewa uzito kuliko tukio jingine lolote. Pili, ubunifu wa mhusika mkuu anayejitokeza sana na wahusika wengine wasielezwe kwa mapana. Tatu, msuko ambao unadhihirisha upangaji mzuri wa maelezo yanayotiririka mwanzoni mwa tukio hadi mwishoni mwa tukio (Barger, 2008). Nne, maelezo yanayotumia muda mfupi iwezekanavyo. Kwa mujibu wa Mohamed (2002), hadithi fupi inapokuwa fupi mno hupoteza vipengele vingine muhimu vya fani. Mohamed (1995) akimrejelea Mohamed Suleiman Mohamed katika hadithi ya "Mateso" inayopatikana katika mkusanyiko wa *Mapenzi ni Kikohozi* (1970), anaeleza kwamba ubora wa utanzu wa hadithi fupi utokana na uwezo wa hadithi kuwa na sifa za kifasihi simulizi hasa baadhi ya sifa za kitenzi na mighani. Finnegan (1970) anataja sifa za kitendi ni kama vile: kuwepo kwa maudhui na uunganifu ambapo ni vyema hadithi iwe imeunganika vizuri katika mtiririko wake na msuko wake wa matukio.

Kwa mujibu wa Mbatiah (2000), hadithi fupi inastahili kuwa na uwezo wa kugusa hisia za msomaji jambo ambalo humshawishi kutathmini zaidi maisha na kuthamini mazingira ya jamii atokayo. Aidha, Mbatiah anamnukuu Edgar Allan Poe (1842; 1846) aliyetoa kanuni za utunzi wa hadithi fupi. Kanuni hizi

ni: hadithi fupi iweze kusomeka katika kikao kimoja, kujengwa kwa wazo moja kwa kujikita na mgogoro mmoja, mgogoro uendelezwe kwa mjengo wa ploti bora na uteuzi mzuri wa lugha. Hata hivyo, anakiri haiwezekani watunzi wote kufuata kanuni fulani kwa sababu utanzu wa hadithi fupi ni mnyumbufu sana.

Kwa mujibu wa Omar (2010), ubora wa hadithi fupi utokana na uwezo wake kukosa uchangamano kama katika riwaya, mwandishi au msimulizi kuzingatia tukio moja, kuwepo kwa mhusika mkuu na wahusika kuwa wachache na wasipambanuliwe kwa mapana (Chokocho na Kayanda, 2016), muda wa kueleza tukio uwe mfupi ukilinganishwa na muda wa riwaya, ukolezaji wa taharuki ili kuvuta makini ya msomaji, msuko sahili wa hadithi na hadithi iweze kusomwa katika kikao kimoja.

Utafiti huu ulitathmini hadithi fupi zilizowasilishwa katika BBC kwa mtazamo wa Edgar Allan Poe (1842; 1846) na Leech (1969) hasa hadithi za waandishi wa Afrika Mashariki zilizosomwa hewani na hatimaye kuchapishwa katika mikusanyiko mbalimbali yenye mada maarufu *Hekaya za Kuburudisha*.

1.2 Suala la Utafiti

Shirika la BBC kupitia idhaa ya Kiswahili ya BBC limechangia katika ukuzaji wa utanzu wa hadithi fupi. Mchango wake unatokana na hoja kuwa kuna hadithi ambazo baada ya kushinda mashindano ya hadithi fupi zilisomwa hewani na mtangazaji maarufu Dalail Mzee na baadaye zikachapishwa na

shirika la Longman kuanzia mwaka wa 1970 hadi 1977 (Longman, 1970). Aidha, utafiti wa kitaaluma haujafanywa katika hadithi fupi hizi za awali zaidi kuandikwa, kusomwa hewani na kuchapishwa.

Utafiti wa wasomi wa hadithi fupi umekuwa ukijikita katika hadithi fupi zilizochapishwa kuanzia miaka ya themanini na kuendelea. Aidha, utanzu wa hadithi fupi ni utanzu ambao unastahili kuchunguzwa kwa kina zaidi hususani kwa kutathmini hadithi fupi zilizowasilishwa katika BBC kwa mtazamo wa Edgar Allan Poe (1842; 1846) na Leech (1969). Hadithi hizi zilisomwa hewani baada ya kushinda mashindano ya hadithi fupi yaliyoanzishwa na BBC na baadaye zilichapishwa katika mikusanyiko minne ambayo ni: *Mapenzi ni Kikohozi* (1970), *Vituko Duniani* (1970), *Pavumapo Palilie* (1971) na *Kinywa Jumba la Maneno* (1977).

Kwa vile kuna pengo katika utathmini wa hadithi fupi zilizowasilishwa katika idhaa ya Kiswahili ya BBC, utafiti huu ulitathmini muundo wa hadithi fupi zilizowasilishwa katika BBC kwa kuzingatia mtazamo wa Edgar Poe (1842; 1846) kwa sababu baadhi ya hadithi hizi kama vile “Mke Wangu” iliyoko katika mkusanyiko wa *Kinywa Jumba la Maneno* (1977) imechapishwa katika mkusanyiko wa *Damu Nyeusi* (2007). Vilevile, utafiti ulitathmini usawiri wa wahusika katika hadithi ili kufanikisha maudhui ya hadithi hizi kwa sababu baada ya hadithi kushinda mashindano; zilisomwa hewani kabla ya kuchapishwa. Kuongezea, baadhi ya waandishi ambao hadithi zao zilisomwa

hewani na hatimaye kuchapishwa bado wanachapisha hadithi zao katika kipindi hiki cha mwamko mpya au karne hii tuliyoko.

1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulijibu maswali yafuatayo:

i. Je, hadithi zilizowasilishwa na BBC 1970 hadi 1977 zilikuwa na muundo upi?

ii. Wahusika wa hadithi fupi zilizowasilishwa na BBC walisawiriwa vipi?

iii. Ni maudhui yapi yaliyowasilishwa katika hadithi fupi zilizowasilishwa na BBC?

1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulikusudia kutimiza malengo yafuatayo:

i. Kuchanganua muundo wa hadithi fupi zilizowasilishwa na BBC 1970 hadi 1977.

ii. Kueleza usawiri wa wahusika katika hadithi fupi zilizowasilishwa na BBC.

iii. Kubainisha maudhui katika hadithi fupi zilizowasilishwa na BBC.

1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Mshawasha wa kuchagua mada hii ulitokana na hoja kuwa utanzu wa hadithi fupi umeanza kushughulikiwa katika ngazi za kitaaluma juzi tu (Mohochi, 2018). Kwanza, mtafiti aliamua kutathmini hadithi fupi zilizowasilishwa

katika BBC kwa kuzingatia mtazamo wa Edgar Allan Poe (1842; 1846) na Leech (1969) hadi kupelekea hadithi hizi kushinda, kusomwa hewani na hatimaye kuchapishwa. Utathmini ulizingatia muundo wa hadithi hizi kwa kujikita na misingi ya hadithi fupi iliyowekwa na Edgar Poe (1842; 1846), uchanganuzi wa wahusika pamoja na utathmini wa maudhui katika hadithi teule.

Pili, mtafiti alikusudia kujenga vigezo vya kuzingatia katika kusanii hadithi fupi, kuelewa usawiri wa wahusika na uwasilishaji wa maudhui ili kusaidia waandishi wa baadaye katika kusuka kazi zao. Kwa namna hii, mtafiti aliangalia misingi iliyowekwa na hadithi hizi za awali kuchapishwa zilizoko katika mikusanyiko minne ya awali kuchapishwa baada ya kuibuka kuwa na mvuto mkuu wa kisanaa. Baadhi ya waandishi wa hadithi hizi kama vile; Said Ahmed Mohamed, Muhammed Said Abdulla na Mohamed Suleiman Mohamed bado wanachapisha kazi zao katika kipindi hiki cha mwamko mpya.

Tatu, utanzu huu umekuwa mojawapo ya utanzu unaofaa kwa wasomi ambao kazi zao zinashindaniwa na mashirika mbalimbali ya uchapishaji. Ili kuimarisha ubunifu wa hadithi fupi, mtafiti alichagua kuhakiki mikusanyiko ya awali zaidi ambayo haijafanyiwa utafiti kama huu. Mikusanyiko hii ni: *Mapenzi Kikohozi* (1970) yenye hadithi kumi, *Vituko Duniani* (1970) yenye hadithi nane, *Pavumapo Palilie* (1971) yenye hadithi nane na *Kinywa Jumba la Maneno* (1977) yenye hadithi nane.

Utafiti huu ulinuia kuwafaidi wapenzi wa fasihi ya Kiswahili hususani wapenzi wa hadithi fupi ya Kiswahili kwani mtafiti alitarajia ya kwamba kazi hii itawachochea watafiti wengine kuangazia vipengele tofauti na vilivyoangaziwa na mtafiti katika mikusanyiko hii minne ya awali zaidi kuchapishwa. Mikusanyiko hii inabeba hadithi fupi zilizoshinda katika mashindano ya hadithi fupi yaliyoandaliwa na BBC.

1.6 Upeo na Mipaka

Utafiti huu ulijikita katika kutathmini hadithi fupi zilizowasilishwa katika BBC. Ijapokuwa kuna mashirika mbalimbali katika uwanja wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA): Mtafiti alijikita na shirika la BBC kwa madhumuni ya kufanikisha malengo ya utafiti huu kwa sababu idhaa ya Kiswahili ya BBC ndiyo ya kwanza kuanzisha mashindano ya hadithi fupi, kuzisoma hewani na hatimaye kuzichapisha (Mohamed, 2002). Uteuzi huu ulitegemea kusudio la kutathmini hadithi fupi zilizowasilishwa na shirika la BBC kwa kuzingatia mtazamo wa Edgar Poe (1842; 1846) na Leech (1969).

Mikusanyiko ya hadithi fupi za Kiswahili iliyochapishwa ni mingi walakini utafiti huu ulishughulikia mikusanyiko minne ya awali zaidi ili kujibu suala la utafiti. Mkusanyiko wa kwanza *Mapenzi ni Kikohozi* (1970) una hadithi kumi, wa pili *Vituko Duniani* (1970) una hadithi nane, wa tatu *Pavumapo Palilie* (1971) una hadithi nane na wa mwisho *Kinywa Jumba la Maneno* (1977) una hadithi nane. Aidha, mtafiti alitumia mbinu kusudio katika kuteua hadithi zilizoafiki mahitaji ya utafiti huu. Idadi ya hadithi iliwakilisha hadithi za

waandishi ambao bado wanachapisha kazi zao mpaka sasa na zile ambazo maudhui yake yanajitokeza katika kipindi hiki cha mwamko mpya.

Hadithi zilizoandikwa na wanawake ni mbili katika mikusanyiko yote minne tuliyohakiki na hivyo basi tuliziteua. Katika mkusanyiko wa *Mapenzi ni Kikohozi* (1970) kuna hadithi moja ya Fauziya Salim yenye mada "Kusoma na Kupenda" (uk 40-45). Vilevile, katika mkusanyiko wa *Kinywa Jumba la Maneno* (1977) tulipata hadithi moja ambayo mwandishi wake ni Zainab Burhani. A. Wahab (uk 1-11) yenye kichwa "Sina Rafiki".

Vilevile, mtafiti alishughulikia vigezo maalumu vilivyomsaidia kufanikisha malengo yake. Vigezo hivi ni; kwanza, kutathmini muundo wa hadithi kwa mtazamo wa Edgar Poe (1842; 1846). Pili, uchanganuzi wa usawiri wa wahusika katika hadithi teule. Tatu, ubora wa maudhui ya hadithi kiasi cha kuzifanya kushinda katika mashindano, kuwasilishwa hewani na hatimaye kuchapishwa na BBC ikiwa kama mhariri. Maudhui haya ni kama vile: elimu, ndoa, mapenzi na uzinzi, tamaa, nafasi ya mwanamke katika jamii, utabaka, utamaduni, bidii, ukatili, utamaushi, kisasi na dini.

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Baadhi ya wasomi walikubaliana kuwa hadithi fupi kama utanzu wa fasihi andishi uliweza kushughulikiwa kiakademia katika karne ya kumi na tisa na utanzu huu uliendelea kupitia mabadiliko mbalimbali (Reid, 1977; Mbatiah, 2000 na Mohamed, 2002). Kufikia sasa karne ya ishirini na moja tafiti

mbalimbali zimefanywa, kwa mfano: Mohochi (1995), Mukopi (2005), Mohamed (2008), Kaui (2011), Muusya (2012), Onchangu (2013), Musili (2015), Nyamu (2015), Wafula (2015) na Tanui (2018).

Mohochi (1995) alishughulikia fani katika hadithi fupi za Kiswahili. Hadithi fupi ambazo alihakiki ni *Wasubiri Kifo* ya Kezilahabi, *Siri ya Bwanyenye* ya Mulokozi, *Kicheko cha Ushindi* ya Mohamed S. Mohamed na *Msiba wa Pamoja* ya Said A. Mohamed. Mtafiti alichanganua vipengele vya fani katika hadithi hizi ikiwemo lugha. Alilenga kudhihirisha kuwa hadithi fupi ni utanzu maalumu wa fasihi wenye sheria mbalimbali zinazoongoza ujenzi wa fani yake. Mwelekeo wa utafiti huu ni tofauti kwani ulinuia kutathmini hadithi fupi zilizowasilishwa katika BBC kwa kuzingatia misingi iliyowekwa na Edgar Poe (1842; 1846) na Leech (1969).

Utafiti mwingine ni wa Mukopi (2005) kuhusu hadithi fupi za kisasa za Kiswahili kama utanzu mahuluti. Mikusanyiko aliyohakiki katika utafiti wake ni: *Pendo la Heba na Hadithi Nyingine* (1997), *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine* (2000) na *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004). Mtafiti alichunguza namna sifa za usimulizi na sifa za uandishi zinavyochangiana ili kuzua utanzu wa hadithi fupi ya Kiswahili ya kisasa. Utafiti wake uliongozwa na nadharia ya mwingiliano matini iliyoasisiwa na Julia Kristeva. Nadharia hii ilitumika kuonyesha mwingiliano kati ya sifa za uandishi na usimulizi wa ngano za kale. Alikana kuwa utanzu wa hadithi fupi ni kimelea cha masimulizi ya ngano za kale. Utafiti huu una mwelekeo tofauti

kabisa kwa maana ulikusudia kutathmini hadithi fupi zilizowasilishwa katika BBC kwa kuzingatia mtazamo wa Edgar Poe (1842; 1846) na Leech (1969). Pili, utafiti huu ulikusudia kuchanganua usawiri wa wahusika kama mojawapo ya vipengele vya uhakiki katika mtindo ili kufanikisha maudhui lengwa.

Vilevile, utafiti wa Mohamed (2008) ulishughulikia usemezano kama mkakati wa kufahamu riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001), *Bina-Adamu!* (2002) na mkusanyiko wa hadithi fupi wa *Sadiki Ukipenda na Hadithi Nyingine* (2002). Mtafiti aliongozwa na nadharia ya usemezano ya Mikhail Mikhailovich Bakhtin (1895-1975) iliyochukuliwa kama mkakati wa kufahamu kazi husika. Kwanza, utafiti huu unatofautiana na wa Mohamed kwa sababu ulijikita na utanzu wa hadithi fupi pekee. Pili, utafiti huu ulinuia kutathmini muundo wa hadithi fupi zilizowasilishwa katika BBC kwa kuzingatia misingi iliyowekwa na Edgar Poe (1842; 1846). Tatu, utafiti huu ulizingatia kipengele cha uhakiki cha usawiri wa wahusika katika nadharia ya mtindo iliyoasisiwa na Leech (1969) kwa sababu Edgar Poe hakukieleza kwa mapana ili kutimiza malengo ya utafiti.

Katika utafiti wa Kaui (2011), mtafiti alitathmini usimilisho wa riwaya na hadithi fupi kwa wanafunzi wa sekondari nchini Kenya. Usimilisho huu ulijihusisha na riwaya ya *Utengano* (1980) na *Siku Njema* (1996) na mkusanyiko wa *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004) na *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (2007). Mtafiti alihakiki hadithi zote katika mikusanyiko yote miwili. Hata hivyo, katika mkusanyiko wa *Damu Nyeusi na*

Hadithi Nyingine (2007) ipo hadithi ya Muhammed Said Abdulla iitwayo *Mke wangu* katika (uk 2-9) ambayo ni mojawapo ya hadithi iliyosomwa hewani katika idhaa ya Kiswahili ya BBC inayopatikana katika mkusanyiko wa *Kinywa Jumba la Maneno* (1977) (uk 48-57). Mtafiti alidhamiria kubainisha dhana, historia, mbinu na matatizo ya usimilisho na kupendekeza njia za kutatua matatizo hayo. Kutokana na utafiti wake, usimilisho ni mwendelezo wa mwingiliano matini na tanzu. Katika uchunguzi wa tanzu hizi za riwaya na hadithi fupi, sifa za tamthilia zilizodhihirika ni kama vile: muundo wa kimazungumzo, uzungumzaji nafsia, utendaji na miktadha ya usemaji kando. Utafiti huu ulichukua mkondo tofauti na wake kwa maana mahususi ya utafiti huu ulitathmini hadithi fupi zilizowasilishwa katika BBC kwa kuzingatia misingi iliyowekwa na Edgar Poe (1842; 1846) na Leech (1969).

Aidha, Muusya (2012) alishughulikia mandhari katika hadithi fupi: ulinganishaji wa mkusanyiko wa *Pendo la Heba na Hadithi Nyingine* (1997) na *Mizungu ya Manabii na Hadithi Nyingine* (2010). Utafiti wake uliangazia kipengele cha mandhari kama kipengele muhimu cha uhakiki. Hata hivyo, utafiti huu ulinuia kufahamu usawiri wa wahusika kama mojawapo ya vipengele vya mtindo ili kufanikisha uwasilishaji wa maudhui. Kwa njia hii, utafiti ulitathmini hadithi fupi zilizowasilishwa katika BBC kwa kuzingatia misingi iliyowekwa na Edgar Poe (1842; 1846) na Leech (1969).

Utafiti wa Onchangu (2013) uliangalia mtindo katika riwaya na hadithi fupi za Clara Momanyi kwa kurejelea riwaya ya *Tumaini* (2006), hadithi fupi ya

“Ngome ya Nafsi” katika *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004) na “Masazo ya ufisadi” na “Mtumbwi wa Maskini” katika *Takrima Nono na hadithi Nyingine* (2011). Utafiti wake ulilenga kuchunguza uteuzi na mbinu mbalimbali za lugha anayotumia Clara Momanyi katika kuwasilisha ujumbe kusudiwa. Tofauti na utafiti huu ni kwamba; kwanza, mtafiti alitathmini hadithi fupi zilizowasilishwa katika BBC kwa kuzingatia misingi iliyowekwa na Edgar Poe (1842; 1846) na Leech (1969). Pili, mtafiti alijikita na kipengele cha usawiri wa wahusika katika uhakiki wake. Tatu, mtafiti alizingatia hadithi fupi za kwanza kuchapishwa kisha za waandishi tofauti tofauti si mwandishi mmoja kama alivyofanya Onchangu.

Athari ya mbinu rejeshi katika hadithi fupi za Kiswahili iliangaziwa na Musili (2015). Mtafiti alihakiki mkusanyiko wa *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine* (2000) na *Kunani Marekani na Hadithi Nyingine* (2011). Uteuzi wa mikusanyiko hii ulitokana na matumizi mengi ya mbinu rejeshi katika mikusanyiko teule. Tofauti na utafiti wa Musili, utafiti huu ulinuia kutathmini hadithi fupi zilizowasilishwa katika BBC kwa kuzingatia misingi iliyowekwa na Edgar Poe (1842; 1846) na Leech (1969). Kuongezea, utafiti ulichanganua suala la usawiri wa wahusika katika kufanikisha maudhui kiasi cha kusababisha hadithi fupi hizi kufikia ubora wa juu na hatimaye kuchapishwa baada ya kusomwa hewani. Hata hivyo, utafiti wake ulifaa katika kupata data kuhusu baadhi ya maelezo ya kijumla ya nadharia ya mtindo kwa sababu utafiti huu ulitumia nadharia ya mtindo.

Nyamu (2015) aliangazia usawiri wa mandhari katika hadithi fupi na umuhimu wake katika kuendeleza vitushi katika hadithi fupi. Mtafiti alihakiki mkusanyiko wa *Maskini Milionea na Hadithi Nyingine* (2012) na *Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine* (2006). Utafiti wake ulidhamiria kuchambua namna mandhari inavyosawiriwa katika kuendeleza vitushi katika hadithi fupi. Utafiti wake uliongozwa na nadharia changamano; nadharia ya uhalisia ya Wilhelm Friedrich Hegel (1770-1831) na ile ya uhalisiajabu iliyoasisiwa na Franz Roh (1890-1965). Utafiti huu ulitumia nadharia ya mtindo iliyoasisiwa na Leech (1969) katika kutalii kipengele cha wahusika na uhusika wao. Aidha, utafiti huu ulitathmini hadithi fupi zilizowasilishwa katika BBC kwa mtazamo wa Poe (1842; 1846).

Mgongano wa tamaduni katika hadithi fupi za Kiswahili uliangaziwa na Wafula (2015). Kazi alizoteua katika utafiti huu ni: *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004), *Kiti cha Moyoni na Hadithi Nyingine* (2007), *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine* (2000) na *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (2007). Nadharia iliyoongoza utafiti wake ni ile ya udhanaishi iliyoasisiwa na Soren Kierkegaard (1813-1855). Aidha, mtafiti alipendekeza utafiti wa nyanjani kufanywa na kupima ukweli wa yale yameandikwa na waandishi. Utafiti wake unatofautiana na huu kwa sababu malengo ya utafiti wake yanazunguka suala la mgongano wa tamaduni katika jamii ilhali utafiti huu ulihakiki mikusanyiko teule kwa kuangalia iwapo hadithi teule ziliafiki mtazamo wa hadithi fupi uliowekwa na Poe (1842; 1846) na usawiri wa wahusika katika kujenga maudhui ya hadithi.

Utafiti wa Tanui (2018) uliangalia usawiri wa maudhui yenye kufunza wanafunzi wa vyuo vikuu maadili mema kwa kutathmini mkusanyiko wa *Alidhani Kapata* (2007) na *Damu Nyeusi* (2007). Utafiti wake ulilenga kufunza maadili yanayofaa miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu ili kutoa mwelekeo juu ya maisha ya wanafunzi wa vyuo ambao ni sehemu ya jamii yetu. Tofauti na utafiti wa Tanui, utafiti huu ulitathmini hadithi fupi zilizowasilishwa katika BBC kwa kuzingatia misingi iliyowekwa na Poe (1842; 1846) na Leech (1969). Vilevile, utafiti ulitathmini suala la usawiri wa wahusika katika kufanikisha dhamira na maudhui ambayo bado yanadhihirika katika kipindi hiki cha mwamko mpya. Hata hivyo, utafiti wake ulifaa katika uchanganuzi wa maudhui kwa sababu yeye pia alitathmini maudhui katika hadithi fupi teule ya "Mke Wangu" iliyoko kwenye mkusanyiko wa *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (2007) na vilevile kwenye mkusanyiko wa *Kinywa Jumba la Maneno na Hadithi Nyingine* (1977) ambapo ilichapishwa awali zaidi.

Isitoshe, Makena (2018) alichunguza uwasilishaji maudhui katika hadithi fupi za Said A. Mohamed. Utafiti wake ulishughulikia vipengele vya fani vya mandhari, wahusika, mianzo na vimalizio vinavyochangiana kukamilishana ili kuwasilisha maudhui katika hadithi fupi za Said A. Mohamed. Mtafiti alitumia Nadharia ya Ummuundo iliyowekewa misingi na De Saussure (1957) kuchambua vipengele vya fani. Mada za hadithi fupi alizochunguza ni; "Sadiki Ukipenda", "Ngondo Pangoni", "Uhuru wa Subira", "Mwungwana", "Mhanga wa Mwamamaua" na "Njia Fupi" zilizoko katika mikusanyiko ya

Sadiki Ukipenda na Hadithi Nyingine (2002), *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine* (2005) na *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine* (2005) mtawalia. Tofauti na utafiti wake uliojikita na hadithi fupi za Said A. Mohamed pekee, utafiti huu ulijikita na tathmini ya hadithi fupi teule za waandishi mbalimbali za awali zaidi kuchapishwa katika BBC hasa miaka ya sabini kwa mtazamo wa Poe (1842; 1846) na Leech (1969).

Kutokana na tafiti hizi, ilibainika kuwa kufikia sasa mwaka wa 2021 hakuna utafiti wa kina uliofanywa ili kutathmini hadithi fupi zilizowasilishwa katika BBC kwa kuzingatia mtazamo wa Edgar Allan Poe (1842; 1846) na Leech (1969). Hivyo basi, utafiti mwingi uliofanywa kuhusu hadithi fupi ulikosa kuziba pengo la kutathmini hadithi fupi za waandishi wa Afrika Mashariki walioanza kuchapisha kazi zao miaka ya sabini na bado wanachapisha hadi sasa. Katika kutaka kuziba pengo hili, ilimbidi mtafiti kutathmini hadithi fupi zilizowasilishwa katika BBC kwa kuangalia iwapo hadithi teule ziliafiki misingi iliyowekwa na Poe (1842; 1846) na Leech (1969). Vilevile, mtafiti alichanganua usawiri wa wahusika katika kujenga maudhui ya hadithi. Kuongezea, watafiti wengi walishughulikia mikusanyiko ya kisasa tofauti na utafiti huu ambao uliangazia mojawapo ya mikusanyiko ya awali kabisa kuchapishwa hapa Afrika Mashariki.

1.8 Misingi ya Nadharia

Kazi ya kifasihi inaweza kuhakikiwa kupitia nadharia mbalimbali walakini utafiti huu ulitumia misingi ya nadharia ya hadithi fupi kwa mujibu wa Poe (1842; 1846) na nadharia ya mtindo ya Leech (1969) ili kutimiza malengo ya utafiti pamoja na kujibu suala la utafiti. Misingi ya nadharia ya hadithi fupi iliyowekwa na Poe na nadharia ya mtindo inaonekana kuwa faafu katika kusukuma utafiti huu kwa kuhakiki hadithi teule katika mikusanyiko ambayo mtafiti atateua.

1.8.1 Misingi ya Nadharia ya Hadithi Fupi kwa Mtazamo wa Poe (1842; 1846)

Misingi ya nadharia ya hadithi fupi ya Poe (1842; 1846) kwa kiasi fulani ni ya kimuundo kwa sababu inaelekeza namna hadithi fupi inastahili kusukwa ili kufikia ubora wake. Kwa mujibu wa Nayef (2013), Edgar Allan Poe aliweka misingi ya hadithi fupi kupitia makala yake *Review of Twice-Told Tales* (1842) na *The Philosophy of composition* (1846). Kwanza, Poe alieleza kwamba utanzu wa hadithi fupi unastahili kusomwa na kueleweka kwa muda usiozidi saa moja. Pili, hadithi fupi inastahili kuwa na nguvu za kifasihi za kuteka nafsi ya msomaji. Tatu, ploti ya hadithi fupi isukwe kwa ubunifu unaodhihirisha mtiririko wa mawazo. Kuongezea, hadithi fupi ijikite na tukio moja tu. Vilevile, mhusika mkuu awe mmoja anayejitokeza kuwa muhimu zaidi tofauti na wahusika wengine wachache ambao hawakuzwi sana. Sita, upeo wa hadithi fupi ujitokeze vyema kutokana na mpangilio mzuri wa matukio. Sentensi katika hadithi fupi ziakifishwe ipasavyo ili kuepuka utata

katika maana lengwa. Mwisho, hadithi iwe na mianzo na miishio yenye kiwango kikubwa cha ubunifu ili kuvuta makini ya msomaji au msikilizaji.

Hadithi fupi inastahili kuwa na uwezo wa kugusa hisia za msomaji ili kumshawishi kutathmini zaidi maisha na kuthamini mazingira ya jamii atokayo (Mbatiah, 2000 na Iribemwangi, 2007). Aidha, Mbatiah anamnukuu Poe (1842; 1846) aliyetoa kanuni za utunzi wa hadithi fupi. Kanuni hizi ni: hadithi fupi iweze kusomeka katika kikao kimoja, kujengwa kwa wazo au hisia moja kwa kujikita na mgogoro mmoja, mgogoro uendelezwe kwa mjengo wa ploti bora na uteuzi mzuri wa lugha ambayo itavuta makini ya msomaji au msikilizaji.

Kutokana na maelezo haya, utafiti huu ulitathmini hadithi fupi zilizowasilishwa katika BBC kwa kutegemea mihimili ifuatayo:

Kwanza, hadithi fupi inastahili kuwa na mtiririko bora wa mawazo ambayo yanaweza kusomwa katika kikao kimoja. Mawazo ya mwandishi au msimulizi yanafaa kukosa kizungumkuti kingi ili kazi yake iweze kuvutia hadhira (Poe, 1842; 1846 na Iribemwangi, 2007).

Pili, hadithi fupi inastahili kujenga tukio moja katika kuwasilisha maudhui lengwa kwa kujikita katika mgogoro mmoja tu. Tukio moja hufanya msomaji au msikilizaji kuelewa na kukumbuka maudhui kwa urahisi (Poe, 1842;1846).
Tatu, ploti katika hadithi fupi inastahili kujengwa vyema kutokana na utatuzi mzuri wa mgogoro (Poe, 1842;1846). Forster (1927) anasisitiza kuwa ploti

huhitaji upevu wa hali ya juu katika uteuzi wa lugha ili ujumbe kusudiwa kueleweka. Anaongezea kuwa ploti inaposukwa vyema hukuza uwezo wa msomaji au msikilizaji kukumbuka hadithi husika.

Nne, hadithi fupi inastahili kutumia lugha kwa haiba ili kuweza kunasa hisia za msomaji au msikilizaji (Poe, 1842;1846). Lugha inafaa kukolea mbinu kama ya taharuki ili kumvutia msomaji au msikilizaji aendelee kusoma au kusikiliza (Omar, 2010).

Misingi ya Edgar Allan Poe imejikita zaidi na suala la muundo wa hadithi fupi; mwelekeo ambao umewaathiri sana wanafasihi wa kimagharibi na Marekani (Mbatiah, 2000). Upungufu wake ni kwamba hakueleza vizuri aina ya wahusika na dhana ya wahusika hao katika kukuza hadithi fupi. Ili kufidia upungufu huu, utafiti ulihitaji nadharia ya kimtindo ili kueleza kikamilifu kipengele cha usawiri wa wahusika na uhusika wao.

1.8.2 Nadharia ya Mtindo kwa Ujumla

Nadharia hii iliasisiwa na Geoffrey Leech. Leech (1969) alishughulikia mtindo katika kuchanganua matini za kifasihi. Msukumo wa kazi yake ulitokana na maoni ya wanaisimu na waitifaki walioshikilia hoja kuwa uhakiki wa kifasihi hutofautiana na hauna mahusiano na uhakiki wa kiisimu. Aliongeza kuwa ni kupitia vipengele vya ukiushi ndiposa mchanganuzi wa matini ya kifasihi anaweza kufanya uhakiki ipasavyo. Vipengele hivi ni: Namna au jinsi ya usimulizi, uteuzi wa msamiati, tamathali za semi ateuazo msanii, lugha ya

msanii, namna ya kuhitimisha hadithi, mpangilio wa matukio, usawiri wa wahusika na uhusika na taswira apendayo kujenga.

Coombes (1953) anakiri kuwa lugha ni kipengele muhimu katika uhakiki wa kazi za fasihi. Anasema lazima mhakiki achunguze mambo yanayodhihirika katika lugha inayotumiwa na msanii hadi kufanya kazi ivutie na ibainike kuwa kazi yenye ustadi. Wamitila (2003) anafafanua nadharia ya mtindo kama uchunguzi wa lugha na uchanganuzi wa namna mbalimbali za kuelezea matukio katika kazi za kifasihi. Anaongezea kuwa nadharia hii husaidia katika kuchanganua vipengele vya fani na maudhui.

Crystal na Davy (1969) wanaeleza mtindo katika fasihi kama mazoea fulani yanayorejelea utumikizi wa lugha ya msanii; ni ule upekee wa msanii katika kazi yake. Kwa mujibu wa Leech na Short (1981), mtindo ni jinsi ambavyo mtu fulani hutumia lugha kutegemea muktadha na lengo maalumu. Aidha, Leech (2013) anapinga ufafanuzi wa Bloch (1953) kuwa mtindo ni kukengeuka katika utumikizi uliozoeleka wa lugha. Wamitila (2003) anapoeleza kuhusu vipengele vya uhakiki vya hadithi fupi anafafanua istilahi “mtindo” kama mazoea ya msanii katika kuandika au kuzungumza anaposanii kazi yake. Mazoea haya ni kama vile: mpangilio wa matukio, lugha ya msanii, namna ya kuhitimisha hadithi, usawiri wa wahusika na uhusika na tamathali za semi ateuazo msanii. Anaongeza kuwa mtindo hudhihirika kwa njia zingine nyingi kando na alizoorodhesha. Kwake, mtindo ni mazoea ya wanasiasa au waandishi katika kazi zao.

Simpson (2004) anabainisha vipengele vya kimsingi vinavyostahili kutumika katika uhakiki unaoegemea umitindo. Vipengele hivi vinafafanuliwa zaidi na Wamitila (2008) ambaye ni mwandishi na mwendelezaji wa nadharia hii. Vipengele hivi vinahusu: Lugha ya kitamathali na mtindo, uteuzi na mtindo, sarufi na mtindo, usimulizi na mtindo, uchimuzi na mtindo, itikadi na mtindo, mtazamo na mtindo, muwala au mshikamano na mtindo na mazungumzo, mbinu za uwasilishaji usemi na mawazo na mtindo.

Kairu (2005) akimnukuu Ngara (1982) anaeleza mtindo kama jinsi ya kujieleza kwa kutumia lugha. Ngara anapendekeza mitazamo miwili katika uchunguzi wa kazi ya fasihi. Mtazamo wa kiisimu na mtazamo wa kifasihi. Mtazamo wa kiisimu huangazia: sarufi, aina za sentensi na muundo. Pili, kiwango cha maana lengwa katika msamiati na tamathali za usemi kama vile jazanda na methali. Tatu, maana ya matini na nne kiwango cha maandishi kinachohusu mambo kama rangi, alama zilizochapishwa, aya na uakifishaji. Mtazamo wa kifasihi huangalia: mtindo unaojumlisha jinsi matukio yamepangwa, wahusika na vipengele vingine vya fani kama vile lugha na vipengele vyake.

Kutokana na maelezo haya, inabainika kuwa dhana ya wahusika na uhusika iliyoelezwa awali kabisa na Leech (1969) ni muhimu katika utathmini wa ubora wa hadithi fupi. Umuhimu wake unabainika kutokana na dhana hii kuendelezwa na wataalamu mbalimabli.

1.8.2.1 Dhana ya Wahusika na Uhusika katika Uhakiki wa Kimtindo

Kutokana na maelezo haya ya kijumla kuhusu nadharia ya mtindo, inabainika kwamba suala la wahusika na uhusika wao lililoelezwa awali zaidi na Leech (1969) ni mojawapo ya vipengele vya mtindo. Ili kutimiza mojawapo ya malengo ya utafiti huu mtafiti alijikita na kipengele cha wahusika na uhusika wao katika kukuza hadithi fupi. Wanamtindo wanaeleza dhana ya wahusika na uhusika wao katika kukuza maudhui ya hadithi fupi kama ifuatavyo:

Kwanza, Mbatiah (2000) anaeleza kwamba wahusika wa hadithi fupi huwa wachache na hawakuzwi kwa mapana kama katika riwaya. Mwandishi hana nafasi ya kuwajenga wahusika kama wale wa riwaya. Wahusika huumbwa kwa maelezo mafupi lakini maangavu. Wanafaa kuumbwa kwa njia ambayo haitaathiri dhamira na maudhui (Iribemwangi, 2007).

Pili, kila mhusika katika hadithi anafaa kuwa na jukumu ambalo linajitokeza waziwazi. Jukumu la kila mhusika huwa na mchango katika kuipatia hadithi mtiririko bora unaochangia ujenzi wa maudhui.

Tatu, uthabiti wa wahusika katika matendo yao ni muhimu. Wahusika hawastahili kubadilikabadilika na endapo mabadiliko yao yataonekana basi kuwe na sababu yenye kuaminika.

Nne, lugha ya wahusika inapaswa kuwa na mshabaha na ile ya hadhira lengwa au wanajamii ambao kazi husika ya fasihi inakusudia kulenga. Ukuruba wa lugha ya wahusika na wanajamii husaidia katika uwasilishaji maudhui kwa njia sahili.

Tano, wahusika wanastahili kuwa wa kusadikika katika matendo yao na sababu za wanayotenda ziwe wazi na za kuaminika. Forster (1927) anasisitiza kuwa wahusika binadamu ndio hutumika sana kwa sababu ni mambo machache yanayofahamika kuhusu saikolojia ya wanyama.

Sita, Forster (1927) anaeleza kwamba wahusika katika hadithi huwa wa aina mbalimbali na kila mhusika ana jukumu lake. Dhamira ya msanii katika hadithi fupi ndiyo humuongoza katika uteuzi wa wahusika.

1.8.2.2 Aina ya Wahusika katika Hadithi Fupi

Hadithi fupi huwa na wahusika wachache walakini wahusika hawa huwa na majukumu mbalimbali na ndiposa tunapata aina mbalimbali ya wahusika. Kwa mujibu wa Forster (1927), hadithi fupi huwa na mhusika mkuu ambaye huhusishwa na takriban visa vyote katika hadithi. Mhusika huyu hujitokeza kutoka mwanzo hadi mwisho wa hadithi. Mhusika mkuu huenda akawa mmoja au wawili (Msokile, 1992).

Wahusika wasaidizi ni wale ambao hutumika katika kujenga mhusika mkuu. Hata hivyo, wahusika wasaidizi wanaweza kuwa na visa vyao lakini mahsusi yao huwa ni kujenga mhusika mkuu. Mbinu ya kisasa ya kusanii wahusika wasaidizi ni kuwajenga sambamba na mhusika mkuu huku wakihusishwa na migongano mbalimbali (Msokile, 1992).

Wahusika wadogo hutumika katika kujenga maudhui au mandhari na wakitolewa katika hadithi hawaathiri ploti. Wahusika hawa husawiriwa kwa kuhusishwa na tukio fulani lisilo na umuhimu mkubwa. Tukio linaweza kuwa kama mhusika huyu kutajwa kuwa amemuuzia mhusika fulani bidhaa (Msokile, 1993).

Vilevile, wahusika bapa ni wale wasiobadilika kutoka mwanzo wa hadithi hadi mwisho (Wamitila, 2008). Wahusika wa aina hii hawabadilishwi na mazingira au na matukio ya wakati wanayokutana nayo. Nia yao huwa ni kujenga tukio moja tu na hivyo basi hawawakilishi sifa halisia za binadamu. Wahusika bapa ni wa aina mbili; kwanza, wahusika bapa sugu ambao huonyesha msimamo wao kulingana na masimulizi ya msanii. Pili, wahusika bapa vielelezo ambao msimamo wao hujulikana kutokana na majina yao. Msanii hutumia mbinu ya majazi au lakabu kuwapa majina yanayooana na sifa zao.

Forster (1927) anaeleza wahusika mviringo kama wahusika wenye kukosa uthabiti kwani wao hubadilika kitabia katika hadithi. Mabadiliko yao hutokana na mabadiliko ya maudhui na mazingira.

Wahusika foili huwakilisha uhalisia ulioko katika mwanadamu (Msokile 1992). Wahusika hawa hutegemea wahusika mviringo na bapa ili kutoa sifa zao. Wao huwa katikati ya bapa na duara.

Dhana ya wahusika na uhusika wao pamoja na maelezo kuhusu aina ya wahusika ilisaidia mtafiti katika kuchanganua usawiri wa wahusika katika kukuza hadithi fupi zilizowasilishwa katika BBC. Mtafiti aliongozwa na mihimili ifuatayo:

Kwanza, wahusika katika hadithi fupi wanastahili kuwa wachache. Aidha, wanastahili kukuzwa kwa uthabiti na njia inayoeleweka ili kuweza kufanikisha lengo kuu la hadithi husika ambalo ni kuwasilisha dhamira na maudhui kwa usahili.

Pili, Kila mhusika anastahili kusawiriwa kwa njia bora ambapo jukumu lake linabainika. Aina ya mhusika katika hadithi fupi ndiyo hubainisha jukumu lake. Mhusika mkuu ana jukumu tofauti na mhusika mvirngo, msaidizi, mdogo, bapa sugu, bapa kieleleo, na foili (Forster, 1927 na Msokile, 1992).

Tatu, lugha ya wahusika inafaa kueleweka na hadhira au wanajamii ambao kazi husika inakusudia kulenga. Maudhui hueleweka iwapo hakuna utata unaozuka katika lugha ya wahusika na wanajamii au hadhira kusudiwa.

Nne, Matendo ya wahusika yanastahili kuwa ya kuaminika. Kusadikika kwa matendo ya wahusika humfanya msomaji au msikilizaji wa hadithi husika kuwa makini katika kuelewa lengo la msimulizi au msomaji (Forster, 1927).

1.9 Mbinu za Utafiti

Stokes na Wall (2014) wanaeleza mbinu za utafiti kama utumizi wa vifaa na ujuzi maalumu wa mtafiti katika kufanikisha utafiti wake. Utafiti huu ulilenga

vipengele vifuatavyo katika mbinu za utafiti: Mahali pa utafiti, muundo wa utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data, uwasilishaji wa matokeo na hitimisho.

1.9.1 Mahali pa Utafiti

Katika kufanikisha malengo ya utafiti huu, utafiti ulikuwa wa maktabani. Usomaji mpana maktabani ulizingatia mikusanyiko teule ya hadithi fupi ambayo ni: *Mapenzi ni Kikohozi* (1970), *Vituko Duniani* (1970), *Pavumapo Palilie* (1971) na *Kinywa Jumba la Maneno* (1977). Pili, usomaji wa historia ya idhaa ya Kiswahili ya BBC ulifanywa ili kuelewa hadithi fupi zilizosomwa hewani katika idhaa hii kikamilifu. Tatu, mtafiti alisoma tasnifu, makala, majarida, vitabu na kusakura mtandao ili kupata data komavu ya yaliyoandikwa kuhusu mada hii. Nnne, mtafiti alisoma kwa kina kuhusu misingi ya nadharia ya hadithi fupi kwa mtazamo wa Poe (1842;1846) na nadharia ya mtindo ya Leech (1969) ambazo ndizo nguzo kuu za utafiti huu.

1.9.2 Muundo wa Utafiti

Utafiti ni wa kimaelezo ukirutubishwa na ule wa kitakwimu. Mbinu ya kimaelezo ilitumika pale ambapo mtafiti alidondoa sentensi au matukio ya kimaelezo na kuyachanganua. Sentensi au matukio ya kimaelezo yaliyodondolewa katika hadithi teule na kuchanganuliwa ndiyo ilikuwa data ya mtafiti. Aidha, mbinu ya kitakwimu ilitumika pale ambapo mtafiti alichagua hadithi teule katika mikusanyiko hii na kuzichanganua. Mbinu ya kitakwimu ilitumika kuteua hadithi mbili katika kila mkusanyiko. Uteuzi wa

hadithi ulizingatia hadithi za waandishi ambao bado wanachapisha kazi zao hadi sasa na zile ambazo maudhui yake yanajitokeza katika kipindi hiki cha mwamko mpya. Mtafiti aliteua hadithi kwa kuzingatia malengo ya utafiti.

1.9.3 Uteuzi wa Sampuli

Sampuli iliteuliwa kwa kujikita kwenye mbinu kusudio. Kwanza, mtafiti alishughulikia utanzu wa hadithi fupi katika fasihi andishi kwa sababu utanzu huu umeanza kushughulikiwa katika ngazi za kitaaluma juzi tu (Mohochi, 2018). Pili, alitathmini mikusanyiko minne ya awali zaidi kuchapishwa kwa sababu haijafanyiwa utafiti wowote kama huu. Vilevile, mtafiti alitumia mbinu kusudio katika kuteua hadithi zilizoafiki malengo ya utafiti ili kupata data iliyokidhi mahitaji ya utafiti huu. Idadi ya hadithi iliwakilisha hadithi za waandishi ambao bado wanachapisha kazi zao mpaka sasa na zile ambazo maudhui yake yanajitokeza katika kipindi hiki cha mwamko mpya. Maudhui haya ni kama vile: elimu, ndoa, mapenzi, tamaa, nafasi ya mwanamke katika jamii, utabaka, utamaduni, bidii, ukatili, utamaushi, uzinzi, kisasi na dini. Pamoja na hayo, utafiti ulishughulikia kipengele cha uhakiki cha mtindo kilichojikita kwenye usawiri wa wahusika katika kufanikisha maudhui.

1.9.4 Ukusanyaji wa Data

Mtafiti alisoma kwa kina maktabani kwa kuzingatia hadithi teule katika mikusanyiko teule ili kupata data iliyohitajika. Ukusanyaji wa data maktabani ulisaidia katika kupata data yenye utoshelevu. Kwa kila hadithi teule mtafiti alichanganua muundo wake kwa kuzingatia mtazamo wa Edgar Poe, alieleza

usawiri wa wahusika katika hadithi teule kwa kuzingatia maoni ya wataalamu walioendeleza mtazamo wa Leech (1969) na ubainishaji wa maudhui yaliyowasilishwa. Sentensi au matukio ya kimaelezo yaliyotolewa katika hadithi teule na kuchanganuliwa ndiyo data ya kimsingi ya mtafiti.

1.9.5 Uchanganuzi wa Data

Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti pamoja na mwongozo utokanao na misingi ya hadithi fupi na ile ya nadharia ya mtindo hususani uhakiki uliorejelea kipengele cha usawiri wa wahusika. Kwanza, mtafiti alichanganua muundo wa hadithi fupi kwa mtazamo wa Edgar Poe. Pili, mtafiti alieleza usawiri wa wahusika katika hadithi fupi teule hususani kwa kurejelea nadharia ya mtindo. Usawiri wa wahusika ulizingatia: Aina ya wahusika, idadi ya wahusika na jukumu la wahusika, uthabiti wa wahusika, kueleweka kwa lugha ya wahusika na wanajamii na kuaminika kwa matendo ya wahusika. Mwisho, mtafiti alishughulikia suala la maudhui kaika hadithi teule. Mtafiti alibainisha maudhui ambayo bado yanajitokeza kwenye kazi zinazochapishwa katika kipindi hiki cha mwamko mpya.

1.9.6 Uwasilishaji wa Matokeo

Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kinathari. Mtafiti alitathmini hadithi fupi zilizowasilishwa katika BBC kwa mtazamo wa Edgar Allan Poe. Uwasilishaji uliongozwa na malengo ya utafiti yaliyorejelea mihimili ya misingi ya hadithi fupi kama ilivyowekwa na Edgar Poe pamoja na kipengele cha usawiri wa wahusika katika nadharia ya mtindo ili kufanikisha maudhui lengwa.

1.9.7 Hitimisho

Msingi wa utafiti huu ni sehemu hii ya kwanza. Sehemu hii imeshughulikia: Usuli wa mada, mtafiti ameangazia suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia na mbinu za utafiti. Sehemu hii ndiyo itakayojenga sehemu zitakazofuata. Sura ifuatayo imetathmini muundo wa hadithi fupi teule zilizowasilishwa katika vipindi vya redio vya idhaa ya Kiswahili ya BBC.

SURA YA PILI

TATHMINI YA MIUNDO YA HADITHI FUPI TEULE

2.1 Utangulizi

Sura hii inashughulikia miundo ya hadithi fupi zilizowasilishwa katika vipindi vya redio vya *British Broadcasting Corporation* (BBC). Katika kushughulikia miundo hiyo, mtafiti amezingatia mihimili ya nadharia ya hadithi fupi iliyoasisiwa na Poe (1842; 1846). Misingi ya Poe imeshughulikia zaidi suala la muundo wa hadithi fupi. Hivyo basi, misingi hii ndiyo imeongoza katika kutathmini miundo ya hadithi fupi teule katika mikusanyiko teule. Misingi yenyewe ni: Kwanza, hadithi fupi kuwa na mtiririko bora wa mawazo ambayo yanasomeka katika kikao kimoja. Pili, inapaswa kujenga tukio moja katika kuwasilisha maudhui lengwa kwa kujikita katika mgogoro mmoja tu. Tatu, ploti ijengwe vyema kutokana na utatuzi mzuri wa mgogoro (Poe, 1842; 1846 na Forster, 1927). Nne, lugha itumiwe kwa mvuto ili kuweza kunasa hisia za msomaji au msikilizaji kama vile matumizi ya taharuki. Tahakiki ya hadithi fupi teule katika kila mikusanyiko teule imebainishwa kwa kujikita katika mihimili hii. Kwa kufanya hivi, utafiti unalenga kuchanganua miundo ya hadithi fupi zilizowasilishwa katika vipindi vya redio vya BBC 1970 hadi 1977.

2.2 Mtiririko wa Mawazo katika Hadithi Fupi Teule

Kwa mujibu wa Iribemwangi (2007), mawazo ya mwandishi au msimulizi yanafaa kuwa sahili ili kufanikisha kazi ambayo ina mvuto kwa hadhira lengwa kutokana na mtiririko bora wa mawazo. Mawazo yanapopangika

vyema hufanikisha usomaji au usimulizi wa hadithi fupi katika kikao kimoja. Hata hivyo, hadithi fupi inastahili kuwa na mawazo ambayo yamepangika bila uchangamano na iruhusu kujifinya kwa mawazo kwa njia inayoeleweka ili iende haraka kiwakati, kimasafa, kimatukio na kimatendo (Mohamed, 1995). Mtiririko wa mawazo katika utathmini unaorejelea uhakiki wa hadithi fupi teule katika mikusanyiko teule umejikita na maelezo ya Poe (1846) pamoja na yale ya Njogu na Chimerah (1999) ambapo mawazo bora huelekezana kwenye usuluhisho wa kazi ya fasihi ili dhamira kubainika kwa uwazi au kwa namna sahili kama ifuatavyo:

2.2.1 Mtiririko wa Mawazo katika Hadithi, "Siku ya Arobaini" (Mohamed, 1970)

Kwanza, katika hadithi hii Sadiki anapokea barua kutoka kwa mkewe Bahati ingawa hana ufahamu kuwa aliyemwandikia ni mkewe. Ujumbe wa barua unamrai wakutane katika ufuo wa bahari wa *People's Beach*:

> ...tuonane hapo *People's* Beach, mnamo saa mbili za usiku kesho... (uk. 23).

Sadiki anadhani barua hiyo imetoka kwa Saida, msichana ambaye hukutana naye dirishani wakati akienda kazini. Anaficha barua hiyo na kuingia kwake ili mkewe Bahati asiione. Tamaa ya Sadiki inamtia matatani kwa sababu mwishowe mkewe anafanikiwa katika upelelezi wake wa kutaka kujua kama mumewe anamwendea kinyume katika maisha ya ndoa.

Hadithi hii inatumia lugha sahili inayofanikisha mtiririko bora wa mawazo yanayoweza kusomeka au kusikilizwa katika kikao kimoja huku dhamira

lengwa ya kusisitiza umuhimu wa uaminifu katika ndoa ikifanikishwa (Njogu na Chimerah, 1999). Matukio yanapangwa kwa kuzingatia muundo msago unaofanya dhamira ya hadithi kueleweka kwa wepesi. Muundo msago ni muundo wa moja kwa moja katika mtiririko wa mawazo wa hadithi (Msokile, 1993).

2.2.2 Mtiririko wa Mawazo katika Hadithi, "Kusoma na Kupenda" (Salim, 1970)

Atiyya (1991) anaeleza kuwa hadithi bora ni ile inayojikita katika kujenga dhamira ya hadithi kutokana na mtiririko bora wa mawazo. Mtiririko bora wa mawazo ni wakati ambapo visa vinakuzwa ipasavyo kwa kuipatia hadithi mwanzo, kilele na mwisho ili kueleza dhamira mbalimbali ya hadithi (Msokile, 1993). Katika hadithi hii, mwandishi anatumia wahusika wanafunzi Zubeda na Abdu wanaochumbiana kwa kubusiana ingawa wanagutuka kwa hofu ya kuonekana na Rama ambaye ni mlinzi wa shule. Licha ya Abdu kuwa na woga, anampa matumaini Zubeda asihofu kwa kumbusu tena. Wanatoka kwa pamoja na kwa utaratibu darasani humo wanakokuwa wamejificha. Wanateua maficho haya kwa kuzingatia kigezo cha wanafunzi wengine kutokuwepo shuleni kutokana na mapumziko mafupi. Wakati wanapotoka Zubeda anasikia mwalimu mkuu akimwadhibu mwanafunzi na ukali wa adhabu zake ndio unapelekea wanafunzi kumbandika jina *Hitler*:

> ...jina lake la kawaida halikutosha...walimbandika jina wakamwita *Hitler*... (uk. 40).

Mapenzi ya Zubeda na Abdu yanajengeka katika kipindi cha mwaka mmoja, Abdu akiwa mgeni katika shule hiyo anapojiunga na darasa la saba. Inakuwa rahisi kwa Abdu kufahamu kuwa Zubeda ni kiongozi katika darasa hilo maana anapendwa na walimu wote na wanafunzi isipokuwa wale wanaomuonea wivu. Zubeda anagundua Abdu ni mwerevu jambo linalomtia wasiwasi wa kushindwa katika mtihani ingawaje hatimaye Zubeda anashindwa na Abdu. Mapenzi yao yanazidi kunawiri na uvumi wa mapenzi hayo unashamiri. Wanapofika umri wa miaka kumi na sita wanaingia darasa la nane:

> ...Zubeda na Abdu waliingia darasa la nane...umri wa miaka kumi na sita.. (uk. 42).

Uvumi wa mapenzi yao unamsababisha mwalimu mkuu kumtuma karani wake darasani kwa kina Abdu na Zubeda wakati wa somo la Jiografia. Karani anamkatiza mwalimu wa somo kwa kusema kuwa baada ya somo wawili hao wanahitajika na mwalimu mkuu. Wanapokwenda mwalimu mkuu anawashauri wawache masuala ya mapenzi maana kwake huo ni uchafu. Wanatengana kwa muda lakini penzi lao linarudi kwa kasi kuu. Rama anawagundua Zubeda na Abdu kwa mara ya tatu na wao wanaona hapana shaka lazima atawachongea. Siku ya pili yake, karani wa mwalimu mkuu anabisha tena mlango na wakati huo ujumbe unawekwa wazi kuwa wanahitajika waende nyumbani kisha warudi na wazazi. Inapofika Jumapili, Zubeda anajiandaa kumwambia babake ndiposa mlango unabishwa na anatambua ni Abdu. Abdu anamuaga kwa safari ya kurudi kwao Mombasa pamoja na wazazi wake. Jumatatu yake Zubeda anarudi shuleni na kuendelea na masomo ila chembechembe za hisia kwa Abdu zingali zipo. Mawazo katika hadithi, “Kusoma na Kupenda” ni sahili na

yenye mtiririko wenye dhamira ya kueleza athari za mapenzi ya mapema kabla ya kumaliza masomo. Ubora wa mtiririko wa mawazo unatokana na mwanzo wa hadithi kubainika ambapo Abdu na Zubeda wanapendana, kilele cha hadithi ni wawili hawa kuzidi kupendana hata wanapokatazwa na mwalimu mkuu wanajipata wamerudiana tena katika penzi. Mwisho wa hadithi unatokana na suluhu ambapo inabidi Abdu kurudi kwao Mombasa baada ya kutoka shule anayosomea Zubeda.

2.2.3 Mtiririko wa Mawazo katika Hadithi, "Ajuta Majuto ya Mjukuu" (Somba, 1970)

Mohamed (1995) anaeleza kuwa mtiririko bora wa mawazo hutokana na mawazo kufinywa na kupangwa ipasavyo suala la usahili wa hadithi likizingatiwa. Kufinywa kwa mawazo ni wakati ambapo mwandishi au msimulizi huzingatia matukio muhimu yanayosaidia katika kufanikisha dhamira ya hadithi. Katika hadithi, "Ajuta Majuto ya Mjukuu" Kamene mwenye umri wa miaka tisa anashuhudia Wayua ambaye ni dadake akitekwa nyara. Muda mwingi unapita hajamuona na uvumi wa kujifungua kwa Wayua unamfikia Kamene. Kamene anapofanya uamuzi wa kumtembelea dadake; anagundua kuwa amebadilika sura, umbo na tabia kutokana na kujifungua watoto wengi katika umri mdogo. Wayua anakuwa mwenye kuchakaa na mwili kudhoofika. Hali hii ni zao la ndoa kati ya dadake na jizee Kyalo lenye uchafu pamoja na kitambi:

> ...Kyalo- jitu lililokuwa na tumbo kubwa kama pipa...
> likilala blanketi haiwezi kulifunika tumbo... (uk. 6).

Inatokea siku moja ambapo Wayua anaandamana na dadake hadi mtoni walakini wanapokuwa wakirudi huku wamebeba mitungi kwa kata kichwani wanavamiwa na watu wawili. Kamene anawastaajabu watu hao wanapotokomea na Wayua. Kamene anapokwenda mbio kuripoti nyumbani hakuna anayeshtuka. Aidha, anapofika umri wa miaka kumi na mitano hivi anagundua waliomteka nyara dadake walikuwa wametumwa na Kyalo. Wakati mmoja anapokuwa akiwaza, anakumbuka maneno ya mamake aliyekuwa akimsifia ukwasi wa Kitonga anayeheshimiwa kutokana na mali yake. Wazazi wake wanakusudia kumwoza Kamene kwa Kitonga. Kamene anakuwa amepanga safari ya kwenda Nairobi ili akutane na muhibu wake Kioko. Safari hii inachochewa na mazungumzo anayosikia baina ya babake na wageni wanaokuwa wanamrejelea Kitonga kama vile mamake alivyowahi kumtajia. Kamene anaona angekuwa amekubali angekuwa mke wa Kitonga wa tatu kwa sasa.

Babake anapomtuma Kamene pombe, Kamene anaitia sumu. Wanaburudika wasijue mauti yanawasubiri. Kitonga anapokua akielekea nyumbani anatangulia kuugua na anaaga dunia njiani. Kwa upande mwingine, tumbo linaanza kumsokota babake Kamene huku povu likimtoka mdomoni:

> ...kitambo si kirefu baba yake akaanza kuumwa na tumbo. Mzee akaanza kulalamika na kujibwaga kitandani...povu jingi likaanza kumtoka kinywani...hakuwahi kufika hospitali, alikata roho njiani... (uk. 10).

Wahaka unamjaa Kamene na anaamua kutoroka ingawa hafiki mbali anagongwa na gari. Inasadifu kuwa anayemgonga ni Kioko ambaye ni mpenzi wake. Anampa huduma ya kwanza na Kamene anapoanza kupata fahamu

anamweleza yote yaliyokuwa yametokea. Majuto yanamfanya atetemeke zaidi na katika harakati za kukimbizwa hospitalini pia yeye anaaga dunia. Kioko anahuzunika na kumwona Kamene mpumbavu kwa kumuua babake na Kitonga kwani anaamini angekataa ndoa hiyo hangelazimishwa na mtu. Mawazo katika hadithi yanatiririka ili kujenga maudhui ya majuto.

2.2.4 Mtiririko wa Mawazo katika Hadithi, "Maisha Yalimwendea Kombo" (Isaakwisa, 1970)

Kwa mujibu wa Wanga (2017), mtiririko wa mawazo katika hadithi ni uwezo wa hadithi kuwa na kisa kinachoeleweka kwa usahili kuanzia mwanzo hadi mwisho wa hadithi husika. Katika hadithi hii, mtiririko bora wa mawazo unabainika wazi kutokana na usawiri wa mhusika Ruth ambaye ni mzaliwa wa kijiji cha mashambani cha Kipembawe. Ijapokuwa kijiji ni cha mashambani, kinahusishwa na starehe za kila aina. Ruth anajulikana kwa utiifu wake tangu utotoni. Moyo wake unavutiwa sana na starehe ingawa umri wake mdogo unamponza. Ukoo anaotoka ni wa kifalme na kitajiri:

> Binti huyo alizaliwa katika ukoo wa kifalme na wa kitajiri... (uk. 37).

Aidha, babake ana wanawake kumi na wawili lakini anajibidiisha kumpa Ruth elimu ili aje awafae wadogo wake katika maisha ya baadaye. Anapojiunga na shule ya wasichana ya Tabora anaongoza katika masomo kadhaa. Jambo la kusikitisha ni kwamba anapohitimu, babake anaaga dunia na kuwacha wasia kuwa mwanawe asiolewe haraka kusudi achunge mali. Hekima ya Ruth inamfanya apate cheo cha mwenyekiti katika Chama cha Maendeleo ya

Wanawake. Ingawa anafanya kazi barabara, anaona maisha ya kijijini hayamfai na hivyo anaamua kuhamia mjini anakojihusisha na starehe za densi na ulevi:

> Ruth aliona maisha ya kukaa kijijini hayakumfaa maana alikuwa ni msichana mwenye elimu na madaraka...akaamua kuhamia mjini na akaanza kujiingiza katika starehe kama za densi na kuchapa mtindi... (uk. 38).

Starehe zinamfanya ashindwe kumudu mali kiasi cha kwamba anauza mifugo na kununua gari aina ya *Volkswagen*. Jumamosi moja, Ben aliyeafikiana na babake Ruth kabla hajafa kuwa angemuoa Ruth anamwandikia barua Ruth kuwa atakwenda kumtembelea kwake nyumbani. Ili kumwepuka Ben, Ruth hajisumbui kumpokea. Ben anapowasili anamdanganya hakupokea barua ilhali alipoipata aliichanachana baada ya kuisoma. Mpango wa Ruth wakati huo ni wa kwenda kutembea na rafiki yake John. Punde John anafika na kupiga honi ya gari. Ruth anatoka nje ili kumkaribisha John ndani kusudi ajiandae waende matembezi na John. Ben anasikia wakiitana majina ya kimahaba. Ben anapomhoji John kidogo, anaelewa ipo siri fulani, jambo ambalo linamfedhehesha. Ruth hajali atakachokula mchumba wake Ben. Njiani anamwambia John kuwa hampendi Ben. Aidha, Ruth anamwahidi John kuwa baada ya densi angeenda kwa John. Wakati huo Ben ametulia nyumbani kwa Ruth.

Nyumbani kwa Ruth kunabishwa na msichana mzuri ambaye baada ya kufunguliwa mlango na Ben anafululiza hadi jikoni. Aliyebisha na kufunguliwa anajitambulisha kama Joyce na kumweleza Ben kuwa anafanya

kazi huko. Joyce anaweka wazi kuwa Ruth si kielelezo cha maadili. Hata hivyo, kijakazi anastaajabu zaidi pale Ben anapomwambia kuwa ni mchumba wa Ruth na ameletwa na harakati za kupanga ndoa. Joyce anaamua kumpikia na anapomaliza kula anamwonyesha chumba cha malazi:

> Baada ya chakula, Joyce akamwonyesha Ben mahali pa kulala, wakaagana.. (uk. 40).

Ruth anakawia hadi siku ya pili akiwa katika makazi ya John ndiposa Ben anaamua kurudi kijijini. Hatimaye Ruth anaachwa na John anayemwambia ukweli kuwa ana mke. Starehe hizi zinamfanya Ruth kupoteza mali na mwishowe anaaga dunia kutokana na ajali wakiwa walevi na mwanamume anayempata klabuni. Mawazo katika hadithi ni sahili na yenye mtiririko unaoeleweka wenye dhamira ya kueleza athari ambazo huwakumba vijana wanapojiingiza katika anasa za pombe pamoja na uamuzi usio wa busara.

2.2.5 Mtiririko wa Mawazo katika Hadithi, "Mzee Khamis, Leo Wapi?" (Mohamed, 1971)

Poe (1842;1846) na Forster (1927) wanaeleza kwamba kufaulu kwa mtunzi wa hadithi fupi ni wakati ambapo anapanga mawazo yake kwa kuzingatia usahili wa matukio na matumizi ya muda mfupi kukamilisha lengo analokusudia au kufanikisha dhamira yake katika kikao kimoja. Mtiririko bora wa mawazo unaojenga maudhui ya ulafi unadhihirika katika hadithi hii ambapo Mzee Khamis anasawiriwa na sifa ya kutokosekana katika karamu, maulidi au sherehe za jando. Licha ya hayo, wakati wa siku za mfungo; Mzee Khamis hufurahia zaidi kutokana na mapochopocho yanayoandaliwa wakati huo.

Anapoona dalili za mlo hakosi kutoa kauli; “Leo wapi?”. Yeye hupata habari za hafla kupitia kwa watoto ambao huzunguka kote mjini hata mashambani. Watoto ambao hukiuka sheria ya kutotoa siri ya mahali penye shughuli ya ulaji:

> Siri ya shughuli pahali...ni siri ya kukatwa mkono... mwanachama akiitoa... (uk. 7).

Mzee Khamis anajulikana kama ‘baba habari’ kwa sababu hujua vipembe vyote vyenye shughuli ya ulaji. Maulidi yanapotokea kwa Bin Barak, anastaajabia sufuria saba za pilau zilizopikwa. Anaamini kuwa yeye si mroho kwani kula ni wajibu ndiposa hasubiri mwaliko. Kabla ya siku ya maulidi, anakunywa dawa ya kusafisha tumbo na kutanua mbavu ili aweze kula ipasavyo. Siku inapofika anachukua kapu na kuchomeka kisu chake nyongani tayari kuelekea maulidini. Njiani anawapuuza watoto wanaomfanyia dhihaka kwa kumuuliza siku hiyo hafla ilikuwa wapi? Anafika mapema kwa Bin Barak ili atumike na anakataa kukaa ukumbini maana anajua jikoni ndiko kwenye fursa ya kujaza kapu lake. Kicheko cha watu hakimtamaushi. Wanamchunga asiibe lakini anafanikiwa kuiba ratili mbili za nyama mbichi na anazitia kapuni:

> ...walikuwa waangalifu asije akaiba...Hawakufuzu, alizinyakua ratili mbili za nyama mbichi... (uk. 8).

Anaposikia dua ya mwisho, anaanza kujisongeza ili awahi chakula. Mpishi anapomuona anamtishia kumpiga kwa mwiko jambo linalomsababisha machozi kumlengalenga kwa kuona ni maonevu. Anamlalamikia mpishi kwa kumwambia shughuli si yake ilhali anagombana. Hatimaye, mpishi anacheka pamoja na kushangaa anapomuona akijaza makoko kapuni. Wakati wa

kuandika chakula, Mzee Khamis anajishughulisha na kutia sinia mbili kapuni. Mzee Khamis hatosheki, anajumuika na watu ili apate kula watakapoandaliwa chakula. Bismillahi! inapopigwa baada ya usomaji wa maulidi anafanikiwa kula robo sinia wakati hata wengine hawajaanza kula. Anaamini mtu hushindwa na binadamu mwenziwe ila si vyakula. Ananyongwa mara mbili na kukwaruza koo jambo linalowaudhi wanaokula karibu na yeye lakini hajali. Mzengo aliyezoea kumtania Mzee Khamis anamtishia Mzee Khamis kuwa ataondoa sinia. Mzee Khamis anamshtua kuwa atamchoma kwa kisu. Watu wanakula na kubaki kumwangalia yeye huku wakimshangaa. Anapomaliza anaelekea kwake taratibu akiwa na maumivu ya shibe:

> Alipomaliza...tumbo lilimfura...aliona taabu, kwenda kulikuwa mashaka. (uk. 9).

Anapofika kwake anaweka nyama mbichi juu ya kishubaka na kapu la wali mvunguni. Usingizi wa shibe unambeba asijijue. Paka wa Mzee Khamis kwa jina Pusi anavutiwa na harufu ya nyama na kupenya dirishani. Mzee Khamis anaota nyama yake inaliwa na paka na anapogutuka anapata uhalisia wa ndoto yake. Anafunga dirisha na kuanza kumpiga paka kwa bakora. Hasira zinamjaa paka ambaye anamrukia uso na kumrarua ndiposa anafungua mlango mbio na kutoka huku akipiga kite. Damu inamtoka na majeraha anayopata yanamlaza kwa homa ingawa kwa Mzee Khamis dawa ni akiba ya wali kapuni. Usiku huo paka anapigana na nyoka na kumwangusha kitandani mwa Mzee Khamis ambaye ananusurika kuumwa na nyoka anayeuliwa na paka wake. Tukio hilo linamtia woga Mzee Khamis ndiposa analala nje kibarazani:

> Pusi alikamata pandikizi la joka akalibingirisha kwenye kitanda cha bwana wake alipolala...alipoangaza hakusema...alitoka nje mbio roho ikimdunda... (uk. 10).

Maulidi mengine yanatokea kisiwani Tumbatu na ingawa anakosa nauli anaamua kutembea hadi huko. Njiani anaomba usaidizi kutoka kwa wanaompita kwa magari lakini wanamfanyia dhihaka. Anafika Mkokotoni na kwa bahati mbaya anakosa mtumbwi wa kumvusha Tumbatu ndiposa anaona aogelee kusudi asikose wali. Mkondo wa bahari unamvuta ila anang'ang'ana asizame baharini. Mzee Khamis anazidiwa na maji ya bahari kwa kuishiwa na pumzi lakini jabali linamsaidia kwa kumpa uwezo wa kujizuia asizame zaidi baharini. Anajipata kwenye gari la hospitali linalokuwa kwenye mwendo wa kasi na upande wa kulia anamuona mzee mmoja mkongwe. Anapouliza alipo, mzee huyu anamweleza ndiye aliyemwokoa kwa ngarawa yake. Mzee Khamis anajuta kukosa wali wa Tumbatu. Aidha, anauliza kama atalazwa kwani anakumbuka siku inayofuata kutakuwa na maulidi ya Mpapa. Nia yake ni asikose maulidi hayo maana wali upo na ni wajibu wake kula:

> ...alifikiria moyoni, nitakimbia...Mpapa siwezi kuikosa. (uk. 11).

Mawazo katika hadithi yanawasilishwa kwa usahili huku dhamira ya hadithi ambayo ni kuonyesha athari za ulafi ikiwekwa wazi kupitia kwa Mzee Khamis anayepata madhara yanayoweza kumuua kama vile kuzama baharini. Mzee Khamis ananusurika kuzama baharini zaidi anapoamua kuogelea hadi kisiwani Tumbatu kusudi akapate kula wali. Aidha, mawazo ya hadithi yamejengwa katika kurasa tano (uk. 7-11) na hivyo ni wazi kwamba mwandishi amefanikiwa kutumia muda mfupi kufanikisha dhamira ya hadithi na kuifanya iweze kusomeka katika kikao kimoja.

2.2.6 Mtiririko wa Mawazo katika Hadithi, “Malipo Duniani, Hesabu Ahera” (Said, 1971)

Kwa mujibu wa Mbatiah (2000), uzuri wa hadithi fupi hutokana na mawazo yaliyopangwa vyema ambayo yanarejelea kuhusu maisha yetu au jamii zetu na mawazo hayo yapangwe kisanaa ili kugusa hisia za msomaji. Kigezo hiki cha utathmini wa ubora wa mtiririko wa mawazo kinabainika katika kila hadithi fupi teule kwa sababu mawazo yamepangwa katika matukio yanayoonyesha hali halisi ya maisha ya utamaduni wa Mwafrika. Katika hadithi hii, mtaa wa Fuga ndiko anakoishi mzee Miraji. Anaishi hapo na mkewe Bi.Asha pamoja na watoto wake wawili Fatuma na Kombo. Wanaishi katika nyumba ya madebe iliyopakwa rangi ya manjano. Kila mwaka Mzee Miraji huipaka rangi lakini watoto wa mtaani hawakomi kuichora ukutani. Ingawa nyumba yake ina madirisha mapana manane, haimletei mwangaza wa kutosha. Isitoshe, nyumba yake inasifika mtaani kote kwa usafi. Mtoto wake wa kike Fatuma, ana umri wa miaka kama kumi na mitano ilhali Kombo ana miaka kumi na miwili. Kipenzi cha wazazi ni Fatuma kutokana na upole wake, huruma na tabia nzuri. Anapendwa hata na rafiki zake wa darasa la nane. Vilevile, urembo wake ni wa kupigiwa mfano:

> ...Alikuwa na umbo la wastani, si mnene si mwembamba...
> nywele ndefu laini na uso wa duara mzuri wenye tabasamu...
> (uk. 12).

Kombo yupo katika darasa la sita ingawa ni mtundu sana tofauti na Fatuma ambaye ni mpole. Hakuna asiyemjua Kombo shule nzima kwa tabia zake mbaya. Anajulikana pia kama fundi wa kalamu na shujaa ndiposa wenzake wakampa jina ‘*Simba’*. Mtu anapokosewa na mwanafunzi mwengine humletea

yeye mashtaka na aliyekosea mwenzake hupata adhabu barabara. Kando na hayo, yeye ni mwanariadha hodari ambaye huletea shule tuzo za kombe la ushindi. Mzee miraji huishi kwa majonzi kutokana na kubishiwa mlango wake na jirani zake kwa mashtaka ya mwanawe Kombo. Siku moja babake Kombe anaugua na anapoona hali yake inazidi kuwa mbaya anawaita wanawe kuwapa wasia. Anamwambia Fatuma iwapo anataka radhi zake sharti amwangalie Kombo na mamake. Kombo naye anaambiwa iwapo anataka radhi sharti awache mchezo na utundu. Siku inayofuata mwendo wa saa mbili mzee anaaga dunia na kilio cha familia kinasikika kote. Anayehusika na shughuli ya kuzika kwa misingi ya mila na desturi inakuwa ni Kombo. Baada ya shughuli za kuzika, asubuhi ya siku inayofuata rafiki zake wanambishia Kombo mlango ili waende kupiga njiwa kwa panda lakini anatoka na kuwafokea waondoke:

> ...akatoka nje...akawashambulia...msiisogee nyumba hii tena! (uk. 13).

Hata hivyo, Kombo baada ya mwaka anahitimu vizuri katika darasa la nane kutokana na uamuzi wake wa kubadili tabia. Anapojiunga na shule ya upili anajituma kimasomo na maadili kiasi cha kupigiwa mfano kwa kuwa kielelezo bora kwa wengine. Kombo anafanikiwa kufanya vyema na anapata ufadhili wa kwenda Uingereza kusomea udaktari. Wakati huu Fatuma anakuwa tayari ameolewa. Kombo anapokuwa Uingereza anapatana na binti wa kwao ambaye wanapendana na anaporudi nyumbani anasafiri naye ambapo wanafanya uamuzi wa kufunga pingu za maisha. Wanabarikiwa na mtoto wa kiume ambaye anampa jina Miraji, jina la marehemu babake. Pindi anapokua, wengi wanamsema Miraji kutokana na utundu wake wa ajabu. Hakuna anayekosa

kumtaja kutokana na utukutu wake. Wengi wanachukulia kuwa Miraji ni malaika anayetumwa na Mungu kumlipa Kombo kwa uchungu ambao alimtaabisha babake alipokuwa hai. Aidha, wengine wanakisia kuwa Kombo ni mkosa radhi za babake:

> ...wengine wanasema huyu si mtoto ni malaika aliyeshushwa kuja kumwonyesha Kombo uchungu wa kumtaabisha mzee wake, wengine wanasema ...amekosa radhi za mzee wake...wewe unafikiri vipi? (uk. 14).

Mawazo katika hadithi yanapangwa ipasavyo na hivyo kufanikisha dhamira ya hadithi ya kukashifu utukutu miongoni mwa vijana wakati wa malezi kutoka kwa wazazi au wakuu wao. Hadithi inahamasisha vijana kuwa wenye kutii kwa sababu mtu anapowasumbua wazazi wake huenda maishani akalipwa kwa kupata mtoto mtukutu kama inavyodhihirika kutoka kwa Kombo ambaye anasumbuliwa na mwanawe Miraji kama alivyokuwa anamsumbua babake, Mzee Miraji.

2.2.7 Mtiririko wa Mawazo katika Hadithi, “Sina Rafiki” (Wahab, 1977)

Iribemwangi (2007) anaeleza kuwa hadithi fupi ya kifasihi inastahili kuwasilisha mawazo vyema kwa kuyajenga kupitia taswira ndiposa ifaulu kusemwa kuwa ina mtiririko bora wa mawazo. Taswira husaidia katika kujenga mawazo, mianzo na miishio ya hadithi yenye ubunifu wa kuvuta makini ya msomaji au msikilizaji (Poe, 1842). Hadithi hii imesukwa kwa mawazo yanayothibitisha ujenzi wa taswira ya tamaa kwa kumsawiri mhusika Hasan ambaye amekaa akivuta sigara huku akitazama watu waliojaa dukani kwa rafiki yake Karama. Hasan anasubiri wateja waondoke dukani kwa

Karama ili amweleze Karama anachohitaji na anaingia bandani mwake anamotengeneza magari. Usiku huo wanakutana mahali pao pa mazoea ambapo ni mbele ya mkahawa na kuzungumza.

Hasan anaonekana kutokuwa na utulivu kwani baada ya mazungumzo mafupi anadai hali yake kifedha si nzuri na anaomba kukopeshwa pesa na Karama. Hasan anadai kazi haimwendei vizuri kama awali. Karama anamwambia ni yeye amekosa uaminifu wa kuthamini kazi yake pamoja na uraibu wa ulevi na kamari. Hasan anamuuliza tena Karama iwapo atamkopesha fedha, Hasan anapewa shilingi mia mbili. Anapoona wingi wa noti katika pochi la Karama anatamani kumpokonya ila hawezi. Hasan anatumia pesa alizokopeshwa na Karama vibaya kwa sababu zinaishia kwenye kamari. Hasan anazidi kudaiwa na watu aliowakopa awali. Mara nyingi Karama ndiye anatatua ugomvi baina ya Hasan na wanaomdai. Hasan anawaza namna ya kulipa madeni maana wapo wanaoahidi kumuua wakimpata:

> ...Wako watu waliomuahidi kumuua wakimkuta njiani kwa jinsi walivyomdai, Kwa hiyo alikuwa mwoga kuranda ovyo ovyo tu... (uk. 1).

Hasan anabaki kuwaza namna atapata hela kwa sababu Karama humsaidia sana na hata anapomwibia humsamehe. Asubuhi moja, Karama anamwambia Hasan amtengenezee pikipiki kwa kuwa anataka kwenda kuzuru shamba lake. Hasan anawaza atakavyopuuza kuweka breki kusudi Karama apate ajali. Hata hivyo, anajishauri apuuze mawazo yake hadi atakapojua mahali Karama anakoweka pesa kwa sababu Karama anapokwenda shambani, humwacha Hasan dukani. Mwezi unapopita ndipo Karama anapata safari ya kutoka mjini

anakoishi hadi shambani. Hasan anajua mke wa Karama kwa jina Bi. Asha ni mpenzi wa sinema na anamshawishi kuwa atampeleka katikati mwa mji kutazama sinema:

> ...Hasan baada ya kuzungumza na Bi. Asha...alimwambia, ningependa kukualika Sinema... (uk. 2).

Bi. Asha anapoonekana kukataa, Hasan anamshawishi asiogope maana atakuwa ameenda naye hivyo mumewe Karama hawezi kulalamika. Hasan anafanikiwa kwenda kutazama sinema na Bi. Asha usiku huo. Uraibu wa Bi. Asha katika sinema unamfanya kuandamana na Hasan kutazama sinema kila wakati Karama anapotoka kwenda shambani. Shambani mwa Karama ni mbali na mjini wanapoishi na mkewe Bi. Asha. Hasan anaanza hata kumwambia Bi. Asha amwache Karama atamwoa lakini Bi.Asha anakataa kauli ya Hasan. Hatimaye, Bi. Asha anamwambia Hasan kuwa anavyojua mumewe huweka pesa za noti katika mojawapo ya madebe yaliyoko dukani.

Alhamisi moja Karama anamwambia Hasan kuwa ana nia ya kwenda shambani na angerudi Ijumaa. Karama anamweleza Hasan ambaye ni fundi wa magari amuundie pikipiki yake kwa kuhakikisha kuwa ina uthabiti wa kwenda masafa marefu bila shida yoyote. Hasan anaunda pikipiki kisha anampelekea Karama nyumbani. Kama ilivyo desturi, Hasan anaachiwa duka na Karama. Usiku uo huo anafanikiwa kwenda na Bi. Asha kwenye sinema. Ijumaa inapofika anafunga duka saa tano na nusu. Kabla ya kutoka, Hasan anaamua kukagua ni debe lipi lililotiwa noti:

> ...Nitalijuaje lile lenye pesa kati ya haya yote?...Aliona lazima ipo alama maalumu ambayo Karama amelitia debe hilo... (uk. 3).

Anaposhindwa kutambua debe lenye pesa za noti anaamua kwenda kumimina pesa za asubuhi kikapuni. Hasan anaelekea hadi jikoni na kumuuliza Bi. Asha mahali Karama huweka pesa. Bi. Asha anamshangaa Karama mbona anatafuta pesa zao ndipo Hasan anajifanya mjanja na kumwambia anamjali yeye maana itokee Karama afe pesa hizo haziwezi kumfaidi Bi.Asha. Inapofika saa tisa, Hasan anaamua kurudi ili afungue duka ndipo anaposikia honi ya gari la hospitali huku gari la polisi linafuata kwa nyuma. Hasan anauliza mahali kwenye mkusanyiko wa watu tukio ni lipi lakini kila mmoja anasema hajui. Dukani na mkahawani kunajaa watu wakizungumza na kuulizana lililotokea. Aidha, kijana mmoja katika kibanda kilichoko karibu na duka la Karama anapokea simu. Anatoka kama amefadhaika. Bwana Musa, mmoja wa wazee pale mjini anapomuuliza hali ni ipi anaanza kulia. Watu wanajaribu kumtuliza na baada ya dakika anafuta machozi na kusema Karama ameaga dunia:

> ...kijana yule...aliweza kusema huku akifuta machozi, Karama amekufa... (uk. 4).

Bwana Musa anadai kuwa watajua chanzo cha mauti na kushauri mipango ianze ya kumteua mtu wa kumpa Bi. Asha habari na kuwateua watakaoenda kuchukua maiti. Baada ya siku tisa, Bi. Asha anampa Hasan funguo auze vitu vilivyobaki dukani. Hasan anafurahia na anapouza anatia nusu ya pesa anazopata mfukoni mwake. Jumamosi moja, polisi anafika na kumwarifu Hasan kuwa anahitajika kufika stesheni mchana. Habari hii inampa wasiwasi kiasi kwamba anauliza wateja maswali mara mbili mbili kuhusu huduma wanayotaka. Anapokwenda kuhojiwa anakiri kutohusika ila anaonekana mwingi wa wasiwasi:

> ...Jasho lilimtoka Hasan alipokutana na macho yale makali... (uk. 5).

Baada ya siku arobaini, Bi. Asha anaona apange vitu vya marehemu mumewe. Anapatana na debe lililofungwa kwa kufuli na juu limewekewa magunia. Anatafuta funguo na anapolifungua anapata noti ambazo haoni haja ya kuhesabu maana mumewe alikuwa amemwambia ana akiba ya elfu sitini. Analia kwa uchungu wa mumewe kutofaidi pesa hizo maana ashaaga dunia. Asubuhi ya siku inayofuata, anamuita bwana Musa na kumwambia amtafutie nyumba au shamba ili iwe rasilimali yake:

> ...alimwita bwana Musa...alimwomba amtafutie nyumba au shamba ili iwe ndio rasilimali yake... (uk. 7).

Baada ya miezi miwili na nusu, bwana Musa anampa Bi. Asha mashamba mawili na nyumba kwa shilingi elfu hamsini na tatu. Muda wote huu, Hasan anapouza anacheza kamari na kukopa sana kwa sababu anajipa matumaini atapata akiba ya peza za Karama. Bi. Asha anaamua kumwambia bwana Musa amwekee stakabadhi za nyumba na shamba. Hasan anazidi kupata wasiwasi wa kupata pesa na mwisho anafanya uamuzi wa kumuoa Bi. Asha. Usiku mmoja, anaamua kumwambia kuwa vitu dukani vinaisha na Bi. Asha anapomjibu kuwa mambo ya duka amemwachia anaamua kumwambia hajaona debe la pesa za Karama mle dukani. Bi. Asha anamwambia labda watafute kwenye sanduku kubwa chumbani. Asubuhi yake wanaamua kutafuta na hatimaye wanapata debe lenye funguo. Hasan anapotambua ndilo lenye pesa anamuamuru Bi. Asha atafute ufunguo:

> ...alijua tu kuwa hilo...alimwamrisha Bi. Asha amtafutie ufunguo... (uk. 8).

Bi. Asha anajihangaisha kutafuta ufunguo hadi mwisho Hasan anaona si tabu atatafuta fundi ili avunje kufuli atoe pesa. Mawazo yanamjia namna atakavyomwangamiza Bi. Asha ili arithi pesa zote. Aidha, anakumbuka maradhi ya Bi. Asha ya tumbo ambayo siku za joto humzidi hadi anahangaika hospitalini ndiposa anaamua atasubiri wakati huo. Joto linapoanza kumsumbua Bi. Asha, Hasan anamletea Bi. Asha dawa mara moja pekee. Bi. Asha anamkumbusha Hasan amletee dawa kwa mara nyingine ili amalizie dozi lakini Hasan anampuuza na kukataa kumletea dawa:

> ...Unaniona ninavyotaabika kwa maradhi na dawa unaweza kuipata!...hushughuliki, ah, vibaya hivyo! (uk. 9).

Inatokea siku ambapo Hasan anaandaa dawa yenye ukali zaidi na kuwaaga wenzake mapema kibarazani. Bi. Asha anapoinywa anazidiwa na badala ya Hasan kumsaidia anampuuza. Bi. Asha anaanza kufoka kwa nguvu kuwa Hasana anataka kumuua lakini anampuuza na kwenda kuvunja lile debe la pesa kwa furaha. Anastaajabu baada ya kupata elfu saba kwa sababu alitarajia pesa nyingi zaidi. Hamaki inampanda na anaanza kumuita Bi. Asha mwizi. Wakati huo, Bi. Asha yuko hoi chini amezidiwa na dawa:

> ...Mwizi, haini, amenidanganya...Alimkuta Bi. Asha amejitupa chini... (uk. 10).

Anampiga mateke naye Bi. Asha anafungua jicho moja na kumwambia Hasan alimuua rafiki yake Karama kwa ajili ya pesa ndipo Hasan anamfokea kwa hamaki na kumwambia kuwa hana rafiki. Inapofika asubuhi, Hasan akiwa msikitini macho yanakolea wekundu. Anajifanya kulia huku akisema bibi yake ameaga dunia. Baada ya sala, watu wanaenda nyumbani kwake. Bwana Musa anakuwa wa kwanza kufika na baada ya kuona maiti anaamua kwenda kwa

idara ya afya kupata msaada. Inafika magharibi ambapo polisi wanakuja kuchukuwa ithibati. Hata hivyo, baada ya mwezi redioni kunatangazwa kuwa Hasan Ali anahukumiwa kunyongwa baada ya kupatwa na hatia ya mauaji ya Karama Said na mkewe Bi. Asha binti Sudi:

> ...watu walisikia katika redio kuwa, mahakama kuu ya nchi imemhukumu... (uk. 11).

Mawazo katika hadithi yanapangwa kwa njia sahili ambapo mhusika Hasan anatekeleza ukatili kutokana na tamaa ya mali ya Karama ambaye ni rafiki yake. Hivyo basi, mtiririko bora wa mawazo unasaidia katika kueleza dhamira ya hadithi ambayo ni athari ya tamaa. Tamaa inayochangia ukatili unaosababisha mauti katika jamii.

2.2.8 Mtiririko wa Mawazo katika Hadithi, "Mke Wangu" (Muhammed, 1977)

Omar (2010) anaeleza kuwa mawazo yanapopangwa kwa kuzingatia utaratibu hitajika, hadithi huwa na mvuto wa juu kwa hadhira lengwa. Mawazo katika hadithi hii yamepangwa vyema ndiposa baada ya miaka thelathini ikachapishwa tena katika mkusanyiko *Damu Nyeusi* (2007). Msimulizi katika hadithi hii anaeleza kuwa anapomaliza masomo ya juu, wazazi wake wanampendekezea wanawake kadhaa wa kuoa kama vile; Fedhele Salim na Salma Fahil lakini mwisho anamteua Aziza miongoni mwa wanawake wengine anaopendekezewa. Hataki anaopendekezewa awali maana hawana sifa azitakazo. Anataka mke ambaye hajui mengi ili amfunze yeye. Anamwambia Aziza kuwa atamlea mwenyewe maana anajua hata shule

hakusoma. Vilevile, anajua kuwa hajakulia mjini akabatilishwa na utamaduni wa mjini. Msimulizi anatoa tawasifu yake ya kuzaliwa katika familia ya kitajiri walakini anaeleza kuwa wao bado hawajawacha utamaduni wao. Sababu ya kumkataa Fedhele Salim ni kuwa, anakumbuka alivyompata wakati mmoja usiku akiwa amevaa vazi fupi pamoja na rafiki yake huku wamemzingira mwanaume katikati. Vilevile, anamkataa Salma Fadhil maana ana utamaduni wa kuficha sura kwa kujiremba marangi ya mashavu na midomo:

> ...Salma...sura yake daima anaificha haionekani kwa kujiremba... (uk. 48).

Aziza ni chaguo lake kwa wanawake anaopendekezewa na mamake maana anamuona hajui mengi ya mjini na hivyo basi itakuwa nadra ndoa yao kusambaratika. Msimulizi anaamua kumuoa Aziza. Baada ya harusi wanatengewa vyumba vitatu ghorofa ya juu. Chakula kinapoiva, mfanyakazi Mapanya huwaletea wale. Vilevile, Mapanya hufanya kazi ya kuwafulia nguo. Msimulizi anapodhania kuwa ni fursa yake kumsoma mkewe na kumfunza, anapata hali ni tofauti maana mkewe ana hekima yake. Mkewe anakuwa hana mazungumzo mengi naye na msimulizi anadhani ni kutokana na ugeni wa ndoa. Ajabu ni kwamba mara kwa mara mkewe humtazama kwa kumchuja jambo linalomtia msimulizi dhiki:

> ...Aziza alikuwa daima akinitazama...tena si mara moja... (uk. 49).

Alasiri moja msimulizi anapokuwa katika harakati za kuchana nywele anagundua mkewe anamchuja sana. Anapomuuliza sababu, anashangaa na jawabu la mkewe anayemwambia hadharani kuwa hamchuji ila anamsikitikia.

Mkewe anaendelea kumwambia kuwa hujisikitikia kwa sababu Mungu alimpa gumegume na hana budi ila kuvumilia. Uchungu wa mkewe unatokana na hali ya msimulizi kutofanya kazi na kutegemea wazazi wake ambao bado ndio wanamlisha pamoja na mkewe. Aziza anaendelea kumwambia anamshangaa kuwa hata pesa anapewa. Kauli hii inamtia msimulizi kustaajabu kutokana na kisio lake la kudhani angemfunza mkewe ustaarabu na inatokea yeye ndiye anafunzwa. Anajitetea kwa kusema bahati ya kazi ndiyo haijasimama maana amejaribu kutafuta lakini hajapata:

> ...Aziza...ulililoliona wewe ni jambo la kazi, basi kazi haijawa riziki... (uk. 50).

Msimulizi anaposema ametia nia, mkewe anamwambia bado kwa sababu imani ya vijana wa mjini ni kuajiriwa tofauti na wa vijijini ambao hujiajiri. Anamwambia hata kuchoma mihogo ni kazi na inafaa msimulizi asichague kazi. Aziza anakiri hana budi kupokea chakula kibivu kwa sababu mumewe haleti kibichi. Aziza anakataa kuletewa mtu wa kumfulia nguo na kumwoshea vyombo. Msimulizi anapomuuliza kama ataweza hiyo kazi anaonyeshwa na mkewe viganja na kuambiwa vyake si dhaifu kama vya msimulizi ambaye hata akimshika mwanamke hawezi kuhisi kitu:

> ...hiyo ndiyo mikono ya mwanamume, hiyo?...unadhani mwanamke anahisi kitu kama ataguswa na mikono kama hiyo? (uk. 51).

Msimulizi hahisi uzito wa maneno ya mkewe kwani anaona ni sawa maana inamsaidia mkewe kutoa kinyongo cha moyoni. Anapoamua ni zamu yake kumwelekeza kuhusu umuhimu wa kuvaa viatu anaambiwa viatu havina faida. Anapojaribu kumweleza mkewe viatu vitamsidia asichomwe na mwiba,

mkewe anamwambia hata akichukua mwiba amshindilie utavunjika maana yeye hana miguu dhaifu:

> ...chukua mwiba uushindilie nyayoni...utazame kama haukuvunjika... (uk. 52).

Kinachomuudhi msimulizi zaidi ni kuwa wapo watu ambao huja kwao kuwapeleleza. Msimulizi anaona fedheha kutembea na mkewe mbele za watu maana anaona hajastaarabika. Aziza pia anaona taabu maana anaona ameolewa na mume asiyetaka watu wamjue. Msimulizi anazidi kushangaa maana tangu amnunulie mkewe mswaki hajautumia. Anapomuuliza sababu ya kutopiga mswaki, analetewa mswaki wa mnazi na unga anaoutumia kama dawa ya meno kupigia mswaki:

> ...aliondoka...akarudi na mswaki wa mnazi na...unga uliokaa baina ya jivu... (uk. 53).

Msimulizi anamwambia Aziza kuwa anamuuliza iwapo hupiga mswaki maana anagundua mswaki alionunua hujatumika, anajibiwa na mkewe kuwa hawezi kutumia manyoya ya nguruwe. Anamwambia kwa kuita jina la msimulizi ambalo ni Yasini kuwa yeye ndiye ameng'olewa meno kwani yake bado mazima. Msimulizi anaona kila anapojaribu kumstarabisha anastarabishwa yeye. Fedheha hii inamfanya kujisemea kuwa kweli mkewe si wa kiwango chake:

> ...Nimtokee kwa wapi mimi Aziza...kweli mimi kwake si mume kifu yake... (uk. 54).

Alasiri moja, Seluwa ambaye ni mtoto wa shangazi ya msimulizi anafika na wanaanza kutaniana na msimulizi maana ilikuwa hata waoane. Yeye si chaguo la msimulizi kutokana na tabia yake ya kuwa mneni sana. Seluwa anataniana

na msimulizi pamoja na Aziza kwa zamu. Punde, Aziza anawaambia Yasini na Seluwa kuwa anashangaa kwa nini aliingia katikati yao maana wanaendana. Seluwa anapotaka kusema, Aziza anamkatiza na kumuuliza iwapo anataka madafu maana amemsikia muuza madafu. Seluwa anapokubali msimulizi anatoa pesa naye Aziza anakimbia dirishani na kumwambia muuza madafu apande na manne. Msimulizi anapomuuliza Aziza sababu ya kumwambia apande anatolewa jicho la ukali na kuulizwa iwapo ni kosa muuza madafu akiingia kwao. Wakati muuza madafu anatayarisha madafu, Aziza anatoa wasifu wa muuza madafu kwa kusema yeye ndiye mwanamume kwa sababu hafikirii kuchana nywele bali anajituma kuvumbua riziki. Anasema mume kama muuza madafu ndiye anatamani na atashukuru iwapo msimulizi atampatia talaka:

> ...huyu ndiye mume wangu kifu yangu...nitashukuru kama utanipa talaka... (uk. 57).

Mawazo katika hadithi yanatiririka vyema na kufanikisha dhamira ya hadithi ambayo ni changamoto zinazotokana na ndoa za utamaduni uliopitwa na wakati kama vile mume kuchaguliwa mke. Mgogoro katika ndoa ya msimulizi na Aziza unatokana na tofauti zao za kimazingira pamoja na malezi maana msimulizi ameathirika na utamaduni wa kisasa tofauti na Aziza anayethamini utamaduni wa kale.

Ubora wa mtiririko wa mawazo umetathminiwa kwa vigezo mbalimbali kama vile: mawazo kuwasilishwa kwa lugha sahili, mawazo kudhihirisha mwanzo, kilele na mwisho wa hadithi, mawazo kuzingatia matukio muhimu tu

yanayofanikisha dhamira ya hadithi, mawazo kupangwa na kuwasilishwa kikamilifu kwa muda mfupi, mawazo kurejelea maisha ya jamii lengwa ili kisa kugusa hisia za msomaji au msikilizaji na mawazo kujengwa kwa kutumia taswira. Kinyume na Poe (1842; 1846), hadithi fupi inazidi kubadilika na kukua kadiri muda unavyosonga kwa sababu baadhi ya hadithi fupi za kisasa zinatumia muundo wa kioo na bado zinaibuka kuwa na ubora. Muundo wa kioo ni matumizi ya mbinu rejeshi katika kukuza mawazo ya hadithi (Msokile, 1993; Chokocho na Kayanda, 2016). Vilevile, suala la mwingiliano wa tanzu ni ubunifu na halikwepeki katika kazi za fasihi maana ushairi unaweza kuwa katika hadithi fupi na bado hadithi fupi ikabakia na sifa zake (Msokile, 1992; Henry, 2018). Mtiririko bora wa mawazo ni msingi wa ujenzi wa tukio moja katika hadithi fupi.

2.3 Ujenzi wa Tukio Moja katika Hadithi Fupi Teule

Poe (1842; 1846) anaeleza ubora wa hadithi fupi ni uwezo wa hadithi husika kujenga tukio moja. Tukio ni jambo au ujumbe ambao mwandishi wa kazi ya fasihi anakusudia kuwasilisha kwa msomaji wa kazi husika ili kubainisha maudhui kwa njia ya kisanii na sahili. Ujenzi wa tukio moja hutokana na uwezo wa hadithi husika kuwasilisha mgogoro mmoja tu unaodhihirika kuanzia mwanzo hadi mwisho (Esenwein, 1909; Mbatiah, 2000; Iribemwangi, 2007). Vilevile, Naude na wenzake (2009) wanaeleza kwamba ili hadithi fupi isemekane kuwa na ubora, inafaa tukio moja likuzwe na kukosekane ukuzaji wa vitukio vinginevyo visivyochangia ukuaji wa tukio kuu. Mbatiah (2000) anaeleza kuwa tukio kuu ndilo hubeba vitukio vingine na vitukio hivyo havifai

kupambanuliwa sana. Tukio kuu limejengwa kwa namna mbalimbali kama inavyobainika katika hadithi fupi teule kama ifuatavyo:

2.3.1 Ujenzi wa Tukio Moja katika Hadithi, "Siku ya Arobaini" (Mohamed, 1970)

Katika hadithi hii mhusika Sadiki anafuatilia ujumbe wa barua anayoipokea kutoka kwa mpenzi asiyemjua. Ujumbe katika barua unakusudia waonane. Tamaa ya Sadiki kwa wanawake inamfanya atimize matakwa ya barua ile na kufululiza hadi ufuo wa bahari wa *People's Beach*. Hatimaye arobaini yake inafika kwa sababu mipango yote imetoka kwa mkewe Bahati ambaye anamdadisi kuhakikisha kuwa anayoyasikia kuhusu usherati wa mumewe ni ya kweli. Mwandishi wa hadithi hii amejikita na tukio moja la athari ya usherati katika maisha ya ndoa na hivyo basi kujenga dhamira ya kusisitiza umuhimu wa uaminifu katika ndoa. Ujenzi bora wa tukio kuu la Sadiki kukosa uaminifu katika ndoa na hatimaye kujulikana na Bahati ufanikisha hadithi kuwa bora:

> ...kwa ghafla anga la taa za gari iliyopita njiani lilimeta juu ya uso wa yule bibi, aliduwaa kuona uso wa mkewe, Bahati. (uk. 27).

2.3.2 Ujenzi wa Tukio Moja katika Hadithi, "Kusoma na Kupenda" (Salim, 1970)

Tukio la athari ya mapenzi ya mapema kabla ya kumaliza masomo hasa kwa vijana wa shule ya msingi limedhihirishwa katika hadithi hii. Mara nyingi vijana wa shule ya msingi huwa katika umri wa chini ya miaka kumi na nane,

wanapojihusisha na mapenzi ya mapema elimu yao huathirika. Mapenzi yao huwa ni ya kitoto tu kama vile Abdu na Zubeda ambao wanajificha darasani ili wabusiane. Uvumi wa mapenzi yao ndio unamfanya mwalimu mkuu kusimama kidete na kuwakashifu ili kukuza maadili. Hatimaye, Abdu anaamua kutoka shule hiyo na kurudi kwao Mombasa. Tukio hili linalandana na mada ya hadithi kwa sababu safari ya mapenzi baina ya wanafunzi imeelezwa na hatimaye athari ya mapenzi hayo kubainika ambapo wanafunzi hao wanatumwa nyumbani kuita wazazi. Abdu anaamua kutorudi kabisa shuleni humo:

> ...Abdu alimwomba Zubeda amfikishie barua yake ya kuacha shule pamoja na vitabu kwa mwalimu mkuu...alikuwa anarejea kwao Mombasa... (uk. 44).

2.3.3 Ujenzi wa Tukio Moja katika Hadithi, "Ajuta Majuto ya Mjukuu" (Somba, 1970)

Kama mada ya hadithi ilivyo, madhara ya ndoa za lazima yanajitokeza kama tukio kuu linalojengwa. Wayua anaishia kuhangaika katika ndoa ambayo hajairidhia baina yake na jizee Kyalo. Kuongezea, Kamene ambaye ni dadake Wayua anapolazimishwa kuingia katika ndoa baina yake na Kitonga kama mke wa tatu anaamua kuwatilia sumu wageni wanaokuja kutoa posa pamoja na babake. Hatimaye, Kitonga na babake Kamene wanaaga dunia suala ambalo linamtia majuto na anapotoroka anagongwa na gari. Vilevile, mauti yanamfika Kamene wakati anapelekwa hospitalini. Mchakato mzima wa matukio haya ni kujenga tukio moja la madhara ya ndoa za lazima. Kuzingatia

ujenzi wa tukio moja, hadithi inapata mvuto na kumfanya msomaji au msikilizaji kuelewa dhamira ya athari ya ndoa za lazima:

> ...Ya nini Kamene kwenda kumuua baba yake na yule mchumba wake. Laiti angalikataa katu katu, asingalilazimishwa...hakika alikuwa mpumbavu! (uk. 11).

2.3.4 Ujenzi wa Tukio Moja katika Hadithi, "Maisha Yalimwendea Kombo" (Isaakwisa, 1970)

Ujenzi wa tukio moja unajitokeza katika hadithi hii kupitia kwa Ruth ambapo tunapata taswira halisi ya athari za tamaa. Tamaa yake katika anasa za dunia inampelekea kupatwa na matatizo. Kwanza, tamaa ya mapenzi kwa rafiki yake John ambaye hata ana mke na watoto inasambaratisha mapenzi halisi baina yake na Ben ambaye anampenda Ruth kwa dhati. Pili, anasa ya kwenda densi inamfanya auze mali aliyorithi kutoka kwa babake na huo unakuwa mwanzo wa kufilisika kwake. Tatu, anaishia kuishi na mwanamume asiyemjua vyema pindi anapopata uhamisho, mwanamume yuyo huyo ndiye anampora akiba yake yote. Mwisho, tamaa inamsababisha Ruth kufariki anapokwenda katika baa kutafuta mtu wa kumsaidia baada ya kuporwa. Aidha, tukio linalojengwa ni la athari hasi inayoibuka kutokana na tamaa:

> ...Ruth akakubali kwa furaha. Baadaye wakaondoka kwa gari huku wakiwa wamepakia machupa ya pombe...walishtukia gari yao imeingia chini ya lori kubwa. Ile gari yao ilisagwa sagwa kabisa hata wao pia... (uk. 44).

2.3.5 Ujenzi wa Tukio Moja katika Hadithi, “Mzee Khamis, Leo wapi?” (Mohamed, 1971)

Tukio moja kuu la kuonyesha athari ya ulafi linajengwa katika hadithi. Mzee Khamis haogopi namna watu wanavyomsema kuwa anapenda kula ilimradi yeye ale hadi ashibe. Kutokana na ulafi uliomjaa hasubiri kualikwa katika hafla yoyote ile. Tabia hii imemkithiri kiasi cha kwamba akitembea huulizwa, “Leo wapi?”. Sherehe iwapo mbali hujikakamua bora afike. Mzee Khamis karibu aage dunia kutokana na ulafi wake kwa sababu anaamua kujitosa majini kusudio likiwa kuwahi hafla kisiwani Tumbatu. Hivyo basi, tukio linalosukwa ni la athari ya uroho ambao unabainka kupitia kwa Mzee Khamis kwani hata anapopelekwa hospitalini anaomba asilazwe ili awahi wali wa maulidi ya Mpapa:

> Wali wa Tumbatu umemkosa naye kaukosa. Lahaula, alizidi kukumbukia siku ya pili...siku ya maulidi ya Mpapa!... Nitakimbia tu, Mpapa siwezi kuikosa. (uk. 11).

2.3.6 Ujenzi wa Tukio Moja katika Hadithi, “Malipo Duniani, Hesabu Ahera” (Said, 1971)

Katika hadithi hii, mwandishi amefanikiwa kuonyesha namna ambavyo mambo anayoyatenda mtu kwa mwengine huja yakamrudia pia. Kupitia kwa watoto wa mzee Miraji ambao ni Fatuma na Kombo ni wazi kuwa tabia za watoto hutofautiana na ni jukumu la mzazi kutochoka kuwapa wasia. Kombo amesawiriwa kuonyesha kuwa mtoto anaposumbua wazazi wake hata anapoamua kubadilika kuna uwezekano mkubwa naye apate mtoto atakayetokea kumsumbua kwa kuwa mtukutu. Miraji ni mtoto wa Kombo,

anatokea kuwa mtukutu kama Kombo alivyokuwa mtukutu katika udogo wake. Kombo alikuwa anamsumbua babake ambaye ni marehemu mzee Miraji. Upo uwezekano kuwa naye marehemu babake, mzee Miraji alikuwa akimsemesha babu yake Kombo. Kisio hili linatokana na swali linaloulizwa mwishoni kuwa msomaji ana lipi la kusema kuhusu vitushi vya hadithi. Tukio limejengeka vyema kiasi cha kuafiki mada ya hadithi kuwa malipo ni duniani na hesabu ni ahera:

> ...wengine wanasema ati Kombo amekosa radhi za mzee wake, na mwenyewe Subhana anamlipa hapa hapa duniani kwa kumbarikia Miraji. Je, wewe unafikiri vipi? (uk. 14).

2.3.7 Ujenzi wa Tukio Moja katika Hadithi, "Sina Rafiki" (Wahab, 1977)

Suala moja kuu linalojengwa katika hadithi hii ni la namna ambavyo tamaa ya pesa huharibu urafiki na hata kusababisha mauti. Kupitia kwa Hasan, inabainika kuwa tamaa ya pesa inamtia katika kamari. Tamaa iyo hiyo inamfanya azidi kukopa pesa nyingi. Licha ya hilo, anaamua kumuua rafiki yake Karama kusudi arithi mali yake hususani pesa. Isitoshe, anapomwoa Bi. Asha mke wa marehemu; Hasan anamuua anapogundua kuwa pesa alizokusudia kupata amezikosa. Mwisho tamaa hii inamfanya kukabiliwa na mkono wa sheria. Anahukumiwa kufungwa maisha kupitia uchunguzi wa polisi na hatimaye uamuzi wa mahakama. Tukio la tamaa ya pesa na athari za tamaa limejengwa ipasavyo katika hadithi hii:

> ...Baada ya mwezi kupita, watu walisikia katika redio kuwa, mahakama kuu ya nchi imemhukumu Hasan Ali kunyongwa kwa kosa la kumuua Karama Said na mkewe Bi. Asha binti Sudi...(uk. 11).

2.3.8 Ujenzi wa Tukio Moja katika Hadithi, “Mke Wangu” (Muhammed, 1977)

Changamoto za ndoa ndilo tukio linalojengwa katika hadithi hii. Ingawa msimulizi hakutaka ndoa yake ipate changamoto kama zile zinazowakumba wenzake mjini, anaishia kuingia katika ndoa yenye changamoto zaidi. Tofauti baina ya ustaarabu wa mjini na kijijini inakuwa chanzo cha kutoelewana kwao katika ndoa. Anapodhani kuwa atamwelekeza mke wake, mambo yanakuwa tofauti maana mkewe naye anaona mumewe ana taabu nyingi za kutojua majukumu yake na anafaa kuelekezwa. Hali hii inamfanya Aziza kumuita mumewe gumegume. Changamoto hizi zinamzidi Aziza hadi mwisho anahiari kumuomba mumewe talaka mbele ya Seluwa na muuza madafu. Tukio linalolengwa hapa ni changamoto za ndoa:

> ...tumekaa kwa kuwa umenioa tu, lakini si mume wangu. Nitashukuru kama utanipa talaka yangu. (uk. 57).

Kupitia kwa ujenzi wa tukio moja katika kila hadithi inakuwa rahisi kwa msikilizaji na msomaji kuelewa dhamira na maudhui ya hadithi fupi husika. Kwa mujibu wa Poe (1842; 1846) ujenzi wa tukio moja katika hadithi hufanikishwa na kujikita katika mgogoro mmoja. Hivyo basi, utathmini wa hadithi fupi teule zilizowasilishwa katika BBC unaonyesha kuwa zinajikita na tukio moja katika kujenga maudhui na dhamira kusudiwa. Aidha, kutokana na hoja kuwa ujenzi wa tukio moja hutegemea uwezo wa mwandishi kujikita na mgogoro mmoja; utathmini wa aina ya migogoro na utatuzi wake ni muhimu katika kutathmini ubora wa hadithi fupi teule.

2.4 Aina ya Migogoro na Utatuzi wa Migogoro katika Hadithi Fupi Teule

Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999), mgogoro ni tofauti za kimatendo au kimawazo ambazo huwakumba wahusika katika kazi za fasihi na hivyo basi kujenga ploti au msuko wa hadithi. Ploti ni mpangilio wa matukio kwa namna ambavyo inabainisha vyanzo vya matukio husika (Mbatiah, 2000). Utatuzi wa migogoro husaidia hadithi kuwa na msuko wa mwanzo, kati na mwisho (Wamitila, 2002). Sehemu ya mwanzo hujikita katika mgogoro unaomhusisha nguli (mhusika mkuu) wa hadithi; sehemu ya kati hukuza mgogoro na sehemu ya mwisho ni usuluhishaji wa mgogoro. Mgogoro unaposuluhishwa vyema na kwa njia ya kueleweka huwa hadithi inapata msuko sahili. Utatuzi mzuri wa mgogoro hutokana na uwezo wa mwandishi au msimulizi kusuluhisha tukio fulani maalumu kwa kujkita na tukio hilo husika (Poe 1842; 1846 na Mbatiah, 2000). Aidha, kuna aina mbalimbali ya migogoro kama vile; mgogoro wa kisaikolojia, mapenzi, ndoa, tamaa, ulafi na malezi. Aina ya migogoro na utatuzi wa migogoro katika hadithi fupi teule unadhihirika kama ifuatavyo:

2.4.1 Aina ya Migogoro na Utatuzi Wake katika Hadithi, “Siku ya Arobaini” (Mohamed, 1970)

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), mhusika anaweza kukumbana na mgogoro unaosababishwa na mvutano wa kiakili. Mgogoro huu unaitwa mgogoro wa kisaikolojia. Mgogoro wa kisaikolojia unadhihirika katika hadithi hii pale ambapo Sadiki anapata barua kutoka kwa mtu asiyemjua. Baada ya kuisoma, anaificha mfukoni na kuingia kwake. Wahaka wa barua kutotaka ionekane na

mkewe unamfanya kuitupa chooni ili kutatua mgogoro huo wa kisaikolojia. Mgogoro wa kisaikolojia unafikia kilele wakati ambapo Bahati anasikia sifa mbaya kuhusu ukware wa mumewe kutoka kwa rafiki zake. Sifa hii inatia doa katika ndoa yake na kusababisha mgogoro wa kisaikolojia ndani yake. Katika kutatua mgogoro huu anapanga njama na kujifanya kimada kiasi cha kuandika barua inayomkutanisha na Sadiki. Sadiki anapoitikia wito wa kukutana na mwanamke asiyemjua inakuwa ni jawabu tosha kwa Bahati kuhakikisha kuwa mumewe ni mzinzi. Kwa namna hii, Bahati anautatua mgogoro wa kisaikolojia ulioko ndani yake kuhusu kiwango cha uaminifu cha Sadiki katika maisha ya ndoa:

> Sadiki alinaswa mtegoni...barua aliyokuwa ameletewa ilikuwa imetoka kwa mkewe mwenyewe, Bahati. Hadithi hii inathibitisha ule msemo maarufu wa Kiswahili, mwizi siku zake arobaini. (uk. 27).

2.4.2 Aina ya Migogoro na Utatuzi Wake katika Hadithi, “Kusoma na Kupenda” (Salim, 1970)

Katika hadithi hii, mgogoro wa hisia za mapenzi unajitokeza baina ya Zubeda na Abdu. Zubeda anavutiwa kwa Abdu wakati ambapo Abdu anajiunga na shule yake mpya. Hatimaye, wote wanaogelea katika bahari moja ya mapenzi. Wanasuluhisha mgogoro wa hisia za mapenzi kwa kuwa wapenzi. Rama ana jukumu la kuhakikisha kuwa analinda kanuni za shule na anapowaona Zubeda na Abdu wakipigana busu anawajibika kwa kutoa ripoti kwa mwalimu mkuu. Uvumi wa mapenzi ya Zubeda na Abdu unamlazimu mwalimu mkuu kuwaita na kuwaonya kuhusu suala la kujihusisha na mapenzi. Aidha, wanaporudia

kosa; anachukua hatua ya kuwaamuru waende makwao walete wazazi. Kwa namna hii, mwalimu mkuu anatatua mgogoro wa uvumi wa mapenzi ya Zubeda na Abdu. Abdu anafaya uamuzi wa kutorudi shule hiyo ili kukwepa changamoto za mapenzi maana kwake anahisi ni vigumu kumwona Zubeda na penzi likose kuendelea. Zubeda anatatua kilele cha mgogoro wa mapenzi kwa kukubali kuwa Abdu ameenda na anafaya uamuzi wa kuendelea na masomo yake. Mgogogro wa hisia za mapenzi unasuluhishwa kwa njia hiyo maalumu ya Zubea na Abdu kutengana:

> ...Sero ya meli iliyomchukuwa Abdu ilipolia, Zubeda alikuwa darasani mwake. Alijizuia, akakwinya meno na kuendelea na masomo yake... (uk. 45).

2.4.3 Aina ya Migogoro na Utatuzi Wake katika Hadithi, "Ajuta Majuto ya Mjukuu" (Somba, 1970)

Wahusika wanapokuwa na imani zinazokinzana katika mitazamo yao husababisha kuwepo kwa mgogoro (Oriedo, 2007). Migogoro ya ndoa na mapenzi inadhihirika katika hadithi hii. Wazazi wa Wayua na Kamene wanaona njia mwafaka ya kujali maisha ya binti zao ni kuwaoza mapema kwa mwanamume mwenye mali hata kama ni mzee. Kamene anapofahamu kuwa kuna sherehe ndogo ya kukamilisha ndoa yake ya lazima baina yake na Kitonga, anaamua kutia pombe sumu anapotumwa na babake. Sumu hiyo inawaua waliokuja kutoa posa, bwana harusi mtarajiwa na babake pia. Ili kuepuka balaa ya tukio la mauaji analosababisha, Kamene anatatua kilele cha mgogoro wa mapenzi na ndoa ya lazima kwa kuamua kutorokea kwa mpenzi wake Kioko. Njiani anagongwa na gari na insadifu kuwa ni Kioko

aliyemgonga. Anapopata fahamu kidogo, anasimulia chanzo cha kutoroka kwake na kueleza kuwa ndiye mtekelezaji wa mauaji ya babake. Hali yake inapozidi kuwa mbaya, Kioko anaamua kumkimbiza hospitalini ingawa baadaye anaaga dunia akipokea matibabu. Usuluhishaji wa migogoro hii ya mapenzi na ndoa unasaidia katika kujenga dhamira ya athari ya ndoa za lazima:

> ...alianza kumhadithia Kioko yote yale yaliyotukia kijijini mwao...Kamene akawa na masikitiko makubwa mno kiasi cha kumuua. Alijuta majuto ya mjukuu... (uk.11).

2.4.4 Aina ya Migogoro na Utatuzi Wake katika Hadithi, "Maisha Yalimwendea Kombo" (Isaakwisa, 1970)

Mgogoro wa tamaa unazuka katika hadithi hii ambapo mhusika Ruth anakumbwa na mgogoro wa tamaa ya mazingira ya mjini. Anaona maisha ya kijijini hayamfai na ndiposa anatatua mgogoro huo kwa kuamua kwenda mjini kuliko na starehe apendazo za ulevi na densi. Ben, ni mchumba wake Ruth. Anapokwenda kumtembelea Ruth, anabaini kuwa penzi lake halithaminiwi na hivyo basi anafanya uamuzi wa kurudi kijijini na kumwacha Ruth ambaye amemezwa na tamaa katika anasa za mjini. Rafiki ya Ruth kwa jina John anapata barua ya uhamisho, Ruth anamwambia waende wote na pia waoane lakini John anamwambia ukweli kuwa ameoa na ana watoto pia:

> ...nilikuwa sijakueleza kwamba nimeoa na nina watoto wawili... (uk.41).

Ruth anapata uhamisho na kukosa mahali pa kuishi kwa sababu ya kuwa mgeni. Anaamua kuishi chumba kimoja na dereva wa teksi. Kutokana na hulka ya wizi iliyoko na dereva wa teksi, anaamua kumpora Ruth kila kitu

akiwa kazini na anawaambia majirani wa Ruth kuwa amefukuzwa nyumba hiyo na mwenyewe. Ruth anaporudi na kugundua kuwa ameibiwa, anaamua kusuluhisha changamoto hiyo kwa kwenda baa kutafuta msaidizi. Hatimaye, anaaga dunia kutokana na ajali wanapokuwa wakitoka na msaidizi wake anayempata huko kwenye baa kutokana na kufanya uamuzi usio wa busara. Athari ya tamaa pamoja na athari ya uamuzi usio na busara inabainika kutokana na mbinu ambazo Ruth anatumia katika utatuzi wa migogoro iliyoelezwa. Ruth anapitia changamoto mbalimbali kutokana na uamuzi anaofanya mwenyewe na ukosefu wa hekima katika kutatua masaibu yanayomkumba. Mauti yake kama mhusika mkuu yanadhamiria kuufunza umma kutumia busara katika kutatua migogoro ya kisaikolojia na ikiwezekana kutafuta mtaalamu wa kisaikolojia ili kuelekezwa ipasavyo.

2.4.5 Aina ya Migogoro na Utatuzi Wake katika Hadithi, "Mzee Khamis, Leo Wapi?" (Mohamed, 1971)

Utatuzi wa mgogoro wa ulafi unadhihirika katika hadithi hii. Mzee Khamis anaposikia kuna hafla hasubiri mwaliko kwa sababu kwake anaona kula ni wajibu. Kutokana na imani yake, anafanya uamuzi wa kwenda kwa Bin Barak ili awahi wali. Watoto kwa watu wazima wanamdhihaki Mzee Khamis kwa kumuuliza; "Leo wapi?" anapokuwa njiani. Anatatua mgogoro wa ulafi uliomtawala kwa kuwapuuza tu. Anapokuwa katika maulidi kwa Bin Barak, mpishi anamfokea na kumkataza kusongea kwenye chakula. Mzee Khamis anamjibu kwa sauti awache kugombania shughuli isiyo yake. Mgogoro mwengine ni baina yake na paka. Paka anapotafuna nyama yake anaamua

kufunga dirisha na kumwadhibu lakini kilele cha mgogoro huu ni wakati ambapo paka anapandwa na mori unaomfanya kumrukia usoni na kumrarua. Mzee Khamis anafungua mlango na kutoka. Maulidi yanapotokea kisiwani Tumbatu; anaamua kwenda kwa mguu licha ya umbali wa safari. Anapofika Mkokotoni anaamua kuogelea ili awahi wali kutokana na kukosa mtumbwi wa kumvusha. Ananusurika kifo kutokana na uroho wake kwani mzee mmoja mkongwe ndiye anamwokoa kupitia ngarawa yake. Utatuzi mzuri wa mgogoro wa ulafi unafanikisha ujenzi bora wa msuko (Naude na wenzake; 2009):

> Alipofumbua macho alijihisi yumo ndani ya behewa. Akaangaza mle ndani akajihisi yumo kwenye gari la hospitali...upande wa kulia alikuweko babu mmoja mkongwe amekaa. Huyu alikuwa ni bwana aliyemwokoa Mzee Khamis... (uk. 11).

2.4.6 Aina ya Migogoro na Utatuzi Wake katika Hadithi, "Malipo Duniani, Hesabu Ahera" (Said, 1971)

Mgogoro wa malezi unakuzwa na hatimaye kusuluhishwa katika hadithi hii. Mgogoro wa kwanza ni baina ya baba na mwanawe. Mzee Miraji anapogundua Kombo ni mtukutu hawachi kumshauri awache tabia yake mbaya. Mwishowe, anapokaribia kufa baada ya kuugua anamwambia iwapo anataka radhi zake abadilike na awe mtiifu. Punde babake anapoaga dunia inambidi Kombo kubadilika. Mgogoro mwingine ni kati ya Kombo na walimu wake. Ingawa ni mtundu, walimu wanampa nafasi ya kushiriki riadha na anawaletea tuzo za vikombe. Aidha, upo mgogogro kati ya Kombe na rafiki zake. Baada ya shughuli za mazishi ya babake, siku inayofuata rafiki zake wanakuja kumuita asubuhi ili wakapige njiwa kwa manati lakini anawafokea

na kuwafukuza kwani ni wazi kuwa anafanya uamuzi wa kubadilika na kuwa mwenye nidhamu. Kuongezea, kuna mgogoro kati ya Kombe na mwanawe Miraji; Mwanawe ni mtukutu sana lakini Kombo hawachi kumshauri na kumkemea ili akome utukutu. Majirani hawakosi kusema kuwa utukutu wa Miraji ni malipo kwa Kombe kwa namna ambavyo alikuwa anamsumbua marehemu babake. Kauli hizi zinamfanya Kombe kuikabili hali iliyoko ya kumshauri mwanawe hadi atakapoamua kubadilika:

> Kombo alikuwa kama wazimu kwa makelele anayopiga mara kwa mara kumkemea Miraji... (uk. 14).

2.4.7 Aina ya Mgogoro na Utatuzi Wake katika Hadithi, "Sina Rafiki" (Wahab, 1977)

Lavanya (2013) anaeleza kuwa mwanadamu anaweza kukabiliana na mgogoro wa kibinafsi kutokana na hali yake ya kimaisha. Hadithi hii inasukwa kwa ujenzi wa mgogoro wa tamaa. Hasan anapokosa pesa baada ya kuwa mwathiriwa wa ulevi na kamari anaona suluhu ni kumkopa rafiki yake Karama. Mara kwa mara, Karama anakuwa wa kusuluhisha ugomvi baina ya Hasan na wanaomdai pesa. Hasan anaona njia mwafaka ya kupata pesa za Karama ni kutoweka pikipiki ya Karama breki na anapofanya hivyo anafanikiwa kumuua kupitia kwa ajali. Anamshawishi Bi. Asha kumuoa kama njia ya yeye kupata mali ya Karama kwa wepesi. Anapokosa pesa alizokusudia anaamua kumuua Bi. Asha kutokana na hamaki. Mahakama inaamua kumhukumu Hasan kifungo cha maisha baada ya kumpata na hatia ya mauaji. Mgogoro wa tamaa unaokuzwa na kutatuliwa ipasavyo unaipa hadithi uhalisia:

> ...kumbe kweli umemuua rafiki yako kwa pesa, lo! na sasa unataka kuniua mimi. Rafiki gani? Sina rafiki mimi! Niambie pesa umezipeleka wapi!... (uk. 11).

2.4.8 Aina ya Mgogoro na Utatuzi Wake katika Hadithi, "Mke Wangu" (Muhammed, 1977)

Utatuzi wa mgogoro wa ndoa unajitokeza katika hadithi hii. Mgogoro wa kwanza ni baina ya msimulizi na wazazi wake. Wazazi wanajituma kumchagulia msimulizi mwanamke wa kwanza na wa pili lakini anawakataa na hatimaye wanapomtajia Aziza anaridhia na kumuoa maana ana sifa atakazo msimulizi. Mgogoro mwengine ni baina ya msimulizi na mkewe kwa sababu anaona kwamba mkewe anapenda kumchuja. Anapomuuliza sababu, mkewe anamwambia hakudhania angepata gumegume maana msimulizi hafanyi kazi anategemea wapewe chakula na wazazi wa msimulizi. Msimulizi anapojaribu kujitetea kuwa anatafuta kazi ila hajapata kazi, anaambiwa tatizo lake ni kuwa yeye ni mchagua kazi maana hata kuchoma mihogo ni kazi:

> ...mkisha kusoma hicho Kizungu chenu mnakuwa basi tena, hamfanyi kazi ila ya uboi, mkae mkitumwa. Unadhani kwetu shamba yupo kijana wa makamo yako wewe, naye hana kazi?...bwana wa mjini, huwezi kukwea minazi ukaangusha nazi, kadhalika huwezi kuchunga punda, basi huwezi hata kununua mihogo, ukakaa kuichoma hapo chini... (uk. 51).

Msimulizi anashangaa anaponunua mswaki ila mkewe hautumii; anapomuuliza mkewe, anamwambia hataki kupata madhara ya vitu vya kisasa ndiposa anatumia mti wa mnazi na dawa yake ya kusaga iliyochanganywa viungo. Aziza anapomuita bazazi wa madafu anamwambia msimulizi kuwa bazazi ni kielelezo cha mume ambaye angemtaka kwa sababu anajituma

kikazi. Anamwambia iwapo atampa talaka itakuwa bora zaidi. Mgogoro wa ndoa unaokuzwa na kusuluhishwa unaipa hadithi hadhi ya ubora.

Forster (1927) anaunga mkono kauli ya Poe (1842; 1846) kuwa utatuzi mzuri wa mgogoro hufanikisha ujenzi wa ploti au msuko. Utathmini wa hadithi fupi teule zilizowasilishwa katika BBC unaonyesha kuwa migogoro inayoibuka katika hadithi fupi teule inatolewa suluhu ipasavyo na hivyo basi kufanikisha ujenzi mzuri wa msuko. Kutokana na utatuzi huu wa mgogoro, msomaji au msikilizaji anapata uwezo wa kukumbuka matukio katika hadithi fupi teule. Mgogoro na utatuzi wake ni muhimu katika hadithi fupi kwa sababu kila hadithi fupi teule imeibuka kuwa na mgogoro wake unaotegemea dhamira hadithi inakusudia kuwasilisha.

2.5 Matumizi ya Lugha katika Hadithi Fupi Teule

Mohamed (1995) anaeleza kuwa matumizi ya lugha hujihusisha na matumizi ya tamathali mbalimbali za semi kama vile kinaya au kijembe pamoja na mbinu za sanaa katika kuwasilisha ujumbe wa kifasihi kwa njia ya mvuto. Msomaji au msikilizaji anaposoma kazi ya hadithi fupi iliyotumia lugha kwa mvuto, huvutiwa na kazi husika jambo linalomfanya aendelee kusoma au kusikiliza (Omar, 2010). Hivyo basi, lugha ya hadithi zilizowasilishwa katika BBC imeendelezwa kwa tamathali mbalimbali na kupata mvuto uliofanya hadithi husika kusomwa hewani katika idhaa ya redio na hatimaye kuchapishwa. Tamathali hizi ni kama vile; Taswira, chuku, msemo, lakabu, methali, nahau, sadfa, uzungumzinafsi, nidaa, tabaini, balagha na kinaya.

2.5.1 Taswira

Taswira ni mkusanyiko wa picha ambazo humjia msomaji au msikilizaji wa kazi za fasihi. Taswira huwa na dhima ya kunasa hisia za msomaji ama msikilizaji (Wanga, 2017). Katika hadithi ya “Siku ya Arobaini” (Mohamed, 1970), taswira ya kuona mazingira yalivyo inadhihirika tunapoambiwa jinsi jua lilikuwa likiingia chumvini, na jinsi lilivyo jekundu, likitapakaza rangi ya dhahabu kwenye bahari, juu ya meli zilizotia nanga, ngarawani, mbinguni na kote: na hata bandari chafu ya kisiwa cha pale ilionyesha kama iliyonyewa na mvua ya damu (uk. 24-25). Katika hadithi “Kusoma na Kupenda”, (Salim, 1970) mwandishi anaeleza kuwa wanafunzi wengi wanasukumana vibega, wengine wanakonyezeana na wengine wananong’ona na kucheka (uk. 41). Maelezo haya yanatupa picha ya namna wanafunzi hufanya wanapoona mwanafunzi mgeni shuleni. Hadithi ya “Malipo Duniani, Hesabu Ahera” (Said, 1971) inatupa taswira ya ulitima tunapoelezwa kuwa nyumba ya Mzee Miraji imeezekwa madebe ya samli yaliyonunuliwa kwa muuzaji madebe mabovu (uk. 12).

2.5.2 Chuku

Chuku ni wakati ambapo kauli au jambo hutiwa chumvi sana (Msokile, 1993). Chuku inabainika katika hadithi ya “Siku ya Arobaini” (Mohamed, 1970). Tunapata maelezo kuwa Sadiki hakutosheka na mke mmoja wala mia moja (uk. 25). Hali hii inaleta dhana ya kuwa Sadiki ni mwanamume ambaye anapenda wanawake kupita kiasi. Katika hadithi ya “Mzee Khamis, Leo wapi?” (Mohamed, 1971), Ulafi wa Mzee Khamis unapigiwa chuku

mwandishi anaposema kuwa mwezi wa mfungo; sita humpata kwa furaha na mzee huyu hutanua pua ili kunusia harufu ya vyakula (uk. 7). Aziza anatumia chuku anapomwambia mumewe katika hadithi, “Mke Wangu” (Muhammed, 1977) kuwa hata akachukuwa mwiba na kumshindilia wayoni utavunjika (uk. 52).

2.5.3 Msemo

Msemo ni fungu la maneno linalotoa ujumbe wenye ukweli kwa njia ya muhtasari. Misemo hutofautiana kwa kiasi na nahau kwa sababu misemo haizingatii muundo wa kitenzi na nomino (Wamitila, 2006). Namna ambavyo Mzee Khamis anapenda kula inasemekana ni vita vya *kufa na kupona* (uk. 8). Msemo wa *kufa na kupona* katika hadithi, “Mzee Khamis, Leo Wapi?” (Mohamed, 1971) umetumiwa ili kuipa hadithi taswira ya ulafi usio na mfano ambao umemjaa mzee huyu. Katika hadithi ya “Mke Wangu” (Muhammed, 1977), msemo umetumiwa wakati ambapo msimulizi anaposema *mtoto mbichi* (uk. 48). Maana yake ni msichana mwanamwali ambaye hajajitosa katika anasa za kidunia.

2.5.4 Lakabu

Lakabu ni majina ya kubandikwa ambayo mtu hupewa na mtu au watu kutokana na tabia au hali yake. Kwa mujibu wa hadithi ya “Kusoma na Kupenda” (Salim, 1970), ukali wa mwalimu mkuu unafanya aitwe *Hitler* (uk. 40). Hivyo basi, lakabu imetumika ili kuipa lugha mvuto na kuonyesha namna ambavyo ukali wake umepita kasi. Mwandishi anatumia lakabu *Ba-jinga*

katika hadithi, “Mzee Khamis, Leo wapi?” (Mohamed, 1971) kuonyesha upumbavu wa Mzee Khamis wa kujifungia ndani ya nyumba na paka ili ampe adhabu kwa kumpiga kwa bakora na mwishowe paka anamtia majeraha ya kumrarua kwa kucha (uk. 10). Katika hadithi ya “Malipo Duniani, Hesabu Ahera” (Said, 1971), Kombo anapewa lakabu *Simba* na wenzake kutokana na ushujaa pamoja na ukali wake hapo shuleni (uk. 12).

2.5.5 Methali

Kwa mujibu wa Wamitila (2001) methali ni msemo unaojitosheleza kimaana, wenye nguvu, muundo au sifa za kishairi na hukusudia kuelekeza, kuadhibu au kuelimisha. Vilevile, methali ni semi fupifupi za kimapokeo zinazoeleza fikra, maarifa, hekima na mafunzo yatokanayo na uzoefu wa jamii maalumu. Hadithi ya “Kusoma na Kupenda” (Salim, 1970) inakamilika kwa methali; *moyo wa kupenda na kuwiza huwa* (uk. 45). Methali imetumika kukusudia kushauri. Katika hadithi ya “Maisha Yalimwendea Kombo” (Isaakwisa, 1970), Ruth anapojifanya mwerevu sana anafanya uamuzi usio wa busara wa kwenda kustarehe kwa ulevi na densi mjini ndiposa mwandishi anasema *akili nyingi huondoa maarifa* (uk. 37). Kuongezea, methali imetumika kuelimisha na kuonyesha kutowezekana kwa jambo wakati John anamwambia Ruth wazi hawezi kumuoa maana tayari ana mke na watoto ndiposa anatumia methali *maji yakimwagika hayazoleki* (uk. 41).

2.5.6 Nahau

Nahau ni fungu la maneno ya kawaida lenye maana isiyotokana moja kwa moja na maneno yaliyounda fungu hilo la maneno (Matei, 2011). Mara nyingi nahau huundwa kwa kitenzi na nomino. Nahau imetumika katika hadithi ya "Kusoma na Kupenda" (Salim, 1970) wakati ambapo mwandishi anasema Abdu *anajikaza kisabuni* (uk 40). Nahau hii inamaanisha kuwa Abdu anajituma ipasavyo kumshawishi Zubeda asiogope. Katika hadithi,"Ajuta Majuto ya Mjukuu" (Somba, 1970) inasemekana kuwa wageni *wanachapa mtindi*; nahau yenye maana kunywa kileo imetumika ili kuipa lugha mvuto (uk. 10). Katika hadithi, "Maisha Yalimwendea Kombo" (Isaakwisa, 1970) Ruth anazidiwa na ulevi ndiposa nahau ya *kuchapa mtindi* (uk. 38) inatumika kuonyesha anajiingiza katika ulevi.Vilevile, katika hadithi ya "Mzee Khamis, Leo Wapi?" (Mohamed, 1971) nahau *kutwanga njia* imetumika yenye maana ya mwendo mrefu anaotembea Mzee Khamis baada ya kuamka mapema (uk. 10).

2.5.7 Sadfa

Utukiaji wa matukio kwa wakati mmoja kama yalipangwa kutukia pamoja lakini kwa hali halisi hayakupangwa kutukia pamoja huitwa sadfa (Wamitila, 2003). Mbinu hii inatumika katika hadithi, "Ajuta Majuto ya Mjukuu" (Somba, 1970) wakati ambapo Kamene anatoroka na inatokea anagongwa kwa gari linaloendeshwa na mpenzi wake Kioko (uk. 11). Katika hadithi ya "Mzee Khamis, Leo Wapi?" (Mohamed, 1971), sadfa inatumika wakati ambapo Mzee Khamis anaota nyama yake inaliwa na paka na anapogutuka usingizini

anampata paka wake akishambulia nyama (uk. 9). Matumizi ya sadfa yanapatia tukio hili uhalisia wenye dhima ya kujenga taharuki katika hadithi.

2.5.8 Uzungumzinafsi

Uzungumzinafsi ni mazungumzo ambayo hudhihirika ndani ya fikra za mhusika na matumizi yake huwa na dhamira ya kukuza msuko (Wamitila, 2003). Uzungumzinafsi unabainika katika hadithi ya "Mzee Khamis, Leo Wapi?" (Mohamed, 1971) wakati Mzee Khamis anapostaajabia wingi wa chakula katika maulidi ya Bin Barak (uk. 7). Matumizi ya mbinu hii ni kuonyesha namna ambavyo mzee huyu ametawaliwa na ulafi katika maisha yake. Katika hadithi ya "Sina Rafiki" (Wahab, 1977), Hasan anasumbuka akili akijiuliza mahali pa kupata pesa (uk. 1). Hangaiko hili linamfanya kujizungumzia na hivyo kufanikisha ujenzi wa maudhui ya mgogoro na tamaa.

2.5.9 Nidaa

Nidaa ni mbinu ya lugha ambayo huonyesha hisia za msemaji. Nidaa imetumika katika hadithi, "Mzee Khamis, Leo Wapi?" (Mohamed, 1971) wakati Mzee Khamis anaposema hawezi ngoja kualikwa kisha anatamka tamko *mawe!* (uk. 7). Katika hadithi ya "Mke Wangu" (Muhammed, 1977), nidaa imetumika msimulizi anapofoka neno *Rabi*! (uk. 54). Anafoka neno hilo baada ya kushindwa atafanya nini ili aweze kumwelekeza mkewe asiyetaka mambo ya usasa.

2.5.10 Tabaini

Tabaini ni mbinu ya lugha ambayo hutumika ili kuleta dhana ya kusisitiza katika kazi ya fasihi na mara nyingi hutumia maneno ya ukinzani (Msokile, 1992). Tabaini imetumika katika hadithi ya "Mzee Khamis, Leo Wapi?" (Mohamed, 1971) ili kusisitiza. Mzee Khamis ananusurika katika mauti na inasemekana hakumbuki kitu si wali, si nyama, si Tumbatu labda lepe la mauti (uk 11). Urembo wa Fatuma unasifiwa katika hadithi, "Malipo Duniani, Hesabu Ahera" (Said, 1971) tunapoelezwa ana umbo la wastani si mnene si mwembamba (uk 12). Katika hadithi ya "Malipo Duniani, Hesabu Ahera" (Said, 1971), Mzee Miraji anaugua sana na inasemekana kuwa si wa siku hiyo si wa siku inayofuata (uk 13). Tabaini hii imetumika kusisitiza kuwa anaugua sana na kifo chake ni cha wakati wowote ule na inatokea anaaga siku inayofuata saa mbili unusu asubuhi.

2.5.11 Balagha

Kwa mujibu wa Oriedo (2007), balagha ni maswali ambayo huulizwa huku muulizaji akiwa na jawabu ama akiwa na jibu analotarajia. Hadithi ya "Malipo Duniani, Hesabu Ahera" (Said, 1971) inaisha kwa swali la balagha maana msimulizi anauliza ipi ndiyo sababu ya Kombo kupata mwana msumbufu (uk 14). Hili ni swali ambalo huenda msimulizi ana jawabu kwa sababu wakati Mzee Miraji alipokuwa hai Kombo alimsumbua basi naye kuna uwezekano analipwa duniani kwa kumpata mwana msumbufu. Balagha imetumika kukejeli katika hadithi, "Mke Wangu" (Muhammed, 1977). Aziza anamkejeli

msimulizi na kumuuliza iwapo ni kwema? (uk 50). Swali hili la balagha lina dhima ya kusisitiza uchungu na majuto ya Aziza katika ndoa yake.

2.5.12 Kinaya

Kinaya ni wakati ambapo mambo hutokea kinyume na matarajio ya msomaji au msikilizaji (Msokile, 1993). Kinaya kinadhihirika katika hadithi ya “Mzee Khamis, Leo Wapi?” (Mohamed, 1971). Mzee Khamis anakula nyama zote katika sherehe ya maulidi kisha mwongeza nyama anapopita anaanza kulalamika wali wake haukutiwa nyama (uk. 9). Katika hadithi, “Sina Rafiki” (Wahab, 1977) inakuwa ni kinaya wakati ambapo Hasan anaunda pikipiki ya Karama na kutoiweka breki makusudi jambo linalomsababishia Karama ajali ya mauti ilhali Karama ni rafiki yake Hasan wa karibu (uk. 3).

Kutokana na matumizi ya vipengele mbalimbali vya lugha waandishi wa hadithi fupi hizi wamefanikiwa katika kusanii kazi zenye mvuto wa aina yake. Kazi ambazo msomaji au msikilizaji anatamani kuzitalii zaidi ya mara moja. Aidha, matumizi haya ya lugha yamechangia katika kukuza dhamira na maudhui ya hadithi fupi teule. Poe (1842; 1846) anaeleza kuwa lugha ina uwezo mkubwa wa kunasa hisia za msomaji au msikilizaji. Tahakiki ya hadithi fupi teule inadhihirisha kuwa kipengele cha taswira kimetumiwa kwa kiasi kikubwa kuliko vipengele vingine vya lugha ili kujenga dhamira na maudhui ya hadithi kwa muda mfupi. Matumizi ya lugha katika hadithi hizi yamesaidia katika kutathmini ubora wa hadithi fupi teule zilizowasilishwa katika idhaa ya redio ya BBC kwa mtazamo wa Poe. Hivyo basi, Poe

amefanikiwa katika kuweka msingi huu kama mojawapo wa msingi wa utathmini wa ubora wa hadithi fupi.

2.6 Hitimisho

Sura hii imeangazia miundo ya hadithi fupi teule zilizowasilishwa katika *British Broadcasting Corporation* (BBC). Mihimili ya nadharia ya hadithi fupi iliyoasisiwa na Poe (1842; 1846) imesaidia katika kutathmini; mtiririko wa mawazo katika hadithi teule, ujenzi wa tukio moja katika kuwasilisha maudhui lengwa, ujenzi mwema wa ploti au msuko kutokana na utatuzi mzuri wa aina ya mgogoro husika na matumizi ya lugha katika usanii wa hadithi fupi. Mihimili hii imesaidia katika kukadiria kiwango cha ubora wa hadithi fupi teule ambazo zilisomwa katika idhaa ya redio ya BBC na hatimaye kuchapishwa katika mikusanyiko: *Mapenzi ni Kikohozi* (1970), *Vituko Duniani* (1970), *Pavumapo Palilie* (1971) na *Kinywa Jumba la Maneno* (1977). Sura inayofuata itaeleza usawiri wa wahusika katika hadithi fupi teule zilizowasilishwa katika idhaa ya redio ya BBC.

SURA YA TATU

USAWIRI WA WAHUSIKA KATIKA HADITHI FUPI TEULE

3.1 Utangulizi

Kulingana na Ngara (1982), uhakiki wa kifasihi hujumuisha dhana ya wahusika na uhusika wao katika kazi husika. Kwa kurejelea nadharia ya mtindo iliyoasisiwa na Leech (1969); dhana ya wahusika na uhusika imetumika kueleza usawiri wa wahusika katika hadithi fupi teule. Katika sura hii, nadharia ya mtindo imetumika ili kufidia upungufu wa nadharia ya hadithi fupi ambayo imejikita zaidi na suala la miundo ya hadithi fupi teule (Mbatiah, 2000). Vigezo ambavyo vimetumiwa katika kutathmini usawiri wa wahusika katika hadithi fupi teule ni: aina ya wahusika, idadi ya wahusika pamoja na jukumu la wahusika katika hadithi fupi teule, uthabiti wa wahusika, mshabaha wa lugha ya wahusika na ile ya hadhira lengwa ili dhamira na maudhui ya hadithi kueleweka kwa usahili na kusadikika kwa wahusika pamoja na sababu wazi za matendo yao. Vipengele hivi vimesaidia katika kueleza usawiri wa wahusika katika hadithi fupi teule zilizowasilishwa katika idhaa ya redio ya *British Broadcasting Corporation* (BBC).

3.2 Aina ya Wahusika

Kwa mujibu wa Forster (1927), wahusika katika hadithi fupi huwa wa aina mbalimbali na jukumu la kila mhusika hujitokeza ndiposa kumweka kila mhusika katika aina yake mahsusi. Aina ya wahusika hueleweka vyema kutokana na jukumu ambalo wamepewa katika hadithi, jukumu hilo hurejelewa kama uhusika wao (Msokile, 1993). Kulingana na Njogu na

Chimerah (1999) jukumu la mhusika huwa muhimu katika kuendeleza dhamira na maudhui ya hadithi fupi husika. Vilevile, aina ya mhusika hubainishwa na jukumu lake katika kazi nzima, wanayoyasema wahusika wengine kuhusu mhusika na mahusiano yake na wahusika wengine (Wanga, 2017). Aina ya wahusika katika hadithi fupi ni kama vile; wahusika wakuu, wahusika wasaidizi, wahusika wadogo, wahusika bapa, wahusika mviringo na wahusika foili. Wahusika hawa wanajitokeza katika hadithi fupi teule za mikusanyiko teule kama ifuatavvyo;

3.2.1 Wahusika Wakuu katika Hadithi Fupi Teule

Kwa mujibu wa Forster (1927), hadithi fupi huwa na mhusika mkuu ambaye huhusishwa na takriban visa vyote katika hadithi. Mhusika mkuu hujitokeza kutoka mwanzo wa hadithi hadi mwisho wa hadithi. Mhusika mkuu huenda akawa mmoja au wawili katika hadithi fupi husika (Msokile, 1992). McCarthy (2000) anaeleza kuwa mhusika mkuu anapokuzwa vyema hadithi hupata mvuto mzuri kwa msomaji au msikilizaji. Wahusika wakuu wanajitokeza kama ifuatavyo kwenye hadithi fupi teule za mikusanyiko teule:

Katika hadithi, “Siku ya Arobaini” (Mohamed, 1970) wahusika wakuu ni wawili ambao ni Sadiki na Bahati. Wahusika hawa wanajitokeza kutoka mwanzo wa hadithi hadi mwisho wa hadithi. Wanasawiriwa ili kukuza dhamira kuu ya hadithi ambayo ni kusisitiza kuhusu uaminifu katika maisha ya ndoa.

Wahusika Abdu na Zubeda katika hadithi, “Kusoma na Kupenda” (Salim, 1970) ndio wahusika wakuu. Kupitia kwa wahusika hawa, maudhui ya elimu yanawasilishwa na jamii inahamasishwa kuhusu umuhimu wa kuzingatia elimu miongoni mwa vijana maana elimu hailandani na mapenzi hasa kwa wanafunzi.

Katika hadithi, “Ajuta Majuto ya Mjukuu” (Somba, 1970) Kamene anaibuka kuwa mhusika mkuu. Kamene amekuzwa kuanzia mwanzo wa hadithi hadi mwisho wa hadithi. Kamene anafanikisha dhamira kuu ya hadithi ambayo ni kukashifu ndoa za mapema miongoni mwa wasichana wadogo. Anapotaka kuozwa na wazazi wake kwa Kitonga; anamuua Kitonga, babake, walioandamana na Kitonga na yeye pia anapata ajali na kuaga dunia anapokuwa akitorokea mauti anayotekeleza.

Mhusika Ruth anajitokeza kama mhusika mkuu katika hadithi, “Maisha Yalimwendea Kombo” (Isaakwisa, 1970) kwa sababu ni kupitia kwake ambapo dhamira ya hadithi inakuzwa. Dhamira katika hadithi ni kukashifu ulevi miongoni mwa wanajamii. Anafanya uamuzi wa kujiingiza katika anasa za densi na ulevi ambazo zinamwathiri katika maisha yake hadi mwishoni anaaga dunia kutokana na ajali akiwa mlevi pamoja na mwanamume anayeandamana naye wanapotoka kwenye baa.

Katika hadithi, “Mzee Khamis, Leo Wapi?” (Mohamed, 1971) mhusika mkuu ni Mzee Khamis ambaye anapatia hadithi mada yake. Amesawiriwa kuanzia

mwanzo wa hadithi hadi mwisho wa hadithi. Kupitia kwa Mzee Khamis mwandishi wa hadithi anafaulu katika kuwasilisha maudhui ya tamaa na ulafi pamoja na athari za tamaa na ulafi.

Mhusika Kombo anabainika kama mhusika mkuu katika hadithi, “Malipo Duniani Hesabu Ahera” (Said, 1971). Dhamira kuu ya mwandishi ni kukashifu usumbufu au utukutu miongoni mwa watoto, hasa wakati wa malezi kutoka kwa wazazi wao. Kombo anajitokeza kama mhusika mkuu kwa sababu ni kupitia kwake ambapo mwandishi anafanikisha dhamira yake. Anawasumbua wazazi wake wakati wa malezi na hatimaye anapooa na kupata mtoto, anajaaliwa mtoto msumbufu zaidi yake alivyokuwa anawasumbua wazazi wake.

Katika hadithi, “Sina Rafiki” (Wahab, 1977) Hasan na Karama wanajitokeza kama wahusika wakuu. Hasan na Karama wamesawiriwa kuanzia mwanzo wa hadithi hadi tamati ya hadithi. Wanategemeana katika shughuli za maisha lakini wivu unamfanya Hasan kumuua rafiki yake Karama. Hasan anapoulizwa na Bi.Asha ambaye ni mke wa Karama mbona alifanya ukatili wa kuua Karama anakiri kuwa hana rafiki.

Msimulizi na Aziza wanakuzwa na mwandishi kuanzia mwanzo hadi tamati ya hadithi, “Mke Wangu” (Muhammed, 1977) ili kujenga maudhui ya mgogoro katika maisha ya ndoa. Kupitia kwa wahusika hawa, maudhui ya asasi ya ndoa yanabainika wazi na hivyo basi wanajitokeza kama wahusika wakuu.

Wahusika wakuu wamejitokeza kuanzia mwanzo hadi mwisho katika kila hadithi fupi teule ili kujenga dhamira na maudhui ya hadithi. Hivyo basi, wahusika wakuu ni uti wa mgongo katika kusanii hadithi fupi kwa sababu wamekuza dhamira na maudhui ya hadithi fupi teule. Wahusika hawa wamechangia katika uwasilishaji wa hadithi fupi teule zilizoibuka kuwa bora na kuwasilishwa katika idhaa ya redio ya Kiswahili ya BBC.

3.2.2 Wahusika Wasaidizi katika Hadithi Fupi Teule

Wahusika wasaidizi hutumika katika kujenga mhusika mkuu na hivyo basi kumsaidia msomaji au msikilizaji kumwelewa mhusika mkuu vyema (Njogu na Chimerah, 1999). Mwingiliano wa mhusika msaidizi na mhusika mkuu humpa msomaji mwangaza zaidi kumhusu mhusika mkuu. Hata hivyo, huenda wahusika wasaidizi kuwa na visa vyao ingawa kazi yao ni kuwajenga au kumjenga mhusika mkuu. Mbinu ya kisasa ya kusanii wahusika wasaidizi ni kuwajenga sambamba na mhusika mkuu huku wakihusishwa na migongano mbalimbali (Msokile, 1992). Wahusika wasaidizi wanabainika kama ifuatavyo kwenye hadithi fupi teule:

Katika hadithi, “Siku ya Arobaini” (Mohamed, 1970) shoga zake Bahati wanamwelezea Bahati kuhusu tabia ya mumewe Sadiki ya kupenda wanawake wengine. Kupitia kwa shoga zake Bahati, mhusika Sadiki anajengwa na shoga zake Bahati kama mhusika mzinzi na mkware. Vilevile, wanamsawiri Bahati kama mwanamke ambaye katika jamii ana nafasi ya kutetea ndoa yake.

Mhusika Rama, wanafunzi katika darasa la Abdu na Zubeda na mwalimu mkuu ni wahusika wasaidizi katika hadithi, “Kusoma na Kupenda” (Salim,1970) kwa sababu ni kupitia kwa wahusika hawa ambapo maudhui ya mapenzi baina ya Abdu na Zubeda yanaelezwa. Rama na wanafunzi katika darasa la Abdu na Zubeda wanamfikishia mwalimu mkuu habari za mapenzi baina ya Abdu na Zubeda. Mwalimu mkuu anajenga maudhui ya elimu kwa kuwatuma nyumbani wawaite wazazi wao shuleni maana mwalimu mkuu anafahamu kuwa elimu haiendani na mapenzi ya mapema kabla ya kumaliza masomo.

Katika hadithi, “Ajuta Majuto ya Mjukuu” (Somba, 1970) wahusika wasaidizi ni; Wazazi wa Kamene na Wayua, Kitonga na Kyalo. Dhamira ya athari ya ndoa ya mapema miongoni mwa wasichana wadogo inajitokeza kupitia kwa wahusika hawa. Kyalo anafanikiwa kumwoa Wayua ilhali Kitonga anajituma kutoa posa kwa wazazi wa Kamene lakini ndoa hiyo inatibuka kutokana na mauti yanayosababishwa na Kamene anapowatilia sumu kwa pombe wakati wa sherehe ya kutoa posa. Kitonga, babake Kamene na Kamene mwenyewe wanaaga dunia.

Wahusika John na Ben ni wahusika wasaidizi katika hadithi, “Maisha Yalimwendea Kombo” (Isaakwisa, 1970). Wanamsawiri Ruth kama mhusika mkuu kwa kuonyesha athari za anasa za ulevi miongoni mwa vijana. John anaelezwa kama kiwakilishi cha namna wanaume huwachukulia wasichana kama vyombo vya kujistarehesha na hivyo anajenga maudhui ya nafasi ya

mwanamke katika jamii. Ben anasawiriwa kuonyesha athari ambayo huwakumba wanawake wanapokosa kuthamini mapenzi kutoka kwa wanaume wanaowapenda bila unafiki. Ruth anapokosa kuthamini penzi la Ben, Ben anaamua kuwachana na Ruth.

Katika hadithi, “Mzee Khamis, Leo Wapi?” (Mohamed, 1971) watoto, Bin Barak, mpishi katika maulidi ya Bin Barak, Mazengo na Pusi ni wahusika wasaidizi ambao wanajengwa ili kufanikisha maudhui ya tamaa na ulafi ambayo yanabainika kupitia kwa Mzee Khamis ambaye hakosekani katika sherehe yoyote ile hata akikosa mwaliko.

Vilevile; Mzee Miraji, Bi. Asha na walimu wa Kombo katika shule ya msingi ni wahusika wasaidizi katika hadithi, “Malipo Duniani Hesabu Ahera” (Said, 1971). Wahusika hawa wanafanikisha dhamira ya athari za utukutu wa watoto wakati wa malezi. Wakati wa malezi ya Kombo kutoka kwa wazazi wake anasumbua sana na kukanywa mara kwa mara na wazazi wake ila hawachi utukutu. Aidha, anapokomaa na kuoa anapata mtoto kwa jina Miraji anayekuwa mtukutu hata kuliko alivyokuwa Kombo utotoni mwake.

Katika hadithi, “Sina Rafiki” (Wahab, 1977) Bi. Asha anajitokeza kama mhusika msaidizi. Bi. Asha anafanikisha dhamira ya hadithi ambayo ni athari ya wivu na tamaa kwa kumjenga mhusika mkuu Hasan anayetekeleza ukatili. Bi. Asha anamwambia Hasan kuwa alimuua Karama ambaye ni mumewe wa kwanza kabla hajaolewa na Hasan. Badala ya Hasan kuomba msamaha

anamfokea kuwa hana rafiki. Ukatili wa Hasan unabainika kwa mara nyingine anapompiga Bi. Asha anayeugua hadi kumuua.

Wazazi wa msimulizi wanajitokeza kama wahusika wasaidizi katika hadithi, “Mke Wangu” (Muhammed, 1977). Wanasaidia katika kujenga maudhui ya mgogoro katika asasi ya ndoa. Maudhui haya yanadhihirika kupitia kwa wahusika wakuu ambao ni msimulizi na Aziza. Wazazi wa msimulizi wanamchagulia msimulizi wanawake kadhaa kama vile; Fedhele Salim na Salma Fadhil ambao msimulizi anawakataa. Mwisho wanamchagulia Aziza lakini ndoa inakuwa na mgogoro kwa sababu mtazamo wa msimulizi kuhusu maisha ni wa kisasa. Msimulizi anathamini kuajiriwa kwa sababu amesoma ilhali mtazamo wa Aziza ni wa jadi kama vile; mtu anaweza kufanya kazi ya kujiajiri kama kuchoma mihogo.

Wahusika au mhusika mkuu hujengwa na wahusika au mhusika msaidizi. Wahusika wasaidizi wamebainika katika kila hadithi fupi teule ili kuwajenga wahusika au mhusika mkuu. Umuhimu wa wahusika wasaidizi ni kusaidia wahusika wakuu kuwasilisha dhamira na maudhui mbalimbali yaliyofanya hadithi hizi kufikia ubora wa kuwasilishwa katika idhaa ya redio ya BBC.

3.2.3 Wahusika Wadogo katika Hadithi Fupi Teule

Kwa mujibu wa Msokile (1993), wahusika wadogo hutumika katika kujenga dhamira kuu au mandhari ya hadithi na wakitolewa katika hadithi hawaathiri ploti ya hadithi. Wahusika wadogo husawiriwa kwa kuhusishwa na tukio

fulani lisilo na umuhimu mkubwa katika hadithi kama vile mhusika kutajwa amemuuzia mhusika fulani bidhaa au amemwambia jambo fulani. Wahusika wadogo wanajitokeza kama ifuatavyo kwenye hadithi fupi teule:

Mhusika Saida ni mhusika mdogo katika hadithi, “Siku ya Arobaini” (Mohamed, 1970) kwa sababu anatajwa tu kama binti ambaye Sadiki anampata dirishani siku zote aendapo kazini.

Katika hadithi, “Kusoma na Kupenda” (Salim, 1970), mwalimu wa Jografia anabainika kama mhusika mdogo maana hata akitolewa katika hadithi haathiri ploti ya hadithi. Ameelezwa ili kusisitiza dhamira kuu ya hadithi ambayo ni kuendeleza elimu.

Wageni wanaoandamana na Kitonga anapokwenda kupeleka posa kwa wazazi wa Kamene ni wahusika wadogo katika hadithi, “Ajuta Majuto ya Mjukuu” (Somba, 1970). Wageni ni wahusika wadogo kutokana na dhima yao ya kuonyesha baadhi ya mila na desturi katika jamii ya Waafrika. Utamaduni unaoonekana katika mchakato wa ndoa unaohusishwa na utoaji wa posa ambapo anayetoa posa huandamana na walio karibu naye kama vile marafiki na wanafamilia.

Katika hadithi, “Maisha Yalimwendea Kombo” (Isaakwisa, 1970) Seth ni mfano wa mhusika mdogo kwa sababu mchango wake katika hadithi ni kumwelekeza Ben katika nyumba ya Ruth kwa kuwa Ben ni mgeni na hatambui anapoishi Ruth.

Babu mmoja mkongwe katika hadithi, “Mzee Khamis, Leo Wapi?” (Mohamed, 1971) anajitokeza kama mhusika mdogo. Mhusika huyu akitolewa katika hadithi hawezi kuathiri dhamira kuu na ploti ya hadithi. Umuhimu wake ni kuwa yeye ndiye anamwokoa Mzee Khamis na ngarawa yake anapozama baharini.

Katika hadithi, “Malipo Duniani Hesabu Ahera” (Said, 1971) Fatuma, watoto wa mtaani na mkewe Kombo ni wahusika wadogo. Maelezo machache ndiyo yanatolewa kuwahusu na kuondolewa kwao katika hadithi hakuwezi kuathiri lengo la hadithi. Fatuma anaelezwa kama dada ya Kombo na mpole anayependwa na kila mtu. Watoto wa mtaani wanaelezwa ili kuonyesha mojawapo ya nafasi ya watoto katika jamii ambayo ni kucheza maana wanachora ukuta wa nyumba ya Mzee Miraji hata akiupaka rangi. Mkewe Kombo naye anasisitiza dhamira ya elimu maana tunaelezwa wanapatana na Kombo ughaibuni anakosomea udaktari.

Mhusika askari anayekwenda kumwambia Hasan anatakikana stesheni ni mhusika mdogo katika hadithi, “Sina Rafiki” (Wahab, 1977). Dhima yake kuu ni kutoa habari za kutakikana kwa Hasan na hivyo basi hata akitolewa katika hadithi haathiri ploti.

Katika hadithi, “Mke Wangu” (Muhammed, 1977) kijana mwanamume anabainika kama mhusika mdogo kwa sababu ametajwa tu kwamba alikuwa katikati mwa Fedhele Salim na shoga yake Fedhele. Hajapambanuliwa kwa undani na hivyo basi hana athari katika ploti ya hadithi.

Tathmini ya wahusika wadogo inaonyesha kuwa hawana umuhimu mkubwa katika hadithi fupi teule. Baadhi ya hadithi zina mhusika mdogo mmoja na bado zimeibuka kuwa bora kutokana na kuwasilishwa hewani katika idhaa ya redio ya BBC. Kando na hivyo; hadithi, “Mke Wangu” ina mhusika mdogo mmoja na imechapishwa tena baada ya miaka thelathini katika mkusanyiko wa *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (2007).

3.2.4 Wahusika Bapa katika Hadithi Fupi Teule

Wahusika bapa ni wahusika ambao hawabadiliki kitabia na hawakui katika mazingira ya aina yoyote ile (Msokile, 1993). Wahusika bapa hubuniwa kwa kuzingatia na kutenda matendo yanayoingiliana na sifa walizopewa na hawabadiliki hata wakati mazingira au mahusiano yanapobadilika (Njogu na Chimerah, 1999). Kwa mujibu wa Wamitila (2008), wahusika bapa hawabadiliki kutoka mwanzo hadi mwisho wa hadithi na nia yao huwa ni

ujenzi wa tukio moja tu, jambo linalowafanya kukosa sifa halisi za binadamu. Wahusika bapa ni wa aina mbili; wahusika bapa sugu ambao msimamo wao hudhihirika kupitia kwa masimulizi au maelezo ya msanii. Wahusika bapa vielelezo ambao pia hawabadiliki kitabia lakini hupewa majina ya kimajazi au lakabu ili kuonyesha sifa zao. Wahusika hawa wanajitokeza kama ifuatavyo kwenye hadithi fupi teule:

Mhusika Sadiki katika hadithi ya "Siku ya Arobaini" (Mohamed, 1970) ni mhusika bapa kielelezo kwa sababu amepewa jina la mjazi. Sadiki ni jina lenye maana ya kukubali. Jina lake linaingiliana na tabia yake ambayo haibadiliki ya kukubali mwanamke yeyote ambaye anaona kuwa anampenda licha ya kuwa na Bahati, mkewe halisi.

Katika hadithi, "Kusoma na Kupenda" (Salim, 1970) mwalimu mkuu ni mhusika bapa kielelezo maana anashikilia msimamao wake wa kuwa mkali hasa kwa kunyoosha maadili ya wanafunzi hadi wanampa lakabu *'Hitler'*. Rama ni mhusika bapa sugu kwa sababu kwanzia mwanzo wa hadithi habadilishi tabia yake ya kushitaki kwa mwalimu mkuu maovu yoyote anayoyaona kutoka kwa wanafunzi ili kumsaidia mwalimu mkuu katika kuimarisha maadili.

Mhusika Kioko katika hadithi, "Ajuta Majuto ya Mjukuu" (Somba, 1970) ni mhusika bapa sugu kwa sababu anashikilia msimamo kwamba Kamene ni mpumbavu kwa kusababisha mauti ya babake, Kitonga, wanaoandamana na

Kitonga na hata Kamene mwenyewe. Kioko anashindwa kuelewa changamoto za kisaikolojia ambazo mdhulumiwa wa ndoa ya lazima hupitia kama vile Kamene anayetaka kuozwa kwa Kitonga akiwa na miaka kumi na mitano.

Katika hadithi ya "Maisha Yalimwendea Kombo" (Isaakwisa, 1970), Joyce ni mhusika bapa sugu kwa sababu tabia yake inadhihirisha heshima na utu. Ben anapokuja kumtembelea Ruth na kumpata hayuko, Joyce anampa chakula na kumwonyesha mahali pa kulala.

Naye Mazengo ni mhusika bapa sugu katika hadithi, "Mzee Khamis, Leo wapi?" (Mohamed, 1971) kwa sababu inabainika kuwa habadilishi tabia yake ya kupenda kumtania Mzee Khamis. Mazengo anamtania Mzee Khamis kuwa atampokonya sinia ya chakula anapokula jambo ambalo linamkera Mzee Khamis maana anapenda kula kupita kiasi.

Katika hadithi ya "Malipo Duniani Hesabu Ahera" (Said, 1971), rafiki zake kombo wa mtaani wanadhihirika kama wahusika bapa sugu kwa sababu ni desturi yao kwenda kulenga njiwa wa watu kwa mawe.

Inspekta wa askari na mtu anayevaa kama raia katika hadithi, "Sina Rafiki" (Wahab, 1977) ni wahusika bapa sugu kwa sababu tabia yao ya kumdadisi Hasan haibadiliki hadi mwishoni wanabaini kuwa Hasan ndiye alimuua Karama na mkewe Bi. Asha kama inavyotangazwa redioni kupitia idara ya mahakama.

Katika hadithi ya “Mke Wangu” (Muhammed, 1977), Mapanya ni mhusika bapa sugu kwa sababu msimulizi anaeleza kuwa tabia ya Mapanya ilikuwa ni kuwaletea chakula kikiiva pamoja na kuja anachukua nguo na kwenda kuwafulia

Desturi ya wahusika bapa sugu na wahusika bapa kielelezo kutobadilika katika tabia zao inasaidia hadithi fupi teule kufanikisha maudhui na dhamira yake. Ufanisi huu unatokana na wahusika kuwa na msimamo dhabiti katika itikadi zao na hivyo basi kukuza dhamira na maudhui kusudiwa katika hadithi.

3.2.5 Wahusika Mviringo au Duara katika Hadithi Fupi Teule

Forster (1927) anaeleza kuwa wahusika mviringo ni wale ambao hukosa uthabiti kwa sababu hubadilika kitabia katika hadithi na mabadiliko hayo huchangiwa na mabadiliko ya maudhui na mazingira. Wahusika mviringo huonyesha uhalisia wa maisha katika kazi ya fasihi (Msokile, 1993). Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999), wahusika mviringo pia huitwa wahusika duara na wana tabia ya kubadilika kitabia, kimawazo au kisaikolojia. Wahusika hawa wanajitokeza kama ifuatavyo katika hadithi fupi teule:

Katika hadithi, “Siku ya Arobaini” (Mohamed, 1970) Bahati anabainika kama mhusika mviringo. Anapoambiwa na rafiki zake kuwa mumewe Sadiki ni mkware, anajifanya kimada na anafanikiwa kubaini ukweli kuwa Sadiki ni mzinzi maana mumewe anakubali kukutana na kimada anayemwandikia barua

asijue ni Bahati. Sadiki anajifanya mjanja na kuficha barua lakini anapokutana na kimada aliyeandika barua anastaajabu kugundua ni mke wake Bahati.

Wahusika Abdu na Zubeda ni wahusika duara katika hadithi ya "Kusoma na Kupenda" (Salim, 1970). Mwanzoni wanajituma katika elimu lakini mapenzi yanapowazidi wanaanza hata kupeana busu shuleni na kuonekana na Rama jambo ambalo ni kinyume na maadili ya shuleni.

Katika hadithi, "Ajuta Majuto ya Mjukuu" (Somba, 1970) Kamene anajitokeza kama mhusika duara kwa sababu anapotumwa na babake awaletee pombe ananyenyekea na kwenda ila anaitia sumu. Babake, Kitonga na wageni wanaoandamana na Kitonga wanapokunywa pombe hiyo wanaaga dunia. Kamene anatia sumu katika pombe maana hajaridhia kuozwa mapema kisha kwa mzee ambaye hampendi maana ana mpenzi wake kwa jina Kioko. Aidha, Kamene anapokua akitoroka baada ya kutekeleza mauti anapata ajali pia na kuaga dunia.

Ruth ni mhusika mviringo katika hadithi, "Maisha Yalimwendea Kombo" (Isaakwisa, 1970). Mwanzoni ni mnyenyekevu lakini anapokua na kujiona ana elimu na madaraka anaamua aondoke kijijini na anahamia mjini ili afanye starehe za densi na pombe. Uraibu huu unasababisha kifo chake kutokana na ajali anayopata akitoka baa huku akiendeshwa na mwanamume mlevi anayepatana naye kwenye baa.

Katika hadithi ya “Mzee Khamis, Leo wapi?” (Mohamed, 1971) Pusi ambalo ni jina la paka wa Mzee Khamis anajitokeza kama mhusika duara. Mzee Khamis anajeruhiwa anapomfungia na kumwadhibu Pusi kwa bakora kutokana na kula mnofu wake wa nyama. Pusi anasahau ukaribu wake na Mzee Khamis na kumrarua kwa makucha hadi kumtoa damu kama njia ya kujitetea anaponusurika kupigwa na bakora na Mzee Khamis.

Mhusika Kombo ni mhusika duara katika hadithi, “Malipo Duniani Hesabu Ahera” (Said, 1971). Kombo, wakati wa malezi yake hususan utotoni ni mtukutu nyumbani na hata shuleni lakini wakati unafika na anabadilika na kufanya bidii katika masomo hadi anafadhiliwa kwenda kusomea udaktari Uingereza.

Katika hadithi, “Sina Rafiki” (Wahab, 1977) Hasan anaelezwa kama mhusika duara kutokana na hali ambapo mwanzoni anakuwa rafiki wa kutegemewa na Karama lakini wivu unamfanya kubadilika hadi anamuua Karama pamoja na mke wake Bi. Asha kusudi arithi mali yao.

Mhusika Aziza katika hadithi ya “Mke Wangu” (Muhammed, 1977) ni mhusika mviringo kwa sababu mwanzoni anakubali kuolewa na msimulizi lakini anapoingia katika ndoa hiyo anamwambia msimulizi heri ampe talaka. Aziza anaona heri apate talaka maana msimulizi anategemea wapewe chakula na wazazi wao wakati anasubiri ajira ilhali Aziza anatarajia msimulizi

anaweza kujiajiri kwa kuchoma mihogo. Aziza anamwambia msimulizi si mume kifu yake maana hafanyi kazi.

Wahusika hawa wanaonyesha uhalisia katika maisha ya binadamu kwa sababu mara nyingi mwanadamu huenda akabadilisha tabia kulingana na mabadiliko ya mazingira. Umuhimu wa wahusika hawa ni kuipatia hadithi fupi teule uhalisia na kuifanya iwe bora hadi kusomwa hewani katika idhaa ya redio ya BBC.

3.2.6 Wahusika Foili katika Hadithi Fupi Teule

Kwa mujibu wa Msokile (1992), wahusika foili huwakilisha uhalisia ulioko katika mwanadamu na hutegemea wahusika mviringo na bapa ili kudhihirisha sifa zao. Wahusika hawa huwa katikati ya wahusika bapa na wahusika mviringo au duara. Wahusika foili huwa na jukumu la kuwaonyesha wahusika wakuu na kuwafanya waonekane sana (Msokile, 1993). Kwa mujibu wa McKinney (2005), wahusika foili hufanikisha kueleweka kwa sifa za wahusika wengine hasa unapochunguza sababu ya wanayosema au wanayotenda. Wahusika hawa wanadhihirika kama ifuatavyo katika hadithi fupi teule:

Shoga zake Bahati katika hadithi, “Siku ya Arobaini” (Mohamed, 1970) wanajitokeza kama wahusika foili kutokana na habari wanayompa Bahati ya ukware wa Sadiki. Habari hii inawafanya wahusika Bahati na Sadiki kuonekana kwenye maisha ya ndoa inayokumbwa na mgogoro wa ukosefu wa uaminifu.

Katika hadithi ya “Kusoma na Kupenda” (Salim, 1970) Karani wa mwalimu mkuu anajitokeza kama mhusika foili kwa sababu anapotumwa na mwalimu mkuu anawajibika na kwenda. Anawaita Zubeda na Abdu wanaotakikana ofisini mwa mwalimu mkuu. Karani anamfanya mwalimu mkuu kujitokeza bayana kama anayethamini elimu pamoja na maadili.

Mhusika Kitonga ni mhusika foili katika hadithi, “Ajuta Majuto ya Mjukuu” (Somba, 1970) kwa sababu msukumo wake wa kutaka kumuoa Kamene mwenye umri wa miaka kumi na mitano unamkuza Kamene ambaye ni mhusika mkuu. Msukumo huo wa ndoa unamkuza Kamene kwa kujenga maudhui ya nafasi ya mwanamke katika jamii anayechukuliwa kama chombo cha starehe na mwanamume.

Katika hadithi ya “Maisha Yalimwendea Kombo” (Isaakwisa, 1970) John anabainika kama mhusika foili kutokana na matukio mengi kuonyesha kuwa anaandamana na Ruth katika starehe ya pombe na densi. Kupitia kwa John, Ruth anakuzwa kama mhusika mkuu ambaye ameathirika na anasa za pombe na densi.

Watoto ni wahusika foili katika hadithi, “ Mzee Khamis, Leo wapi?” (Mohame, 1971). Wakati mwingi wanapomwona Mzee Khamis wanamchokoza ‘Mzee Khamis, Leo wapi?’ na hivyo kumdhihirisha Mzee Khamis kama mhusika mkuu anayetawaliwa na ulafi na tamaa.

Katika hadithi ya “Malipo Duniani Hesabu Ahera” (Said, 1971), mtoto wa Kombo kwa jina Miraji anaibuka kama mhusika foili. Miraji anakuwa mtukutu kupindukia jambo linaloibua tetesi kuwa huenda Kombo analipwa duniani kwa sababu alipokuwa anakua alimsumbua marehemu babake Mzee Miraji, maana Kombo alikuwa mtukutu.

Bwana Musa anajitokeza kama mhusika foili katika hadithi, “Sina Rafiki” (Wahab, 1977). Bwana Musa anapogundua Bi. Asha ameaga, anaamua kwenda kwa idara ya afya na uchunguzi unasaidia askari katika kubaini kuwa Hasan ni katili anayehusika katika kifo cha Bi. Asha na hapo awali kifo cha mumewe Karama.

Katika hadithi ya “Mke wangu” (Muhammed, 1977) muuza madafu anabainika kama mhusika foili kutokana na Aziza kumtumia kama kielelezo cha mume bora na kumwambia msimulizi anatamani mume kama muuza madafu maana anawajibika na kufanya kazi. Muuza madafu anajengwa kama mhusika mwenye bidii na kazi, sifa ambayo ni muhimu katika asasi ya ndoa ili kuzuia mgogoro katika ndoa.

Wahusika foili wanasaidia katika hadithi fupi kwa sababu ni kioo cha wahusika wakuu. Wanasaidia katika kueleza baadhi ya sifa za wahusika au mhusika mkuu na hivyo basi dhamira na maudhui ya hadithi fupi teule kujitokeza kwa uwazi (Poe, 1938).

3.3 Idadi ya Wahusika na Jukumu la Wahusika katika Hadithi Fupi Teule

Kwa mujibu wa Mbatiah (2000), wahusika katika hadithi fupi wanastahili kuwa wachache na kwa kawaida hawakuzwi kwa mapana kama inavyobainika katika riwaya. Wahusika wanastahili kukuzwa katika kipindi fulani tu; hasa cha mvutano au mgogoro ambao ni baina yao na wengine au mvutano wa mhusika mwenyewe (Wamitila, 2003). Ingawa wahusika wa hadithi fupi hawafai kukuzwa sana kiwakati, inafaa wakuzwe kikamilifu kwa kueleza majukumu yao kwa ukamilifu. Wamitila (2002) anaeleza kuwa jukumu la mhusika katika hadithi ni mambo ambayo mhusika anatenda au anatendewa ili kujenga dhamira na maudhui ya hadithi. Mwandishi anastahili kuweka jukumu hili waziwazi maana ana nafasi ndogo ya kujieleza. Jukumu la mhusika linapojitokeza vyema husaidia matukio ya hadithi fupi kukumbukwa na msomaji au msikilizaji hata kama jina la mhusika litamtoka fikirani. Idadi ya wahusika na majukumu yao inabainika kama ifuatavyo katika hadithi fupi teule:

3.3.1 Idadi ya Wahusika na Jukumu lao katika Hadithi, “Siku ya Arobaini” (Mohamed, 1970)

Wahusika wanastahili kuwa wachache na jukumu lao liwe wazi ili kujenga dhamira na maudhui ya hadithi (Iribemwangi, 2007). Hadithi hii ina wahusika watano ambao ni: Sadiki, Bahati, Saida, shoga zake Bahati na dereva wa gari. Kila mhusika wa hadithi hii amesawiriwa na jukumu lake na hivyo basi kuchangia katika ujenzi wa dhamira ya hadithi kwa namna ifuatavyo:

Kwanza, Sadiki ni mhusika mkuu. Sadiki anasawiriwa kama mume ambaye hathamini maisha ya ndoa maana bado ana tamaa ya wanawake wengine licha ya kuwa na mke wake halali wa ndoa. Sadiki anajenga dhamira ya athari ya ukosefu wa uaminifu kutokana na tamaa ya jicho la nje katika maisha ya ndoa kama inavyodhihirika:

> ...Sadiki alikuwa ni kijana anayependa sana wanawake... alikuwa na njaa isiyo na mipaka, na ijapokuwa alikuwa na mke, hakutosheka... (uk. 25).

Pili, Bahati pia anasawiriwa kama mhusika mkuu. Bahati ni mkewe Sadiki ambaye anasawiriwa kama mke anayetekeleza majukumu yake katika maisha ya ndoa ipasavyo. Jukumu lake ni kusisitiza uaminifu na uwajibikaji wa mwanamke kwenye maisha ya ndoa:

> ...alikuwa kashughulika akaingia jikoni na kutoka huku anaitandika meza ya kulia kwa vinono vya kutoa mate.. (uk. 23).

Tatu, Saida ni mhusika mdogo. Saida ni jirani ya Sadiki na ni kiwakilishi cha baadhi ya wanawake ambao Sadiki huwamezea mate. Ametumiwa na mwandishi kuonyesha nafasi ya mwanamke katika jamii. Mwanamke anachukuliwa kama kivutio cha mwanamume na chombo cha kumstarehesha mwanamume:

> ...Saida yule kisura anayemkuta dirishani siku zote aendapo kazini. Na ikiwa ndiye basi Sadiki aliona kaokota hazina ya uzuri... (uk. 23).

Nne, Shoga zake Bahati ni wahusika wasaidizi. Wanapewa jukumu la kumdokezea Bahati mwenendo wa tabia za mumewe ambaye ni mkware. Wanapozidi kumweleza Bahati tabia za mumewe, Bahati anachukua hatua ya

kumpeleleza ndiposa anamwandikia barua kwa siri kujifanya ni mwanamke mwengine tofauti. Shoga zake Bahati wanamsaidia Bahati kupata ukweli wa tabia ya Sadiki kuwa ni mkware na mzinzi:

> ...Sadiki alinaswa mtegoni, kwani ile barua aliyokuwa ameletewa ilikuwa imetoka kwa mkewe mwenyewe, Bahati... (uk. 27).

Tano, dereva wa gari ni mhusika mdogo. Amesawiriwa ili kusuluhisha kilele cha hadithi ambacho ni uchunguzi wa Bahati kuhusu uzinzi wa mumewe. Dereva anamulika kwa taa kali uso wa bibi aliyekuwa na Sadiki na hapo ndipo Sadiki anastaajabu kuona ni Bahati. Hata hivyo, hapo awali Sadiki alikuwa ameshuku harufu ya mkewe maana anaijua vilivyo:

> ...bibi aliyejifunika buibui gubigubi...Sadiki akaanza kutembea juu ya kifua cha habibi, shingoni, nyweleni, usoni lakini lo! Pua yake ilinusa harufu ya mwili ambayo aliijua vilivyo...ghafla anga la taa za gari iliyopita njiani ilimeta juu ya uso wa yule bibi na aliduwaa kuuona uso wa mkewe... (uk. 27).

Ubora wa hadithi hutegemea idadi ndogo ya wahusika ambao hupewa majukumu maalumu ili kutumia muda mfupi (kikao kimoja) kuwasilisha maudhui (Poe, 1938). Kwa mujibu wa Bramah (2016), wahusika watano wanatosha katika uandishi wa hadithi fupi. Hadithi hii inatumia idadi ya wahusika watano kama anavyopendekeza Bramah katika kufanikisha maudhui na dhamira ya hadithi fupi. Hata hivyo, wahusika wakuu na wasaidizi ndio wamepewa nafasi kubwa katika kujenga lengo la hadithi fupi teule.

3.3.2 Idadi ya Wahusika na Jukumu lao katika Hadithi, “Kusoma na Kupenda” (Salim, 1970)

May (2002) anaeleza kuwa alivutiwa na hadithi fupi za Poe kutokana na namna anavyotumia idadi ndogo ya wahusika kueleza matukio muhimu katika hadithi fupi. Hadithi hii ina wahusika tisa ambao ni: Abdu, Zubeda, Rama, mwalimu mkuu, mwanafunzi anayekemewa na mwalimu mkuu, wanafunzi katika darasa la Abu na Zubeda, mwalimu wa Jografia, karani wa mwalimu mkuu na wazazi wa Abdu. Dhamira na maudhui ya hadithi imeendelezwa kupitia kwa jukumu la kila mhusika kama ifuatavyo:

Wahusika Abdu na Zubeda ni wahusika wakuu. Wanafunzi ambao kando na masomo, wanashindwa kustahamili hisia za mapenzi kiasi cha kwamba wanakuwa wanafunzi wapenzi hadi kupeana busu shuleni kwa kujificha katika mojawapo ya darasa ambalo halina wanafunzi. Jukumu lao ni kuonyesha athari za uhusiano wa kimapenzi ya mapema miongoni mwa vijana kabla ya kumaliza masomo:

> ...Abdu alimvuta tena Zubeda na kumbusu kwa haraka kwenye shavu lake laini kisha akamwacha... (uk. 40).

Mhusika Rama ni mhusika msaidizi. Yeye ni mlinzi wa shule mwenye jukumu la kuhakikisha kuwa kila kitu shuleni kipo sawa ikiwemo mienendo ya wanafunzi. Rama anakuza dhamira ya kuwajibika katika kazi yoyote ile mtu anahusishwa nayo:

> ...walipogunduliwa na Rama, mwangalizi wa shule ilikuwa ni mara ya tatu. Hapakuwa na shaka kuwa Rama atawachongea tu... (uk. 44).

Mwalimu mkuu ni mhusika bapa kielelezo. Anahakikisha kuwa nidhamu na elimu inaendelea kwa njia bora katika shule. Anawajibika katika kuhakikisha mazingira ya shule ni bora kwa wafanyakazi, walimu na wanafunzi. Maudhui ya elimu na maadili yanaendelezwa kupitia kwa majukumu ya mwalimu mkuu:

> ...wanafunzi walimbandika jina wakamwita *Hitler*. Miongoni mwa mambo ambayo *Hitler* hakuyapenda katika shule yake ilikuwa ni mapenzi. Nayo akiyaita 'uchafu'. Alikuwa hapendi 'uchafu' baina ya wanafunzi wa kike na wa kiume... (uk. 40).

Mwanafunzi anayekemewa na mwalimu mkuu ni mhusika mdogo. Jukumu lake ni kuonyesha athari ambayo huwakumba wanafunzi wanaovunja kanuni za shule. Maudhui ya maadili yanasisitizwa kutokana na adhabu anayopata kwa kuvunja kanuni za shule:

> ...Zubeda alisimama na kutega sikio na mara alitambua sauti ya mwalimu mkubwa aliyekuwa akimkemea mwanafunzi. Mara Zubeda alisikia bakora zimewaka moto zikifuatiwa na usiahi mkubwa wa maumivu... (uk. 40).

Jukumu la mwalimu wa Jografia kama mhusika mdogo linabainika kama mwalimu ambaye anawajibika katika kazi yake ya ufunzaji. Mwalimu huyu ni kielelezo cha walimu bora ambao wanaendeleza elimu. Karani anapofika anampata darasani akifunza:

> ...mwalimu wa Jografia alipokuwa kashughulika na kusomesha ramani ya Afrika iliyotundikwa mbele ya wanafunzi alikatizwa na karani wa mwalimu mkubwa... (uk. 43).

Wanafunzi katika darasa la Abdu na Zubeda ni wahusika wasaidizi. Wanajenga taswira ya namna ambavyo wanafunzi huchangia katika kueneza habari yoyote shuleni. Uvumi wa mapenzi ya Zubeda na Abdu unaendelezwa

na wanafunzi hawa. Jukumu la wanafunzi hawa la kueneza uvumi linakuza dhamira ya kukashifu tabia zilizo kinyume na maadili ya jamii:

> ...wenye vijicho walianza kutapakaza uvumi. Walimu nao waliingiwa na wasiwasi na kuanza kupeleleza. Hawakuchukua muda kuyaona yote, kwani yalikuwa wazi... (uk. 42).

Naye karani wa mwalimu mkuu ni mhusika foili. Jukumu la karani ni kuwajibika kwa kazi yake. Anatumwa na mwalimu mkuu zaidi ya mara moja. Anawajibika na kupeleka habari kuhusu kuhitajika kwa Abdu na Zubeda ofisini mwa mwalimu mkuu. Jukumu analolifanya la kutumwa na kuenda linakuza maudhui ya kuwajibika:

> ...mlango wa darasa la nane uligongwa tena na karani wa mwalimu mkubwa. Zubeda alipomwona roho ilimpasuka na alijua kuwa saa imekwisha fika... (uk. 44).

Wazazi wa Abdu ni wahusika wadogo. Wanasawiriwa ili kuipa hadithi taharuki. Wanachukua hatua ya kurudi Mombasa pamoja na Abdu ambaye anawacha shule na maelezo hayapo kama huko Mombasa anakoenda ataendelea na masomo.

> ...Abdu alimwomba Zubeda amfikishie barua yake ya kuacha shule pamoja na vitabu kwa mwalimu mkubwa kwani yeye alikuwa anarejea kwao Mombasa pamoja na wazee wake na kwa hivyo hapakuwa na haja tena ya kumpeleka mzee wake... (uk. 44).

Kwa mujibu wa Omar (2010), wahusika wanastahili kuwa wachache na usawiri wao udhihirishe mbinu ya taharuki ili kusanii kazi yenye mvuto kwa hadhira. Hadithi hii inatumia wahusika wachache ambao majukumu yao yameelezwa (Poe, 1846). Mbinu ya taharuki inabainika kupitia kwa Wazazi wa Abdu kwa sababu hatujui kama huko Mombasa Abdu anaenda kusoma

ama kufanya nini? Tathmini hii inaonyesha mojawapo ya sifa za ubora wa hadithi fupi unaoifanya kusomwa hewani katika idhaa ya redio ya BBC.

3.3.3 Idadi ya Wahusika na Jukumu lao katika Hadithi, "Ajuta Majuto ya Mjukuu" (Somba, 1970)

Kwa mujibu wa Pelayo (2001), idadi ya wahusika katika hadithi fupi inastahili kuwa ndogo. Jukumu lao linastahili kuelezwa kwa kuzingatia muda kidogo lakini kwa ukamilifu. Katika hadithi hii, idadi ya wahusika ni wanane: Wayua, Kamene, wazazi wa Kamene na Wayua, Kyalo, Kitonga, wageni walioandamana na Kitonga na Kioko. Wahusika hawa wanakuzwa kwa majukumu mbalimbali ili kujenga dhamira na maudhui ya hadithi kama inavyobainika:

Mhusika mkuu Wayua ni kiwakilishi cha wasichana ambao wanaozwa mapema bila hata hiari yao. Anaozwa kwa mzee Kyalo kama mke wa nne. Jukumu la Wayua kutokana na kuozwa mapema ni kuonyesha athari ya utamaduni unaomdunisha mwanamke:

> ...alikuwa mkewe Kyalo wa nne...mwili ulikuwa umenyong'onyea... (uk. 6).

Mhusika mkuu Kamene ni dadake Wayua mdogo ambaye licha ya kuwa na umri mdogo anashuhudia dadake akiozwa mapema na kwa lazima. Aidha, anapokua anapangiwa ndoa ya lazima baina yake na Kitonga. Hatima yake ni kuwa ndoa hii inasababisha mauti ya babake, Kitonga, walioandamana na Kitonga na yeye mwenyewe anaaga dunia. Kamene anafanikisha dhamira ya

athari ya ndoa za lazima na mapema miongoni mwa wasichana katika jamii inayoongozwa na utamaduni uliopitwa na wakati:

> ...Alikuwa na umri wa miaka tisa tu wakati aliposhuhudia kuchukuliwa kwa dada yake Wayua. Alifikiri ni mchezo lakini kumbe alichukuliwa mbali kupita kiasi na kuonana kutakuwa wakijaliwa...(uk. 6)... ya nini Kamene kwenda kumwua baba yake na yule mchumba wake, laiti angalikataa katu katu asingalilazimishwa... (uk. 11).

Mhusika msaidizi Kyalo ni kiwakilishi cha wazee ambao bado wanaongozwa na utamaduni ambao umepitwa na wakati. Kyalo anakuza maudhui ya utamaduni unaowadhulumu wanawake na kuwachukulia wanawake kama vyombo vya kujistarehesha tu:

> ...Kyalo lilikuwa jitu chafu mno na Kamene alishindwa kabisa kuelewa kwa nini dada yake Wayua alikubali kuolewa naye. (uk. 6).

Mhusika msaidizi Kitonga amepewa nafasi ya mwanamume ambaye anatumia mali ili kujinufaisha kwa kuwachukulia wanawake kama vyombo vya starehe tu. Hajali umri mdogo wa wanawake anaooa, mradi tu ameridhiwa na wazazi wa binti basi yeye anakuwa tayari kutoa pesa na kuoa:

> ...Katika karne hizo, faida ya wake ilikuwa kuwazalia waume wao watoto na kulima mashamba tu...kwa nini mtu kwanza kuozwa mume asiyempenda na halafu kufanywa mtumwa? Alipokuwa akiwaza hivi mara akakumbuka maneno aliyoambiwa na mama yake siku moja, mwanangu Kamene, Kitonga ni mtu anayeheshimiwa sana. Ana mali na wake wengi... (uk.8).

Babake Wayua na Kamene ni mhusika msaidizi. Mzee huyu anayeendeleza utamaduni uliopitwa na wakati pamoja na malezi ya kidikteta ambayo hayampi mtoto nafasi ya kufanya uamuzi muhimu wa maisha yake hasa suala la ndoa:

> ...magharibi ilipoingia, Kamene aliitwa mle chumbani walimokuwa wale wageni na akajulishwa kwa mtu mmoja ambaye ndiye aliyetakikana awe mchumba wake.Alikuwa mfupi, wa makamo kidogo...alikuwa na wake wawili na Kamene alikuwa awe wa tatu... (uk. 9).

Mhusika msaidizi mamake Wayua na Kamene ni kiwakilishi cha wanawake ambao wanazidi kuikandamiza jinsia ya kike kutokana na utamaduni uliopitwa na wakati. Tamaa ya mali inampelekea kukubali kuwaoza binti zake kwa wanaume waliowazidi umri kwa mbali. Anakuza dhamira ya athari ya tamaa na utamaduni uliopitwa na wakati miongoni mwa wanajamii:

> Wee mwanangu una bahati sana, una baba mwenye hekima, anayejiweza na pia anayekutafutia mtu mwenye nafasi akuoe... (uk. 9).

Wageni wanaoandamana na Kitonga ni wahusika wadogo. Wao ni kiwakilishi cha wanajamii wasiopenda mabadiliko. Wanajamii ambao wanamdhalilisha mwanamke na kumchukulia kama kiumbe dhaifu:

> ...kwa unyonge na udhaifu Kamene akaamkiana na yule bwana...baada ya kuamkiana naye, baba yake akamwamuru kutoka nje na kwenda kuwaletea wageni pombe ili wajiburudishe kwa kuwa yule bwana alikuwa amekwisha mpenda Kamene na wale wageni wote waliokuwapo pale walitikisa vichwa vyao ili kuwa ishara ya maridhiko kwamba ndoa ifanywe kwa haraka...(uk. 9).

Kioko ni mhusika bapa sugu ambaye anaendeleza maudhui ya taasubi ya kiume, anamwelekezea Kamene lawama yote kwa mauaji anayosababisha . Kutokana na kauli yake, anachukulia kuwa mauti yote yanayomkumba babake Kamene, Kitonga, wanaoandamana na Kitonga na Kamene ni mauti yaliyosababishwa na Kamene. Anakosa kutathmini uchungu anaopitia Kamene wa kuozwa kwa mzee asiyempenda:

> ...ya nini Kamene kwenda kumwua baba yake na yule mchumba wake. Laiti angalikataa katu katu asingalilazimishwa. Msichana huyo hakika alikuwa mpumbavu! (uk. 11).

Hadithi fupi teule inatumia wahusika wanane katika kufanikisha dhamira na maudhui ya hadithi fupi. Wahusika wa hadithi fupi huwa wachache na hawapambanuliwi kwa upana kama wahusika wa riwaya (Njogu na Chimerah, 1999). Kuzingatia kigezo cha usawiri wa wahusika, hadithi hii inazingatia mojawapo ya kanuni za ubora wa hadithi fupi.

3.3.4 Idadi ya Wahusika na Jukumu lao katika Hadithi, "Maisha Yalimwendea Kombo" (Isaakwisa, 1970)

Sundararaj (2011) anaeleza kuwa hadithi fupi isiyozidi kurasa kumi na tano inastahili kutumia wahusika wachache na ikiwezekana mhusika mkuu mmoja au ikiwa kuna sababu maalumu wahusika wakuu wawili. Hadithi hii imesawiriwa kwa kurasa nane na mhusika mkuu mmoja. Aidha, wahusika wa hadithi ni kumi na wawili: Ruth, babake Ruth, wake kumi na wawili wa babake Ruth, wanachama wa Chama cha Maendeleo ya Wanawake, John, Seth, Ben, Joyce, Bwana Maina, dereva wa teksi, majirani wa Ruth huko Magomeni na jamaa anayesababisha ajali ya mauti. Kila mhusika ameelezwa na jukumu lake kuwasilishwa ili kujenga dhamira na maudhui ya hadithi kwa namna ifuatayo:

Ruth ni mhusika mkuu. Anawakilisha watu ambao hufanya maamuzi yasiyo na busara. Licha ya kuwa na elimu, hatima yake ni kuishi maisha ya kuhangaika. Anaona maisha ya kijijini hayana maana na kuhamia mjini ili

astarehe kwa ulevi atakavyo. Anafanikisha dhamira ya athari ya ukosefu wa hekima katika kufanya uamuzi wa maisha mema miongoni mwa vijana:

> ...akili nyingi huondoa maarifa, Ruth aliona maisha ya kukaa kijijini hayakumfaa maana alikuwa ni msichana mwenye elimu na madaraka ...akaamua kuhamia mjini na akaanza kujiingiza katika starehe kama za dansi na kuchapa mtindi... (uk. 37).

Baba yake Ruth ni mhusika mdogo. Yeye ni kiwakilishi cha mzee ambaye ameshikilia utamaduni mkongwe pamoja na mzee ambaye anawajibika katika kuhakikisha maisha ya wanafamilia wake yako sawa. Anakuza maudhui ya elimu kwa sababu anahakikisha Ruth anapata elimu:

> ...Binti huyo alizaliwa katika ukoo wa kifalme na wa kitajiri. Kwa hiyo, baba yake alikuwa na nafasi nzuri hata alioa wake kumi na wawili. Pia, hakukosa kumtimizia bintiye mahitaji yote yaliyohusu elimu... (uk. 37).

Wanachama wa Chama cha Maendeleo ya Wanawake ni wahusika wasaidizi. Wamesawiriwa na kupewa jukumu la wanawake ambao wanawajibika katika kuendeleza mwanamke. Wanamchagua Ruth kama kiongozi wao ambaye anawajibika. Wanachama hawa wanafanikisha maudhui ya nafasi ya mwanamke katika jamii. Wanaonyesha kuwa mwanamke ana nafasi ya kumkuza mwanamke mwenzake na hivyo basi kuikuza jamii:

> ...wanachama wa Chama cha Maendeleo ya Wanawake pale mtaani pao wakamchagua kushika uongozi wa chama chao; naye akakubali. Uongozi wake ukafana mno na kuleta maendeleo makubwa... (uk. 37).

Mhusika msaidizi Ben ni kiwakilishi cha kijana mwaminifu ambaye anathamini mapenzi na mwenye msimamo katika penzi lake kwa Ruth. Ruth anakosa msimamo katika penzi. Anampuuza Ben na kujipendekeza kwa John. Ruth anataka aoelewe na John. Amekuzwa ili kuonyesha dhamira kuwa

mwanamke ni kiumbe mwenye tamaa na asiye na msimamo thabiti katika mapenzi:

> ...Yule aliyesemekana kuwa ndiye atakayemwoa Ruth alikuwa akiitwa Ben. Alimwandikia Ruth barua ya kumwarifu kwamba angekuwa mgeni wake siku ya Jumamosi. Ruth aliipokea barua ile, aliifungua na kabla ya kumaliza kuisoma, alitupa macho mwisho wa barua; alipoona jina la Ben alichana hiyo barua na kuitupa ndani ya moto... (uk.38).

Mhusika mdogo Seth ni kiwakilishi cha watu ambao huwa na moyo wa kusaidia wanajamii wengine. Ben anapomuuliza nyumba anayoishi Ruth anamwonyesha bila kusitasita. Seth amesawiriwa ili kufanikisha maudhui ya utu:

> ...Ben akafunga safari na kupanda basi mpaka mjini. Hakujua nyumba aliyokuwa akikaa Ruth kwa hivyo ilimbidi kumwuliza Seth, mwenye hoteli mmoja. Bwana Seth akamwonyesha nyumbani kwa yule kipusa... (uk. 38).

Mhusika msaidizi John ni kiwakilishi cha wanaume ambao wanawachukulia wanawake kama vyombo vya kujistarehesha. Mwanzoni anakubali kuchumbiana na Ruth hadi Ruth anampuuza mpenzi wake halisi ambaye ni Ben. John anapopata uhamisho, Ruth anasisitiza waende wote na pia waoane ndiposa John anaamua kumwambia ukweli haiwezekani maana ana mke na watoto. Mwandishi amekuza dhamira ya mwanamke kuchukuliwa kama chombo cha starehe kupitia kwa mhusika John:

> ...Ruth aliposikia hivyo alifadhaika sana, alimhoji sana John na kumsihi kwamba ingefaa na yeye pia aiache kazi ili wafuatane wote mpaka Mwanza wakaoane huko.John alikunja uso na kumwambia, nasikitika nilikuwa sijakueleza kwamba nimeoa na nina watoto wawili... (uk. 41).

Mhusika bapa sugu Joyce ni kiwakilishi cha wafanyakazi ambao wamewajibika na wenye maadili. Anapompata Ben nyumbani kwa Ruth

anamhudumia kwa unyenyekevu na heshima. Anamwonyesha mahali pa malazi. Maudhui ya uwajibikaji na maadili yanafanikishwa kupitia kwa Joyce:

> ...Yule msichana akamwambia kweli Ruth ameharibika siku hizi. Anathubutuje kukuacha hapa na wewe ni mgeni wake?...Joyce akaenda jikoni na kushughulika kupika chakula cha Ben. Baada ya chakula, Joyce akamwonyesha Ben mahali Pa kulala, wakaagana... (uk. 40).

Mhusika mdogo Bwana Maina ni kiwakilishi cha wananchi ambao wanafuata sheria kwa kutochukua sheria mikononi mwao. Ukuta wake unapogongwa na Ruth akiendesha gari akiwa mlevi anasubiri haki ichukue nafasi yake. Baadaye analipwa fidia ya kubomolewa ukuta wa nyumba yake. Dhamira ya athari hasi inayotokana na ulevi inabainika kupitia kwa Bwana Maina anayelipwa fidia na Ruth anayesababisha ajali akiwa mlevi:

> ...Usukani ukamponyoka na gari ikagonga ukuta wa nyumba ya Bwana Maina. Gari hiyo ilipondeka pondeka vibaya haikuweza kutengenezwa kamwe...zaidi ya hayo ikamlazimu kumlipa Bwana Maina fidia ya nyumba yake... (uk. 41).

Naye dereva wa teksi anayembeba Ruth huko Dar es Salaam ni mhusika duara. Jukumu lake ni kuelimisha jamii umuhimu wa kutoamini watu ovyo ovyo. Anawakilisha watu ambao si waaminifu kutokana na tabia yao ya wizi:

> ...mhuni alipofika nyumbani akasema moyoni mwake unaona basi, Mungu akupe, akupe nini donda! Nilichokuwa nikitafuta si hiki? Akaingia ndani akakusanya kila kitu hata sanduku la Ruth, akabana mlango, huyoo! (uk. 43).

Majirani wa Ruth huko Dar es Salaam ni wahusika wadogo. Wao ni kiwakilishi cha majirani ambao hawawajibiki. Mhuni alipokuwa anabeba vitu wangechukuwa simu na kumpigia Ruth ili kuthibitisha iwapo alikuwa anafahamu kilichokuwa kikiendelea. Tatizo lao ni kuwa walimwamini huyo

Mhuni. Dhamira ya kukashifu hali ya kutowajibika inafanikishwa kupitia kwa majirani wa Ruth:

> ...Akaenda zake. Akawaambia majirani wamweleze Ruth kwamba alikuwa amefukuzwa pale kwa sababu ya kutolipa kodi ya nyumba... (uk. 43).

Jamaa anayesababisha ajali ya mauti ya Ruth na yeye mwenyewe ni mhusika msaidizi. Yeye ni kiwakilishi cha vijana ambao wameathirika na uraibu wa pombe na starehe. Uraibu huu ndio unampelekea kufanya ajali kubwa ajabu yenye madhara ya mauti. Dhamira ya athari ya ulevi imekuzwa kupitia jamaa huyu:

> ...Ruth akabaki akilia wala asijuwe la kufanya, akakosa hata mahali pa kulala usiku ule. Mwishowe akaona heri azurure zurure kwenye mabaa...yule jamaa alikuwa top hata hakujali mwendo wa gari. Ghafla walishtukia gari yao imeingia chini ya lori kubwa. Ile gari yao ilisagwa sagwa kabisa hata wao pia wakaacha roho zao pale pale... (uk. 44).

Tofauti na hadithi nyingine, hadithi hii ina wahusika kumi na wawili lakini wahusika wanne wanajitokeza kama wahusika wadogo. Mhusika Seth, Bwana Maina, wake kumi na wawili wa babake Ruth na majirani wa Ruth huko Magomeni ni wahusika wadogo. Hivyo basi, wahusika wanane ndio wenye mchango mkubwa katika kufanikisha dhamira na maudhui ya hadithi fupi teule.

3.3.5 Idadi ya Wahusika na Jukumu lao katika Hadithi, “Mzee Khamis, Leo Wapi?” (Mohamed, 1971)

Msingi wa hadithi fupi ni usawiri wa wahusika, hadithi fupi inastahili kuwa na idadi ndogo ya wahusika. Vilevile, mhusika mmoja anaweza kuwa mcheshi ili hadithi ivutie hadhira (Lyon, 2014). Katika hadithi hii, idadi ya wahusika ni

saba: Mzee Khamis, watoto wa mtaani, Bin Barak, mpishi katika maulidi ya Bin Barak, Mazengo, Pusi na babu mmoja mkongwe. Ukuzaji wa wahusika hawa unasaidia katika kujenga dhamira na maudhui ya hadithi kama ifuatavyo:

Mhusika mkuu ni Mzee Khamis. Anasawiriwa kama kiwakilishi cha wanajamii ambao wametawaliwa na ulafi. Ulafi wake umepita kiasi, inasemekana hapendi kukosa wali wa mahali popote pale. Athari ya ulafi katika jamii inakashifiwa kupitia kwa Mzee Khamis:

> ...Hitima gani wende usimkute Mzee Khamis, kama ataachiwa daste la halua huweza kulibeba lote. Karamu za arusi, maulidi, sherehe za jando hazimkosi mzee huyo hata ziwe wapi... (uk. 7).

Wahusika watoto ni wahusika wasaidizi katika hadithi. Jukumu lao ni kumfahamisha Mzee Khamis mahali ambapo pana hafla ili kama ilivyo ada kwake aende angalau apate kula wali. Jukumu la watoto hawa ni kusisitiza tabia ya ulafi inayoonekana kwa Mzee Khamis na hivyo kukuza maudhui ya tamaa na ulafi:

> Alikwisha pata habari kutoka na watoto ambao huzunguka mji mzima hata mashamba kwa udokezi wa wali na halua... (uk. 7).

Vilevile, mhusika msaidizi Bin Barak ni kielelezo cha wanajamii ambao wapo katika tabaka la juu lakini hawatengi wanajamii wa tabaka la chini. Anaamua kuandaa maulidi ambayo yanahudhuriwa na watu mbalimbali akiwemo Mzee Khamis. Dhima ya Bin Barak ni kujenga maudhui ya utabaka kwa sababu ya uwezo wake kuandaa maulidi na kuwepo kwa chakula kingi:

> ...Maulidi hayo safari hii yalikuwa kwa Bin Barak. Mzee Khamis alisema peke yake, sufuria saba za pilau! (uk. 7).

Mhusika msaidizi mpishi katika maulidi ya Bin Barak anapewa jukumu la kukashifu tabia ya ulafi hadharani ili kukuza jamii yenye maadili:

> ...mpishi alipomwona akisogea alimuhamakia, Mzee Khamis, unajisogeza nini? Unataka kutushughulisha tu. Kaa upande. Ukifika hapa nitakupiga mwiko. Mzee Khamis akahisi maonevu... (uk. 8).

Mhusika msaidizi Mazengo ni kiwakilishi cha wanajamii ambao wanatangamana na wengine vyema kwa kuelewa utofauti wa binadamu na kuishi nao kwa amani. Ijapokuwa anamfanyia Mzee Khamis utani, utani huo ni wa kuleta ucheshi tu lakini haupiti mipaka ya kumvunjia heshima. Jukumu la Mazengo ni kuhamasisha umoja katika jamii, ni jukumu la mwanajamii kumwelewa kila mmoja alivyo licha ya utofauti wa tabia:

> ...Mazengo, kijana aliyekuwa akipenda kumtania Mzee Khamis, alitishia kutaka kuiondoa sinia. Mzee Khamis alikitoa kisu chake na kuapa kuwa atamwua... (uk. 9).

Pusi ni jina la paka wa Mzee Khamis, paka amesawiriwa kama mhusika msaidizi. Jukumu lake ni kuendeleza dhamira ya athari ya ulafi. Anapokula chakula cha Mzee Khamis, mzee huyo anaamua kufunga dirisha na mlango ili ampe adhabu. Aidha, paka anamjeruhi kwa makucha na ndiposa anafungua mlango na kutoroka nje akilia kwa uchungu:

> "...Aliposhtuka, jicho alilitupa kwenye kishubaka, ndipo kumwona pusi kashughulika kuiseketua nyama...pusi alimrukia mzee huyo kwa hamaki akamparura makucha usoni... (uk. 10).

Babu mkongwe ni mhusika mdogo. Amesawiriwa kama mwenye jukumu la kuonyesha utu. Mzee Khamis anapozama baharini, babu mkongwe

anamwokoa Mzee Khamis na kushughulika namna ambavyo atapata matibabu hospitalini. Maudhui ya utu yanaendelezwa kupitia kwa babu mkongwe:

> ...Alipofumbua macho alijihisi yumo ndani ya behewa. Akaangaza mle ndani akajihisi yumo kwenye gari la hospitali lililokuwa ndani ya mwendo. Upande wa kulia alikuweko babu mmoja mkongwe amekaa. Huyu ni bwana aliyemwokoa Mzee Khamis kwenye ngarawa... (uk. 11).

Tathmini ya idadi ya wahusika na jukumu lao katika hadithi fupi teule inabainisha kuwa wahusika wachache wanatumiwa kufanikisha dhamira na maudhui ya hadithi. Maudhui ya ulafi yanaelezwa kupitia Mzee Khamis ambaye anaibua ucheshi kutokana na ulafi wake uliopita kiasi. Hivyo basi, ubora wa hadithi unajitokeza kwa sababu hadithi inazingatia mojawapo ya kanuni za hadithi fupi zilizowekwa na Poe (1846).

3.3.6 Idadi ya Wahusika na Jukumu lao katika Hadithi, “Malipo Duniani, Hesabu Ahera” (Said, 1971)

Kwa mujibu wa Hills (2000), wahusika wachache wanahitajika katika kusanii hadithi fupi na hawapambanuliwi kwa mapana kama katika riwaya ili hadithi kusomeka katika kikao kimoja. Hadithi hii ina wahusika tisa: Mzee Miraji, Bi. Asha, Kombo, Fatuma, watoto wa mtaani, walimu wa Kombo katika shule ya msingi, rafiki zake Kombo wa mtaani, mke wa Kombo na Miraji ambaye ni mtoto wa Kombo. Dhima ya kila mhusika hususani kupitia ukuzaji wake inasaidia katika kueleza maudhui na dhamira ya hadithi kama ifuatavyo:

Mhusika Mzee Miraji ni mhusika msaidizi. Amepewa jukumu la kufanikisha maudhui ya malezi kwa sababu anajibidisha kuwapa wanawe Fatuma na Kombo maelekezo yanayokuza maadili yao:

> ...Hatimaye saa zikafika na baba mtu akajiona yu hoi, ndipo alipomwita Fatuma akamuusia, ukitaka radhi zangu lazima umwangalie Kombo na mama yako pia...Niitie huyo Kombo. Kombo akafika kichwa chini. Ukitaka radhi zangu lazima uache mchezo wako... (uk. 13).

Mhusika msaidizi Bi. Asha ni kiwakilishi cha wanawake ambao wanawajibika katika maisha ya ndoa. Anawajibika kama mke wa mzee Miraji kwa kuhakikisha kuwa nyumba yake ni safi. Anakuzwa ili kujenga maudhui ya uwajibikaji:

> ...Hapana nyumba safi pale mtaani kushinda ya Bwana Miraji, na kelele za fagio zilisikika mara kwa mara- alikuwa Bi. Asha akifagia au kuosha choo... (uk. 12).

Naye Kombo ni mhusika mkuu mwenye jukumu la kuonyesha kwamba ingawa mtoto anaweza kuwa mtukutu, wakati hufika na mwishowe akabadilika na kuwa mwenye nidhamu. Hata hivyo, upo uwezekano mtu apate mtoto mtukutu kama yeye. Malipo ya utukutu aliokuwa nao kwa waliomlea. Dhamira ya kusisitiza umuhimu wa nidhamu inaendelezwa kupitia kwa Kombo:

> ...Baada ya mwaka mmoja wa kujitahidi, Kombo alifikia kwa urahisi darasa la nane, na hatimaye aliingia sekondari. Huku alijitahidi kikwelikweli naye akawa mwanafunzi wa kupigiwa mfano...Kombo alikuwa kama ana wazimu kwa makelele anayoyapiga mara kwa mara kumkemea Miraji... (uk. 14).

Mhusika mdogo Fatuma ni kiwakilishi cha watoto ambao ni kielelezo bora katika jamii kwa sababu nidhamu yake ni ya kupigiwa mfano na wazazi,

majirani, walimu pamoja na wanafunzi wenzake. Jukumu la Fatuma ni kusisitiza umuhimu wa nidhamu:

> ...Kipenzi cha wazee wake alikuwa Fatuma, naye alikuwa mkubwa wa nduguye Kombo. Fatuma, mwenye umri wa miaka yapata kumi na tano hivi, alikuwa mpole na mwenye huruma, na tabia nzuri hii haikukawia kuvutia mashogaze wa darasa la nane... (uk. 12).

Watoto wa mtaani ni wahusika wadogo. Wameelezwa ili kuonyesha nafasi ya watoto katika jamii. Watoto hawa katika jamii wana nafasi ya kucheza na ni muhimu wapewe nafasi ya kucheza kwani ni sehemu ya makuzi yao. Dhamira inayoendelezwa na watoto hawa ni kusisitiza nafasi ya mchezo katika makuzi ya watoto:

> ...Mzee Miraji alijaribu sana kuuweka safi ukuta wake kwa kupaka chokaa mwaka hata mwaka. Lakini wapi! Haikuwa ndio kinga ya watoto na vijitoto wa pale pale Mtaani kuufanya ndio karatasi yao ya kuandika maneno wayatakayo... (uk.12).

Walimu wa Kombo ni wahusika wasaidizi. Wanapewa jukumu la kuonyesha nafasi ya walimu katika ukuzaji wa maadili, vipawa pamoja na elimu. Ingawa Kombo ni mtovu wa nidhamu wanajaribu kumpa wasia na hata nafasi ashiriki katika michezo na anadhihirisha ubora wake. Jukumu la walimu ni kukuza maudhui ya maadili, ukuzaji vipawa na elimu:

> Alikuwa mkimbiaji mashuhuri...ndiye aliyeleta kombe mwaka 66... (uk. 13).

Rafiki zake Kombo ni wahusika bapa sugu. Wanajaribu kumrudisha Kombo katika tabia ya upotovu wa nidhamu lakini Kombo anadhihirisha kuwa na msimamo thabiti wa kuwa mwenye maadili mema. Rafiki zake wanapotaka waende kulenga njiwa wa watu kwa manati anawafukuza. Jukumu la rafiki za

Kombo ni kufanikisha dhamira ya athari ya marafiki wabaya katika malezi ya mtoto:

> ...asubuhi ikafika, vijana kama desturi yao wakagonga dirisha la mbao ... Kombo Akatoka nje huku anapaniapania lile shati lake la maraka, akawashambulia, ondokeni hapa... (uk.13).

Mke wa Kombo ni mhusika mdogo. Yeye ni kiwakilishi cha wanawake katika jamii ambao wanajituma kwenye elimu. Kupatana kwake na Kombo huko Uingereza ambako Kombo anasomea udaktari ni ishara ya kuwa ni mwanamke aliyeelimika. Jukumu la Mke wa Kombo ni kukuza maudhui ya elimu kwa jinsia ya kike:

> Huko Uingereza akafuzu na akakumbana na mwana wa kwao mmoja akampenda na akaoa... (uk. 14).

Mhusika msaidizi Miraji ni mtoto ambaye ni kifungua mimba wa Kombo. Kombo anapokuwa mdogo inadhihirika wazi kwamba anamsumbua babake kwa kuwa mtukutu. Sadfa ni kuwa anajaaliwa mtoto mtukutu kama alivyokuwa yeye. Miraji amesawiriwa ili kupatia kichwa cha hadithi uhai kuwa ukimtendea mzazi maovu malipo yake ni papa hapa duniani:

> ...Kombo alikuwa kama ana wazimu kwa makelele anayopiga mara kwa mara kumkemea Miraji... (uk. 14).

Maudhui na dhamira ya hadithi fupi teule yanafanikishwa kupitia wahusika wachache ambao wamepewa majukumu mbalimbali katika hadithi. Ubora wa hadithi unatokana na hadithi kutimiza lengo lake katika muda wa kikao kimoja kwa sababu wahusika wake hawapambanuliwi kwa mapana kama vile katika riwaya (Poe, 1846).

3.3.7 Idadi ya Wahusika na Jukumu lao katika Hadithi, “Sina Rafiki” (Wahab, 1977)

Fagih (2008) anaeleza kuwa hadithi fupi inastahili kutumia wahusika wachache lakini itakuwa udhaifu iwapo majina ya wahusika yatakua yale yamezoeleka na wanajamii kama vile jina Ahmad kwenye mazingira ya Uswahilini. Katika hadithi hii, kuna idadi ya wahusika tisa: Hasan, Karama, Bi. Asha, kijana anayepokea habari za kifo cha Karama, Bwana Musa, askari anayempa Hasan ripoti ya kutakikana kwa Hasan kwenye stesheni, inspekta wa askari, mtu anayevaa kama raia Hasan anapohojiwa na idara ya mahakama. Kutokana na jukumu la kila mhusika katika hadithi, maudhui na dhamira inajitokeza kama ifuatavyo:

Mhusika mkuu Hasan ni kiwakilishi cha marafiki ambao wanaishi kutegemea wenzao. Kuendelea kiuchumi kwa rafiki yake kunampa roho ya wivu. Hasan anamwonea kinyongo rafiki yake Karama ambaye anafanya bidii ili kujiendeleza kiuchumi. Jukumu la Hasan ni kukuza dhamira ya athari ya wivu na tamaa kwa sababu tamaa yake inajenga wivu hadi anamuua Hasan:

> ...Aliwaza Hasan, Karama hana yeyote, yeye tu na ana mapesa hata hajui afanye nini! Na mimi nipo hapa hohe hahe!...Hata wakitia shaka watapata wapi ithibati kamili? (uk. 2).

Mhusika mkuu Karama ni kielelezo cha watu ambao hujituma katika maisha ili kuhakikisha wameimarika kiuchumi. Anatumia mbinu halali katika kusaka riziki kwa kujituma kuuza katika duka lake. Jukumu la Karama ni kujenga maudhui ya bidii na kazi:

> ...pale alipokuwa akivuta sigireti, Hasan aliweza kuona watu waliojaa na kusongana Dukani kwa Karama... (uk. 1).

Naye Bi. Asha ni mhusika msaidizi. Yeye ni kielelezo cha wanawake wenye mapenzi kwa waume wao. Karama anapoaga anahisi uchungu kutokana na ukweli kuwa anaaga dunia bila kufaidi pesa alizokuwa anatafuta kwa bidii. Maudhui ya mapenzi yanajengwa kupitia kwa Bi. Asha:

> ...He! Mapesa yote haya! Masikini mume wangu hata hajawahi kuzifaidi! Hapo alijipweteka chini, machozi yakimtiririka... (uk. 7).

Kijana anayepata habari za kifo cha Karama ni mhusika mdogo. Amesawiriwa ili kuonyesha uhusiano mwema uliopo baina ya Karama na jirani zake. Kutokana na kijana huyu kulia na kugubikwa na majonzi ni ishara tosha kuwa Karama ni jirani mwema. Jukumu la kijana huyu ni kuendeleza dhamira ya umuhimu wa majirani kuishi kwa utangamano mwema:

> ...simu ya pale kibandani karibu na duka la Karama ililia, kijana mmoja alikimbilia kwenda kusikiliza. Alipotoka mle ndani kijana yule alionyesha amefadhaika sana... (uk. 4).

Mhusika foili Bwana Musa ni kielelezo cha wazee wenye busara katika jamii. Jukumu lake ni kuelekeza wanajamii wengine. Kunapozuka utata au suala linalohitaji utatuzi anatoa maelekezo ya busara. Dhima ya Bwana Musa ni kusisitiza umuhimu wa wazee kama washauri wakuu kwa wanajamii:

> ...alimwita bwana Musa. Baada ya kufika na kumkaribisha alimwomba amtaftie nyumba au shamba ili iwe ndio rasilimali yake. Bwana Musa alipokea utumwa huo...Baadaye bibi huyo alifunga waraka zake zote akazitia katika kile kidawati na kumkabidhi bwana Musa amwekee. (uk. 8).

Idara ya mahakama imejitokeza kama mhusika bapa sugu. Imetumiwa ili kuonyesha kuwa wanajamii wakifuata mkondo wa sheria ipasavyo basi haki

nayo husimama wakati ukifika. Jukumu la idara ya mahakama ni kusisitiza umuhimu wa kufuata sheria kwa wanajamii katika kutafuta haki:

> Bwana Musa alikuwa wa mwanzo kuingia ndani kwa maiti...alifululiza mpaka Idara ya Afya...Askari wengine walimfuata...Baada ya mwezi kupita, watu walisikia katika redio kuwa, mahakama kuu ya nchi imekuhukumu, Hasan Ali kunyongwa kwa kosa la kumuua Karama Said na mkewe... (uk. 11).

Askari, inspekta wa askari na mtu aliyevaa kiraia ni wahusika bapa sugu. Jukumu lao ni kuonyesha namna ambavyo idara ya polisi hujituma au huwajibika katika kufanya upelelezi ili kufanikisha idara ya mahakama kutoa hukumu. Jukumu la wahusika hawa ni kukuza maudhui ya haki:

> ...alifika askari pale dukani na baada ya kuuliza...kule stesheni alipelekwa katika chumba ambamo alikuwemo inspekta askari mmoja na mtu mwengine aliyevaa kiraia. Baada ya kukaa kitako, inspekta alimuuliza Bwana Hasan, nani aliyekuruhusu kuuza duka la Karama?... (uk. 5).

Hadithi fupi teule inatumia wahusika wachache katika kuwasilisha lengo la hadithi. Aidha, jukumu la kila mhusika linaelezwa kwa ukamilifu ili kujenga matukio mbalimbali katika hadithi. Hata hivyo, mwandishi anatumia majina ya wahusika yaliozoeleka katika utamaduni wa Uswahilini kama vile Hasan na Bi. Asha. Mwandishi angeteua majina kama Zawadi na Sifa. Hata hivyo, mwandishi ametumia jina Karama ambalo halijazoeleka sana. Ubora wa hadithi unatokana na hadithi kutumia idadi ndogo ya wahusika. Hadithi hii inafuata mojawapo ya vipengele vya tathmini ya ubora wa hadithi fupi kwa mujibu wa Poe (1846).

3.3.8 Idadi ya Wahusika na Jukumu lao katika Hadithi, “Mke Wangu” (Muhammed, 1977)

Ubora wa hadithi fupi hutokana na wahusika kuwa wachache. Wahusika wanastahili kusawiriwa kwa njia maalumu inayoipa hadithi mwanzo na mwisho unaovutia hadhira lengwa (Pitlor, 2011). Hadithi hii ina idadi ya wahusika kumi: msimulizi, Aziza, wazazi wa msimulizi, Fedhele Salim, Salma Fadhil, Mapanya, shoga yake Fedhele, kijana mwanamume ambaye alikuwa amesimama katikati ya Fedhele na shoga yake Fedhele, Seluwa na muuza madafu. Ukuzaji wa wahusika hawa kwa majukumu yao mbalimbali unafanikisha dhamira na maudhui ya hadithi kwa namna ifuatayo:

Mhusika mkuu ni msimulizi wa hadithi. Amepewa jukumu la kujenga maudhui ya ndoa. Anaeleza vigezo ambavyo alitumia ili kumuoa mke wake ambaye amemridhia baada ya kuchaguliwa na wazazi wake. Kupitia kwa msimulizi, tunapata kuelewa nafasi ya mwanamke katika jamii. Namna ambavyo mwanamke anachukuliwa na mwanamume:

> ...mimi nilitaka mke mtoto mbichi, nimvumbike mwenyewe mpaka aive. Na Aziza nilimwelekeza atakuwa hivyo kwa sababu, kwanza, hakusoma skuli akapata kuwa mjuaji sana, wala hakukulia mjini akapata kukalamka kwa utamaduni... (uk. 48).

Vilevile, Aziza ni mhusika mkuu. Yeye ni mfano wa mwanamke ambaye anafahamu majukumu ya mwanamke na mwanamume kwenye ndoa. Kulingana naye, mwanamume anafaa kujituma katika kutafuta riziki kwa njia halali. Anaamini kazi ni kazi mradi tu ni halali. Jukumu la Aziza ni kukuza maudhui ya uwajibikaji hasa kwa mwanamume kwenye maisha ya ndoa:

> ...Nimemwita bwana huyu aje huku kusudi mumwone, Aziza alihutubu. Huyu ni binadamu kamili, kwani huyu ni mkulima, tena ni mfanyakazi. Pesa anazopata huyu ni za halali; hana haja ya kitu cha wazee. Huyu ni mwanamume, hafikiri kukaa akachana nywele... (uk. 57).

Wazazi wa msimulizi ni wahusika wasaidizi. Wamepewa jukumu la kuonyesha namna ambavyo utamaduni mwengine huchangia katika kuharibu ndoa. Utamaduni wa wazazi kutendekeza mtoto wa kiume humfanya asijitume kimaisha kwa kuwategemea wazazi wake hata akiwa na familia yake. Jukumu lao ni kuonyesha changamoto za ndoa zinazosababishwa na wazazi:

> ...Baada ya arusi na sherehe zake, mke wangu alikuja kuhamia kwetu nyumbani. Katika mpango wao, wazee walitutengea vyumba vitatu vikubwa juu ghorofani peke yetu; chakula kikipikwa huko huko kwa wazee, na sisi tukiletewa chetu... (uk. 49).

Wahusika wadogo Fedhele Salim, shoga yake Fedhele na kijana mwanamume ni mfano wa vijana ambao wamekengeuka kimaadili. Wanatembea usiku pamoja na kuvaa mavazi yasiyo na stara. Salma Fadhili anajiremba uso kwa rangi ya kila aina ili apendeze. Dhima ya wahusika hawa vijana ni kuonyesha athari za utamaduni wa usasa katika maisha ya vijana:

> ...Fedhele! Yule niliyemkuta saateni saa mbili usiku- sijui mimi nilikuwa narudi kutoka wapi vile? Kavaa kanzu mpaka mapajani, kafuatana na shoga yake na wamemtia kijana mwanamume katikati yao...Namjuwa Salma. Yeye ni mtamaduni wa kutosha. Simtaki kwa utamaduni wake. Sura yake daima anaificha kwa kujiremba marangi ya mashavu na mdomo... (uk. 48).

Mhusika bapa sugu Mapanya ni kiwakilishi cha wafanyakazi wa nyumbani ambao wanawajibika katika kutekeleza majukumu yao. Anashughulika ipasavyo kufanya kazi za nyumba kwa kumhudumia msimulizi na Aziza

ambaye ni mke wake. Jukumu lake ni kukuza maudhui ya uwajibikaji katika kazi:

> ...sisi tukiletewa chetu kwa wakati, wakaa tatu kila siku. Nguo zake Aziza, Mapanya alikuwa akija akimchukulia kwenda kumfulia... (uk. 49).

Naye Seluwa ni mhusika msaidizi. Amesawiriwa ili kuonyesha mchango wa familia katika kukuza udugu. Anakuja kumtembelea msimulizi na mke wake na ni kupitia kwake ambapo angalau utani unasikika siku hiyo katika nyumba ya msimulizi.

> ...Seluwa kaja siku ile...hutoki maadam mimi mkeo nimefika, nilifungika tukawa Pamoja, na katika jumla ya mambo yake, moja ni lile la kuniingia maungoni kwa masihara ya upuzi na kutaniana na mke wangu kwa kuitana majina mara ‘mke mwenzangu’ na pengine ‘wifi yangu’. (uk. 55).

Mhusika foili muuza madafu ni kiwakilishi cha wanaume ambao wamewajibika na wanajituma katika kukidhi mahitaji ya familia zao. Aziza anatamani angepata mume kama yeye ambaye anajituma kufanya kazi bila kubagua. Jukumu la muuza madafu ni kielelezo cha uwajibikaji wa wanaume katika kufanya kazi:

> ...Basi huyu au mtu kama huyu ndiye mume wangu kifu yangu. Wewe, bwana, tumekaa kwa kuwa umenioa tu lakini si mume wangu. Nitakushukuru kama utanipa talaka yangu... (uk. 57).

Hadithi hii inathibitisha kuzingatia kanuni ya idadi chache ya wahusika kwa njia ya kipekee. Mwanzo wa hadithi unadhihirisha matumizi ya mbinu rejeshi na mwisho inaisha na taharuki maana hatujaelezwa kama msimulizi anampa Aziza talaka au la. Jukumu la kila mhusika linadhihirika ipasavyo kutokana na hadithi hii kuwasilisha dhamira kuu ya ndoa. Tofauti na hadithi nyingine,

ubora wa hadithi hii unaifanya kuchapishwa tena katika mkusanyiko wa *Damu Nyeusi* (2007).

3.4 Uthabiti wa Wahusika Wakuu katika Hadithi Teule

Uthabiti wa mhusika au wahusika ni kutobadilika kwa matendo ya mhusika anayewasilisha lengo kuu ili maudhui ya hadithi kueleweka kwa njia sahili (Moses, 2014). Kwa mujibu wa Wamitila (2002), hadithi fupi inastahili kuzingatia uthabiti hususani katika mwili wake kwa kuhakikisha wahusika hawabadiliki badiliki na endapo mabadiliko yao yataonekana basi kuwe na sababu yenye kuaminika. Uthabiti wa wahusika katika matendo yao husaidia kujenga dhamira na maudhui ya hadithi fupi. Uthabiti wa wahusika unafaa kuhakikisha kuwa wahusika pia wamekuzwa kikamilifu hasa kwa kuzingatia wahusika au mhusika anayeitawala hadithi (Wamitila, 2003). Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999), mhusika anayeitawala hadithi ni mhusika mkuu. Hadithi fupi hufanikisha uthabiti wa wahusika kwa kutumia maelezo sahili kueleza matendo sahili (Goyet, 2014). Uthabiti wa wahusika unadhihirika kama ifuatavyo katika hadithi fupi teule:

Mhusika Sadiki na Bahati ni wahusika wakuu katika hadithi ya “Siku ya Arobaini” (Mohamed, 1970). Uthabiti wa mhusika huleta uhalisia wa kuwepo kwa mhusika kama huyo katika jamii, mhusika mkuu hujengwa kwa kuzingatia tabia yake ambapo kama ni mchoyo abaki kuwa mchoyo katika hadithi ili aweze kuathiri hisia za msomaji au msikilizaji (Nasser, 2007). Sadiki anaendelea kuonyesha tamaa yake kwa wanawake wengine licha ya

kuwa na mke wake halali Bahati (uk. 24). Sadiki ni mume ambaye anakuza maudhui ya mgogoro katika ndoa pamoja na tamaa inayoweza kusambaratisha ndoa yake.

Uthabiti wa mhusika Bahati unajitokeza kama mhusika mdadisi ambaye anatumia mbinu zote ili kupata ukweli kuhusu mienendo ya mumewe Sadiki katika ndoa. Anaandika barua kujifanya ni kimada wa Sadiki ili kuhakikisha kama barua hiyo itamkutanisha na Sadiki baada ya rafiki zake Bahati kumwambia mumewe anamwendea kinyume kwenye maisha ya ndoa. Uthabiti wa matendo yake ya upelelezi unaleta suluhu ya mgogoro katika ndoa:

> ...Sadiki alinaswa mtegoni, kama ile barua aliyokuwa ameletewa ilikuwa imetoka kwa mkewe mwenyewe Bahati. Hadithi hii inathibitisha ule msemo maarufu wa Kiswahili, mwizi siku zake arobaini... (uk. 27).

Katika hadithi, “Kusoma na Kupenda” (Salim, 1970) Zubeda na Abdu ni wanafunzi ambao uthabiti wao unadhihirika kutokana na ukuzaji wao kama wanafunzi ambao badala ya kuzingatia masomo wanajitosa katika mapenzi. Athari ya mapenzi kabla ya kumaliza masomo ni kuwa wanakwenda kinyume na sheria za shule kutokana na wao kupigana busu kwa kujificha kwenye darasa lisilo na wanafunzi. Dhamira ya hadithi ni ukuzaji wa maadili miongoni mwa wanafunzi ili wazingatie elimu. Mwalimu mkuu anapewa mashtaka na Rama ambaye ni mlinzi wa shule na anachukuwa hatua ya kuwafukuza ili wawaite wazazi wao:

> ...aliwaamuru waende makwao wakawaite wazazi wao na wasipofanya hivyo basi wasihudhurie tena shule... (uk. 44).

Katika hadithi ya “Ajuta Majuto ya Mjukuu” (Somba, 1970) Kamene na Wayua wamepewa uthabiti wa wahusika ambao wanapitia dhuluma za utamaduni uliopitwa na wakati. Wayua ambaye ni dadake Kamene anaozwa kwa Kyalo na madhara yake ni afya kudhoofika pamoja na kujifungua watoto wengi (uk. 6). Uthabiti wa ukuzaji wa mhusika huyu katika harakati za kuozwa mapema unakuza dhamira ya athari ya ndoa za mapema.

Naye Wayua anapangiwa ndoa baina yake na Kitonga na athari yake ni kwamba mauti yanatokea. Anawatilia sumu katika pombe; babake, Kitonga na wageni wanaoandamana na Kitonga wanaaga dunia. Kando na wao, anapotoroka anagongwa na gari njiani na mwishowe anaaga dunia. Wayua anachukua hatua hizi kama suluhu za ndoa ya lazima anayopangiwa. Ukuzaji wa mhusika Wayua kwa uthabiti unajenga dhamira ya kukashifu ndoa za mapema na lazima:

> ...Kamene akapokelewa vema kule hospitali na matibabu yakaanza saa ile ile, lakini juu ya jitihada kuu iliyofanywa na matabibu, moyo wa Kamene ulikuwa hafifu na punde si punde yeye pia akaaga dunia...ya nini Kamene kwenda kumwua baba yake na yule mchumba wake... (uk. 11).

Mhusika Ruth ni mhusika mkuu katika hadithi, “Maisha Yalimwendea Kombo” (Isaakwisa, 1970). Uthabiti wa mhusika Ruth unabainika kutokana na maamuzi ambayo anafanya. Tamaa yake ya anasa za ulevi inafanya maisha kumwendea kombo. Anakumbwa na tamaa ya kwenda mjini kufanya starehe ya pombe na densi na hatima yake ni kuuza mali nyingi aliyokuwa amewachiwa na marehemu babake. Tamaa za anasa zinamfanya kupoteza pesa zake pamoja na uhai wake kwani anapopata uhamisho wa kwenda Dar es

Salaam bado anajitosa katika starehe za ulevi. Dhamira ya athari ya ulevi inawasilishwa kupitia uthabiti wa mhusika Ruth kuwa mlevi, ulevi unaomletea mauti:

> ...Ruth akabaki akilia wala asijuwe la kufanya, akakosa hata mahala pa kulala usiku ule...ghafla walishtukia gari yao imeingia chini ya lori kubwa. Ile gari yao ilisagwa kabisa hata wao pia wakaacha roho zao pale pale... (uk. 44).

Katika hadithi, "Mzee Khamis, Leo Wapi?" (Mohamed, 1971). Dhamira ya kukashifu ulafi inakuzwa kupitia uthabiti wa matendo au tabia ya Mzee Khamis. Mhusika huyu amekuzwa kutokana na sifa ya kuwa hakosekani katika hafla yoyote ile, hasubiri hata mwaliko. Anatembea mwendo mrefu mradi tu awahi wali. Kando na hayo, anahatarisha maisha yake sababu kuu ikiwa wali. Paka anapokula chakula chake anajifungia ndani pamoja na paka huyo na kuanza kumtia adabu kwa kumpiga bakora. Paka anamtia Mzee Khamis majeraha ya kucha. Aidha, anazama baharini wakati ambapo anaogelea ili akawahi wali kisiwani Tumbatu. Mzee Khamis amekuzwa kwa uthabiti wa tabia ya ulafi. Sababu ya ukuzaji huu ni kukashifu tabia ya ulafi katika jamii:

> ...hapakuwa na mtumbwi wa kumvusha mpaka Tumbatu. Ingawa alisubiri sana hapakutokea chochote. Wasiwasi wa kukosa wali ukamjaa. Akakumbuka taabu yake ya mwendo. Moyo ukamshawishi, utakwenda karamu ishaliwa nawe utakosa mengi. Pale tu, si mbali ati. Haya jitose... (uk. 11).

Mhusika Mzee Miraji katika hadithi ya "Malipo Duniani Hesabu Ahera" (Said, 1971) anapewa uthabiti wa mzee ambaye anajituma katika kukuza maadili ya watoto wake Fatuma na Kombo. Uthabiti wa ukuzaji wake

unasaidia kujenga maudhui ya malezi. Kabla ya kuaga dunia, anawaita watoto wake na kuwaachia wasia ambao ni muhimu sana katika maisha yao (uk. 13). Vilevile, Kombo ni mhusika mkuu. Anasawiriwa kama mhusika mwenye matendo ya kuudhi na mtukutu. Utukutu wake unajulikana na wazazi wake, rafiki zake, walimu na hata majirani zao. Anfanya uamuzi wa kubadilisha tabia baada ya wasia wa babake kabla hajafa. Licha ya Kombo kubadilika na kuwa na nidhamu, anaoa na kujaaliwa mtoto mtukutu kama alivyokua yeye. Mtoto huyu anaitwa Miraji. Anamsumbua Kombo jambo linalofanya watu kukisia kuwa malipo kweli ni duniani na hesabu ni ahera. Uthabiti wa ukuzaji wa Kombo kama mwana mtukutu ambaye baadaye anajaaliwa mtoto mtukutu kama alivyokua yeye kwa jina Miraji unafanikisha dhamira ya kusisitiza umuhimu wa nidhamu wakati wa malezi:

> ...Kila unapokwenda ambapo utakuta watu wanapiga domo, basi utasikia habari za Miraji. Watu wengi wanasema huyu si mtoto bali ni malaika aliyeshushwa kuja kumwonyesha Kombo uchungu wa kumtaabisha mzee wake, wengine wanasema ati Kombo amekosa radhi za mzee wake... (uk. 14).

Katika hadithi, “Sina Rafiki” (Wahab, 1977) Hasan anaendelezwa kama mhusika ambaye ametawaliwa na tamaa inayompelekea kuingiwa na roho ya ukatili. Uthabiti wake kama mhusika mwenye tamaa unadhihirika kuanzia mwanzoni mwa hadithi. Mgogoro wa tamaa unakuzwa hadi suluhu ya mgogoro huu inapatikana. Tamaa ya kumiliki mali ya rafiki yake Karama inampelekea kumuua Karama pamoja na mke wake Bi. Asha. Uchunguzi unafanywa na kukamilika. Hasan anapatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo cha maisha gerezani. Uthabiti wa matendo yake ya kikatili ni kukuza dhamira ya athari ya tamaa na wivu:

> ...Baada ya mwezi kupita, watu walisikia katika redio kuwa, mahakama kuu ya nchi imemhukumu Hasan Ali kunyongwa kwa kosa la kumuua Karama Said na mkewe Bi. Asha... (uk. 11).

Msimulizi na Aziza ni wahusika wakuu katika hadithi ya "Mke Wangu" (Muhammed, 1977). Uthabiti wa msimulizi unakuzwa kama mhusika ambaye anaamini mwanamke chaguo lake ni yule ambaye hajaathiriwa na utamaduni wa kisasa. Anapendekezewa wake mbalimbali na wazazi wake, anawakataa hadi mwisho anapotajiwa Aziza ndipo anamridhia kwa kuamini kuwa ana hulka ambazo yeye anazitaka (uk. 49). Aidha, baadaye anastaajabu kujua kuwa anapodhani atamfunza mkewe ustaarabu anajipata yeye ndiye anafunzwa. Maudhui ya mgogoro katika ndoa yanaendelezwa kupitia kwa uthabiti wa imani ya msimulizi kuwa Aziza ameathirika na utamaduni wa mashambani.

Aziza anajitokeza kama mwanamke asiyependa mwanamume ambaye hafanyi kazi bali anawategemea wazazi wake. Aziza anaamini mwanamume halisi hapaswi kuchagua kazi maadamu ni halali. Uthabiti wa msimamo wa Aziza wa kukashifu msimulizi kutofanya kazi unakuza maudhui ya mgogoro katika ndoa kwa sababu msimulizi bado anategemea wapewe chakula na wazazi wake. Suala hili la msimulizi kutojituma kusaka kazi ama kufanya kazi yoyote linamfanya Aziza kuudhika na kuona aliolewa na gumegume:

> ...chana nywele zako ukatembee huko ndilo unaloweza kufanya; nini zaidi kuliko hilo! Jambo la kufanya kazi liko baidi na wewe. Halidhukuru wala halikupitii rohoni mwako. Uko chini ya wazee wako tu baas, kama mtoto unayenyonya... (uk. 50).

Uthabiti wa wahusika wakuu haudhihiriki katika kila hadithi fupi teule. Baadhi ya wahusika wakuu katika hadithi fupi wanabailika ili kufanikisha dhamira inayokusudiwa kama vile athari ya mgogoro katika ndoa. Tofauti na maoni ya Poe (1846), utathmini wa hadithi fupi teule hizi unaonyesha kuwa uthabiti wa wahusika wakuu hutegemea lengo ambalo mwandishi anakusudia kutimiza. Hivyo basi, hadithi haiwezi kulazimishwa kuwa na wahusika ambao hawabadiliki katika matendo yao. Frow (2014) anaeleza kuwa uthabiti wa wahusika au mhusika huwezi kulazimishwa kwa sababu mhusika hupewa sifa za uhalisia wa binadamu ili kuwasilisha dhamira na maudhui ya hadithi.

3.5 Mshabaha wa Lugha ya Wahusika Wakuu na Lugha ya Hadhira Lengwa katika Hadithi Teule

Iribemwangi (2007) anaeleza kuwa lugha ya wahusika inastahili kusababisha mguso wa kihisia kuliko mguso wa kiakili wa hadhira lengwa. Mguso wa kihisia hutokana na lugha ya wahusika kuwa na mshabaha au kuingiliana na lugha ya hadhira ambayo hadithi inakusudia kulenga. Wahusika wakuu ndio hutawala hadithi nzima. Hivyo basi, utathmini wowote wa wahusika unafaa kuwazingatia wahusika wakuu ipasavyo (Wamitila, 2003). Kwa hivyo, wahusika wakuu ndio watazingatiwa katika uchanganuzi wa mshabaha wa lugha ya wahusika na lugha ya hadhira lengwa. Mshabaha wa lugha ya wahusika na lugha ya hadhira lengwa husaidia katika uwasilishaji wa mandhari, maudhui na dhamira ya hadithi kwa njia sahili. Mshabaha wa lugha ya wahusika na lugha ya hadhira lengwa unabainika kama ifuatavyo katika hadithi fupi teule:

Katika hadithi ya “Siku ya Arobaini” (Mohamed, 1970) Sadiki anasawiriwa kwa lugha ambayo inaingiliana moja kwa moja na mandhari ya Uswahilini. Mandhari ni sura ya mahali katika kazi ya fasihi (Oriedo, 2007). Kwa mfano:

> ...mawimbi yalimpasukia miguuni, na akahisi mbubujiko wa mchanga chini ya nyayo Zake. Upepo wa pwani ulimvumia Sadiki na kumbumburusha. Alifumba macho kwa Raha na akajiona mwepesi kama vile akiogelea... (uk. 25).

Vilevile, Bahati amesawiriwa kwa lugha ambayo inaonyesha mazingira ya Uswahilini. Utamaduni wa Uswahilini unadhihirika kupitia kwa mavazi na desturi ya wanawake wa Uswahilini kujipodoa kwa manukato ya kipwani:

> ...bibie, nakungojea wewe, Sadiki alibabaika mbele ya yule bibi aliyejifunika buibui gubigubi. Jifunue basi nikuone, kimwana...ile harufu ya asumini iliyochanganyika na udi, ilikwisha kumlevya Sadiki... (uk. 26).

Katika hadithi, “Kusoma na Kupenda” (Salim, 1970) Zubeda na Abu wanaelezwa kwa lugha yenye mshabaha na lugha ya jamii yenye wanafunzi. Wanawakilisha namna ambavyo wanafunzi hujihusisha kwa mapenzi ya mapema kabla ya kumaliza masomo yao. Aidha, lugha yao inaingiliana moja kwa moja na umri wao kwa sababu licha ya kuwa wapenzi, mapenzi yao yanadhihirisha utoto kutokana na maongezi yao:

> “Tutaingia matatani Abdu. Rama lazima atatuchongea. Hii ni mara ya tatu,” Zubeda alimkumbusha Abdu na kuzidi kubobojeka. Abdu alimvuta tena Zubeda na kumbusu kwa haraka kwenye shavu lake laini... (uk. 40).

Fagih, (2008) anaeleza kuwa lugha ya wahusika inastahili kuwa na mshabaha na lugha ya hadhira lengwa ili kuhakikisha jamii inaelewa lengo la mwandishi. Katika hadithi ya “Ajuta Majuto ya Mjukuu” (Somba, 1970) mamake Kamene na Wayua anatumia lugha ambayo inaingiliana moja kwa moja na hadhira

iliyolengwa na hadithi husika. Lugha yake inawakilisha jamii ambayo inaongozwa na utamaduni ambao umepitwa na wakati. Utamaduni unaomhini mtoto wa kike nafasi ya kujiendeleza kimaisha, hasa kielimu kwa kumwoza mapema:

> ...mwanangu Kamene, Kitonga ni mtu anayeheshimiwa sana. Ana mali na wake wengi. Mama hakumalizia yaliyokuwamo moyoni mwake...nia yake hasa angefurahi kuona kwamba binti yake ameolewa na mtu wa heshima na mali... (uk. 8).

Wayua amesawiriwa kwa lugha ambayo inaonyesha maneno halisi ambayo msichana anapohisi anadhulumiwa anaweza kusema na kutenda. Hali hii ni kutokana na kulipa kisasi kama njia ya kusuluhisha mgogoro wa kisaikolojia anaopitia wa kutoelewa kwa nini aozwe kwa mzee:

> ...pale pale akaanza kusikitika kwa kukumbuka kwamba amempoteza baba yake maana ile pombe aliyokuwa amempa aliitia sumu... (uk. 11).

Katika hadithi, “Maisha Yalimwendea Kombo” (Isaakwisa, 1970) Ruth amesawiriwa kwa lugha ambayo inaonyesha uhalisia wa fikira ya jamii ya vijana. Kutamauka katika maisha humfanya mwanadamu hasa vijana kufanya uamuzi ambao hauna busara hata kidogo, jambo ambalo husababisha athari kubwa zaidi kama anasa za ulevi:

> ...Ruth akabaki akilia wala asijue la kufanya, akakosa hata mahali pa kulala usiku ule. Mwishowe akaona heri azurure zurure kwenye mabaa labda angebahatika kupata mtu mwenye huruma wa kumsaidia. Alipoingia katika baa moja kwa bahati akaitwa... (uk. 44).

Katika hadithi ya “Mzee Khamis, Leo Wapi?” (Mohamed, 1971) lugha ambayo inatumiwa na Mzee Khamis ni dhihirisho tosha kuwa yeye ni kiwakilishi cha mazingira ya utamaduni wa Uswahilini. Lugha yake

inaingiliana na mazingira ya utamaduni wa Uswahilini kutoka na namna anavyoteua msamiati pamoja na dhana ambazo anarejelea:

> ...Sufuria saba za pilau! Haya ni maulidi ya kunywiwa haluli. Yallahi, sijui watahudhuria wengi? Haidhuru, wananijua mimi... (uk. 7).

Mhusika Kombo katika hadithi, "Malipo Duniani, Hesabu Ahera" (Said, 1971) anakuzwa kwa lugha ambayo inaonyesha hadithi hii inalenga hadhira ya Kiafrika. Jamii ya Kiafrika huwa na mila yenye imani kuwa jambo lolote hasi unalotenda malipo yake huwa ni papa hapa duniani. Kombo anajaliwa kupata mtoto ambaye anamsumbua sana kwa utovu wake wa nidhamu na kisio ni kuwa analipwa kwa kumtaabisha marehemu babake:

> ...watu wengi wanasema huyu si mtoto bali ni malaika aliyeshushwa kuja kumwonyesha Kombo uchungu wa kumtaabisha mzee wake...Subhana anamlipa hapa hapa dunian kwa kumbarikia Miraji. Je, wewe unafikiria vipi? (uk. 14).

Katika hadithi ya "Sina Rafiki" (Wahab, 1977) Hasan na Karama wanasawiriwa kwa lugha ambayo inaonyesha namna halisi ya maisha ya marafiki katika jamii. Aidha, marafiki mara nyingi katika jamii huwa na mtazamo wa kusaidiana lakini kunapoingia dosari kama vile wivu miongoni mwa mmoja wao, mambo hubadilika na kuchukua mkondo mwengine kama vile chuki inayoweza kusababisha mauti:

> ...Alivyokuwa ni fundi, alifahamu kuwa katika mashine kama ile, breki ni kitu muhimu sana. Mikono ilimcheza Hasan. Je athubutu? Nani atayejua?... alitia akitoa... (uk. 2).

Msimulizi katika hadithi "Mke Wangu" (Muhammed, 1977) anatumia lugha inayodhihirisha wazi kuwa inaingiliana na hadhira ambayo mazingira yao ni ya Uswahilini. Utamaduni wa mwanamume kuchaguliwa mke hupatikana

katika jamii ya Waswahili ama wanajamii wanaoishi katika eneo la Pwani. Hivyo basi, lugha ya msimulizi ni ithibati tosha kuwa hadithi fupi teule inalenga hadhira ya Kipwani:

> ...Mke niliyechaguliwa na wazee wangu alikuwa ndiye niliyemwelekeza rohoni mwangu. Aziza nilimteua mwenyewe baina ya wengi niliotajiwa kwa majina nami nikawaweka kando... (uk. 48).

Utathmini wa hadithi fupi teule unadhihirisha kuwa lugha inayotumika na kila mwandishi wa hadithi inalenga hadhira fulani maalumu. Lugha inapoingiliana na utamaduni wa hadhira lengwa hufanikisha dhamira na maudhui ya hadithi kueleweka kwa usahili (Ngara, 1982). Hivyo basi, hadithi fupi teule zinafanikisha lengo kuu kutokana na uteuzi wa lugha inayoingiliana na hadhira lengwa jambo linalofanya hadithi hizi kufikia kiwango cha ubora.

3.6 Kusadikika kwa Wahusika Wakuu na Uwazi wa Sababu za Matendo yao katika Hadithi Teule

Kusadikika kwa wahusika ni uwezo kwa wahusika kutenda au kutendewa mambo mbali mbali ambayo yanaweza kumkumba mwanadamu wa kawaida (Paris, 1997). Wahusika wanastahili kuwa wa kusadikika katika matendo yao na sababu za wanayotenda ziwe wazi na za kuaminika. Kwa mujibu wa Wamitila (2003), kusadikika kwa wahusika hutokana na uhusiano wa wahusika wenyewe kwa wenyewe na sababu ya kutenda mambo wanayoyatenda. Kusadikika kwa wahusika hutokana na uwazi wa matendo yao. Forster (1927) anaeleza kuwa wahusika binadamu ndio hutumika sana kutokana na hoja kuwa ni mambo machache yanayofahamika kuhusu

saikolojia ya wanyama. Kusadikika kwa wahusika na uwazi wa sababu za wanayoyatenda kunadhihirika kama ifuatavyo katika hadithi teule:

Kusadikika kwa wahusika hufanikishwa na matendo ya wahusika kuelezwa kwa ukamilifu ili kujenga dhamira na maudhui ya hadithi (Swain, 2008). Katika hadithi ya "Siku ya Arobaini" (Mohamed, 1970) Sadiki ni mhusika ambaye anasadikika. Uhalisia wake upo wazi kwa sababu anawakilisha tabia halisi ambayo huwa na wanaume wengi katika jamii. Sababu ya kutafuta wanawake wengine licha ya kuwa ameoa imewekwa wazi na hii ni kutokana na ukweli kuwa ni mwenye tamaa kwa wanawake. Anajaribu kuficha uzinzi wake kwa sababu anajua mkewe akitambua kutaibuka mgogoro katika ndoa yake na Bahati:

> "Mume wangu leo una nini?"... "Aa, sina kitu. Hii habari ya madeni inaniharibu akili...njia ya mkato ya kugombana na rafiki ni kumkopesha..." (uk. 24).

Vilevile, Bahati ni mhusika ambaye anaaminika kuwa anaishi katika ulimwengu halisi. Sababu ya kusadikika kwake ni kutokana na maudhui anayoendeleza ya nafasi ya mwanamke katika ndoa. Wakati mwingi wanawake hupata changamoto za ndoa, mojawapo ikiwa mwanamume kuwa na udhaifu wa tamaa kwa wanawake wengine. Ujumbe wa tamaa ya mwanamume humfikia mke wake kupitia kwa marafiki wa mkewe, suala linalodhihirika katika hadithi hii na hivyo kumfanya mhusika bahati kuwa wa kusadikika:

> ...licha ya shoga zake kumzibua masikio. Atasadikije naye hakuona ishara yoyote? Zaidi ya hayo Sadiki alionyesha hajifai kwa mapenzi juu ya mkewe... (uk. 25).

Katika hadithi, "Kusoma na Kupenda" (Salim, 1970) kuaminika kwa wahusika Zubeda na Abdu kunatokana na ukweli kuwa katika jamii suala la mapenzi baina ya wanafunzi wanaosoma lipo. Vijana wanapokua hukumbwa na mabadiliko katika miili yao. Wanaposhindwa kukabiliana na mabadiliko hayo hujipata katika mahusiano ya kimapenzi kabla ya kumaliza masomo. Sababu ya kupendana kwao ni kutokana na mabadiliko ya kimwili ambayo yanaamsha hisia zao za kimapenzi. Aidha, mwalimu mkuu anajitolea ili kuhakikisha tabia ya wanafunzi kuhusiana kimapenzi haiendelei kwa kukashifu mahusiano yoyote yale yanayoibuka:

> ...miongoni mwa mambo ambayo yule *Hitler* hakuyapenda katika shule yake ilikuwa ni mapenzi. Nayo aliyaita 'uchafu'. Aliuwa hapendi... (uk. 40).

Katika jamii za Kiafrika, utamaduni wa wasichana kuozwa mapema ni changamoto ambayo inaendelea hata katika karne hii ya ishirini na moja. Wasichana wanaozwa katika umri mdogo suala ambalo linachangia watoto wa kike kukumbwa na changamoto za dhulma katika jamii. Hivyo basi, wahusika Kamene na Wayua katika hadithi ya "Ajuta Majuto ya Mjukuu" (Somba, 1970) ni wa kusadikika. Changamoto za kuozwa mapema wanazopitia ni uhalisia wa jamii ya sasa. Kamene anaamua kuwatilia sumu babake, Kitonga na wanaoandamana na Kitonga kutokana na maudhiko ya kuozwa kwa lazima. Anachukua hatua hii kama suluhu ya matatizo yanayomkabili:

> Wageni walipoachana na kwenda kiasi cha muda mfupi, yule bwana ambaye angekuwa mume wake Kamene ghafla akaanguka chini, povu na jasho jembamba likaanza kumtoka...kitambo si kirefu baba yake akaanza kuumwa na tumbo... (uk. 10).

Katika hadithi, “Maisha Yalimwendea Kombo” (Isaakwisa, 1970) kusadikika kwa Ruth kunatokana na uhalisia wa jamii ambapo mtu anapofanya mambo bila kutumia busara hujuta kwa kukumbana na ugumu wa maisha. Ruth anaamua kujiingiza katika starehe hasa za ulevi na densi baada ya kuona maisha ya mjini ndiyo yanamfaa. Mhusika huyu anamulika ukweli wa vijana wengi katika jamii ambao maisha huwaendea kombo baada ya kuthamini anasa ambazo huwa na athari hasi. Matendo ya Ruth yanajenga uhalisia katika jamii na hivyo kumfanya mhusika wa kusadikika:

> Ruth aliona maisha ya kukaa kijijini hayakumfaa maana alikuwa ni msichana mwenye elimu na madaraka. Basi akaamua kuhamia mjini na akaanza kujiingiza katika starehe za dansi na kuchapa mtindi... (uk. 38).

Katika hadithi ya “Mzee Khamis, Leo Wapi?” (Mohamed, 1971) kusadikika kwa Mzee Khamis kunatokana na tabia yake ya ulafi na tamaa ambayo pia hubainika miongoni mwa wanajamii mbalimbali. Mazingira ambayo amesawiriwa ni ya Uswahilini na kutokosekana kwake katika kila maulidi hata kama hajapewa mwaliko rasmi kunazidi kumfanya kuwa mhusika wa kusadikika. Filosofia yake kuwa kula ni wajibu inaingiliana na mandhari anayosawiriwa kama ifuatavyo:

> ...kula ni wajibu. Shibe ni shibe tu, kwani tumeletewa nini duniani? Si kula? Ningojee kualikwa, mawe! Kama mimi atanialika nani?... (uk. 7).

Mhusika Kombo ni wa kusadikika katika hadithi, “Malipo Duniani Hesabu Ahera” (Said, 1971). Amesawiriwa kama mhusika mtukutu anayemsumbua babake ambaye ni Mzee Miraji. Malezi ya Kombo yanakuwa ni ya kumsumbua babake. Anapoelekea kukomaa ndipo anaamua kuwacha utukutu hasa baada ya wasia wa mwisho kutoka kwa babake. Anapokuwa na familia anajaaliwa mtoto wa kiume kwa jina Miraji na inatokea kuwa anakuwa mtukutu kupita kiasi. Uhalisia wa wahusika hawa unabainika wazi kutokana na mada ya hadithi kuwa malipo huwa papa hapa duniani na hesabu ni ahera. Wanajamii katika utamaduni wa Kiafrika hunasibisha kutokea kwa hali fulani na historia wanayofahamu kama ilivyo katika hadithi hii na hivyo kufanya wahusika kuwa wa kusadikika:

> ...watu wengi wanasema huyu si mtoto bali ni malaika aliyeshushwa kuja kumwonyesha Kombo uchungu wa kumtaabisha mzee wake... (uk. 14).

Urafiki ni baadhi ya hali ambayo haikosekani katika jamii ambapo watu wanatangamana kila siku. Hasan na Karama ni mojawapo ya wahusika wa kusadikika katika hadithi ya “Sina Rafiki” (Wahab, 1977). Urafiki wao unadhihirika kutokana na hali ambapo wanasaidiana mmoja wao anapotaka msaada. Karama anapotaka kuondoka kidogo anamtegemea Hasan kumuuzia dukani maana ni rafiki yake. Hasan anapokumbwa na changamoto za fedha anamkopa Karama maana ni rafiki yake. Mwingiliano wa marafiki hawa unawapatia uhalisia wa wanajamii ambao wanasadikika:

> ...Usiku ule hasan na Karama walikutana pale pale mbele ya mkahawa wanapokaa siku zote kuzungumza. Baada ya mazungumzo mafupi, Hasan, aliyekuwa na papara ya kuondoka, alikatiza hadithi na kusema, Karama siku hizi hali yangu mbaya sana... (uk. 1).

Utamaduni wa Waswahili huwa maaraufu kwa mwanamume kuchaguliwa mke anapofika umri wa kuoa. Mke wa kuchaguliwa mara nyingi husababisha mgogoro katika ndoa kwa sababu huwa kuna uwezekano mkubwa mwanamke na mwanamume hawajapata kuelewana tabia vizuri. Katika hadithi ya "Mke Wangu" (Muhammed, 1977) Aziza na msimulizi ni wahusika wa kusadikika kwa sababu ni kiwakilishi cha maisha ya ndoa katika utamaduni wa Mswahili. Msimulizi anapendekezewa wanawake kadhaa lakini mwisho anamridhia Aziza. Mgogoro unaibuka kati yao ndani ya ndoa maana wanakinzana katika kuelewa majukumu na tabia za kila mmoja. Aziza anataka mwanamume anayefanya kazi hata kama ni ya kujiajiri naye msimulizi anasubiri kuajiriwa. Vilevile, Aziza ameshikilia imani za kale kama kutotumia mswaki wa kisasa tofauti na msimulizi ambaye anaona imani ya Aziza imepitwa na wakati. Tofauti hizi zao zinasababisha mgogoro katika ndoa kama ifuatavyo:

> ...Nadhani kusoma Kizungu kumekuziba macho usione tofauti yao. Huoni kama yale ni manyoya? Na manyoya yenyewe si ya ng'ombe wala mbuzi? Yasini! Sitotia manyoya ya nguruwe kinywani mwangu... (uk. 54).

Wahusika wakuu katika kila hadithi fupi teule wanatenda au wanatendewa mambo ambayo katika ulimwengu halisi yanaaminika kuwa ya kweli. Hivyo basi, utathmini wa usawiri wa wahusika wakuu kupitia kigezo cha kusadikika kwa wahusika unaashiria kuwa ubora wa hadithi fupi teule pia hutegemea wahusika kuthibitisha uhalisia wa maisha ya mwanadamu (Frow, 2014). Kuzingatiwa kwa kanuni hii kunafanikisha dhamira na maudhui ya hadithi fupi teule kueleweka kwa usahili na hadhira lengwa.

3.7 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia usawiri wa wahusika katika hadithi fupi teule kama mojawapo wa kipengele cha uhakiki wa kimtindo kwa kutumia mihimili ya nadharia ya mtindo iliyoasisiwa na Leech (1969). Uhakiki umezingatia vipengele vifuatavyo: aina ya wahusika, idadi ya wahusika pamoja na jukumu lao katika hadithi fupi teule, uthabiti wa wahusika wakuu, mshabaha wa lugha ya wahusika wakuu na lugha ya hadhira lengwa na kusadikika kwa wahusika wakuu. Mada hizi zimesaidia katika kueleza ubora wa dhana ya wahusika na uhusika wao katika hadithi fupi teule ambazo zilisomwa katika idhaa ya redio ya BBC na hatimaye kuchapishwa katika mikusanyiko; *Mapenzi ni Kikohozi* (1970), *Vituko Duniani* (1970), *Pavumapo palilie* (1971) na *Kinywa Jumba la Maneno* (1977). Sura inayofuata itabainisha maudhui katika hadithi fupi teule ambayo yanajitokeza katika kipindi hiki cha mwamko mpya. Maudhui kama vile; elimu, ndoa, mapenzi na uzinzi, tamaa, nafasi ya mwanamke katika jamii, utabaka, utamaduni, bidii, ukatili, utamaushi, kisasi na dini.

SURA YA NNE

TATHMINI YA MAUDHUI YA HADITHI FUPI TEULE

4.1 Utangulizi

Sura hii inashughulikia maudhui yaliyowasilishwa katika hadithi fupi teule, maudhui ambayo bado yanajitokeza katika kipindi hiki cha mwamko mpya. Wamitila (2003) anaeleza kuwa nadharia ya mtindo iliyoasisiwa na Leech (1969) husaidia kuchanganua vipengele vya fani na maudhui katika kazi ya fasihi. Maudhui yanafaa kuwa na umuhimu wa kuelekeza jamii. Fani ni ufundi wa kisanaa unaojumuisha vipengele kama vile: wahusika, ploti, mandhari na usimulizi (Njogu na Chimerah, 1999). Maudhui ni jumla ya mambo yote yanayoelezwa katika kazi ya fasihi; dhamira ikiwemo kama sehemu ya maudhui (Wamitila, 2003). Dhamira ni kusudio la msanii wa kazi ya fasihi ilhali maudhui ni mawazo, fikira na ujumbe katika kazi ya fasihi (Oriedo, 2007). Maudhui ni ujumbe wa jumla kuhusu matukio, kitu, wahusika au hali ya maisha kama yanavyoelezwa katika kazi ya fasihi (Njogu na Chimerah, 1999). Mhimili wa nadharia ya mtindo unaoshikilia kuwa maudhui ni kipengele muhimu katika utathmini wa ubora wa kazi za fasihi ndio umesaidia katika uteuzi wa maudhui ya hadithi fupi teule. Maudhui yaliyowasilishwa katika hadithi fupi teule yalikuwa na umuhimu maana bado yanawasilishwa katika hadithi fupi za kipindi hiki cha mwamko mpya. Maudhui hayo ni kama vile: elimu, ndoa, mapenzi na uzinzi, tamaa, nafasi ya mwanamke katika jamii, utabaka, utamaduni, bidii, ukatili, utamaushi, kisasi na dini.

4.2 Umuhimu wa Elimu

Kwa mujibu wa Chandra na Sharma (2004), elimu ni mchakato ambao hukuza ufahamu wa mwanadamu na kumfanya mtu muhimu na mwenye maisha bora katika jamii. Umuhimu wa elimu unasisitizwa kama maudhui makuu katika hadithi, "Kusoma na Kupenda" (Salim, 1970). Abdu na Zubeda wanatumwa nyumbani kuwaita wazazi wao kwa sababu mwalimu mkuu anafahamu umuhimu wa elimu. Abdu na Zubeda wanajihusisha katika mapenzi kabla ya kumaliza masomo. Wanajihusisha katika mapenzi ambayo yanaweza kuathiri elimu yao ndiposa mwalimu mkuu anayaita 'uchafu'. Vilevile, mwalimu wa Jografia anajituma katika kuwaelimisha wanafunzi kuhusu bara lao la Afrika ili waelewe mazingira yao.

> ..mwalimu wa Jografia alipokuwa kashughulika na kusomesha ramani ya Afrika iliyotundikwa mbele ya wanafunzi, alikatizwa na karani wa mwalimu mkubwa...karani huyo alimkabidhi kikaratasi, na alipokifungua na kukisoma, mwalimu aliwatupia macho Zubeda na Abdu,...mnatakiwa na mwalimu mkubwa baada ya somo... (uk. 43).

Fullan (2016) anaeleza kuwa mzazi anayewajibika ni yule ambaye anathamini elimu ya mtoto wake kwa sababu elimu ni msingi wa maisha bora ya baadaye. Babake Ruth anafafanuliwa kwa namna inayoonyesha anathamini elimu katika hadithi ya "Maisha Yalimwendea Kombo" (Isaakwisa, 1970). Anashikilia msimamo kwamba elimu ni tegemeo la maisha bora ya baadaye.

> ...baba yake alikuwa na nafasi nzuri hata alioa wake kumi na wawili... hakukosa kumtimizia bintiye mahitaji yote yaliyohusu elimu maana alijua kwamba yeye ndiye atakayewatunza nduguze... (uk. 37).

Elimu inaelezwa kuwa na nafasi ya kujenga maisha bora na hata kupanua uelewa wa mazingira ya kimataifa. Uelewa wa mazingira ya kimataifa

hutokana na mtu anaposafiri ughaibuni kuendeleza elimu yake. Usafiri huo unaweza kumfanikisha mtu kupata elimu ya mazingira ya jamii ya ughaibuni. Katika hadithi, “Malipo Duniani Hesabu Ahera” (Said, 1971), Kombo anafanya bidii katika elimu. Bidii inayomfungulia nafasi ya kusomea udaktari nchini Uingereza na bila shaka anaporudi nchini kwao anafaa wagonjwa wanapougua kwa kufanya huduma za tiba.

> ...Baada ya mwaka mmoja wa kujitahidi, Kombo alifikilia kwa urahisi darasa la nane, na hatimaye aliingia sekondari. Huko alijitahidi...Kombo akapata bahati ya kuchaguliwa kwenda Uingereza kusomea udaktari... (uk. 14).

Katika hadithi ya “Mke Wangu” (Muhammed, 1970), mhusika Aziza amesawiriwa ili kuhamasisha vijana kuwa ingawa wamepata elimu hawastahili kusubiri kuajiriwa. Elimu inastahili kumfanya mtu kufikiria namna ya kujiendeleza kimaisha bali si kukaa na kutegemea wazazi katika mambo ya msingi kama kupewa chakula.

> ...hivyo ndivyo mlivyo, mkisha kusoma hicho Kizungu chenu mnakuwa basi tena, hamfanyi kazi ila ya uboi, mkae mkitumwa...basi huwezi hata kununua mihogo, ukakaa kuichoma hapo chini nje, ukauza... (uk. 51).

Umuhimu wa elimu unasisitizwa katika hadithi fupi teule. Maudhui haya bado yanawasilishwa katika kazi za fasihi za sasa kwa sababu elimu bado ni msingi wa kujenga jamii bora. Elimu husaidia katika kuimarisha kipato cha wanajamii, kuwepo kwa huduma bora za afya na utangamano mzuri wa wanajamii (Behrman na Stacey, 1997). Hivyo basi, maudhui ya elimu yaliyowasilishwa katika hadithi fupi teule zilizosomwa hewani katika idhaa ya redio ya Kiswahili ya BBC bado yana umuhimu mkubwa katika kipindi hiki cha mwamko mpya.

4.3 Changamoto katika Ndoa

Mbiti, (1991) anaeleza ndoa kama makubaliano rasmi yanayofanya mwanamume na mwanamke kuishi pamoja kwa lengo la kuanza familia na kupata watoto. Anaongezea kuwa katika jamii ya Kiafrika mwanaume hujichagulia mwanamke au kuchaguliwa na wazazi au wanafamilia kama vile shangazi. Misingi ya ndoa ni heshima, mapenzi na uaminifu ili kupunguza changamoto katika ndoa. Sadiki amesawiriwa katika hadithi ya "Siku ya Arobaini" (Mohamed, 1970) kama mwanamume mzinzi. Bahati ni mke wa Sadiki na anadokezewa na rafiki zake kuwa mumewe si mwaminifu. Kupitia kwa Sadiki na Bahati, hadithi inakuza maudhui ya ndoa kwa kuonyesha changamoto za ukosefu wa uaminifu na uzinzi katika maisha ya ndoa.

> ...alikuwa mjanja, kwani nyendo zake zote alizokuwa akizienda, mkewe hakusikia angalau mchakato, licha ya shoga zake kumzibua masikio... (uk. 25).

Katika hadithi, "Sina Rafiki" (Wahab, 1977) maudhui ya changamoto katika ndoa yanaelezwa kupitia kwa Bi. Asha na mumewe Karama. Wanaume wanaelimishwa umuhimu wa kutenga muda na kuwa na wakati wa kujipumzisha hasa kwa kuzuru maeneo mbalimbali wakiwa na wake wao. Mapenzi katika ndoa huimarika wakati ambapo wanandoa wanapata muda wa kupumzika na angalau kuzuru sehemu ya burudani ili kujiliwaza pamoja. Hasan anajishughulisha zaidi na kazi ya dukani na kukosa nafasi ya kuwa pamoja na mkewe Bahati. Karama, rafiki ya Hasan anatumia pengo hilo kumshawishi Bi. Asha waende usiku kutazama sinema wakati Hasan hayuko baada ya kupata safari ya kwenda shambani kwake ambako ni mbali na

wanakoishi. Hivyo basi, mume anastahili kutenga muda na kujiburudisha na mke wake ili kujenga uthabiti wa ndoa.

> ...sinema ilimkolea Bi. Asha, ikawa ndio ada, kila Karama anapokwenda shamba, wao hufuatana na kutoka. Mazoea yaliendelea vizuri sana hata Hasan akaweza kumshawishi Bi.Asha amwambie Karama amwache na yu tayari kumwoa... (uk. 3).

Maudhui ya changamoto katika ndoa yanadhihirika katika hadithi ya "Mke Wangu" (Muhammed, 1977). Mwanamke kukulia mashambani si kigezo tosha cha utathmini wa ubora wake katika maisha ya ndoa. Ndoa inahitaji zaidi kuelewana na kuthaminiana. Msimulizi anadhani kwa sababu Aziza amekulia maisha ya mashambani basi ndoa yake haitakua na mgogoro lakini baadaye wanazozana katika ndoa. Wanazozana kwa sababu msimulizi anaongozwa na usasa tofauti na Aziza ambaye anaongozwa na utamaduni. Aziza hawezi kutumia mswaki wa kisasa, kijiti kinamtosha kupiga mswaki. Suala linalosisitizwa ni kuelewana katika ndoa, mume na mke wawajibike kuelewana katika ndoa ili kuzuia mgogoro.

> ...Aziza ni lazima awe mbichi na mfuto katika mambo mengi ya mjini yaliyokuwa sababu za kuharibu ndoa nyingi za wenzangu kwa muda mchache wa makazi yao. Maadam kakulia shamba, Aziza lazima awe hana mambo mambo... (uk. 49).

Ndoa yoyote ile haiwezi kukosa changamoto zake kwa sababu mwanadamu lazima atatofautiana na mwenzake kwa njia yoyote ile. Muhimu zaidi ni watu kuelewana na kujenga mapenzi, heshima na uaminifu katika ndoa. Tathmini ya maudhui ya ndoa katika hadithi fupi teule inaonyesha kuwa maudhui haya yana uzito hata kwa jamii ya sasa kwa sababu yanatuelekeza katika kujenga ndoa bora.

4.4 Athari za Mapenzi na Uzinzi

Mapenzi ni msukumo wa ndani ambao humfanya mtu kumthamini mwengine. Kwa mujibu wa Burke (1999), baadhi ya watu huwa na mapenzi ya ubinafsi na unafiki katika uhusiano wao. Aidha, uzinzi ni wakati ambapo mtu hushiriki matendo ya kisherati. Lewis (2008) anaeleza kuwa mwanamke anapogundua kwamba mumewe anashiriki matendo ya kisherati hafai kumkashifu ila aangalie ni jambo gani kama mwanamke halitimizi kwa mumewe. Bahati katika hadithi, "Siku ya Arobaini" (Mohamed, 1970) anadhihirisha mapenzi ya dhati kwa mume wake. Licha ya kuwa na fununu za uzinzi wa mumewe, Bahati hamwonyeshi Sadiki dharau. Anawajibika kumwandalia chakula kizuri. Sadiki anamsaliti Bahati kutokana na tamaa kwa wanawake wengine kwa sababu anafurahia anapopokea barua kutoka kwa mpenzi asiyemjua. Sadiki anakwenda kuisoma kwa mara nyengine chooni ili asionekane na mke wake wa ndoa Bahati.

> ...Bahati mkewe Sadiki, alikuwa kashughulika akaingia jikoni na kutoka huku anaitandika meza ya kulia kwa vinono vya kutoa mate. Kisha akamkaribisha mumewe... (uk. 23).
> ...Kutia chakula mdomoni ni mazoea tu, kama si hivyo angalitia pengine. Akili yake yote aliiacha kwa ile barua. Ilikuwa ndani ya roho yake...mkewe alipomwuliza nini, alijidai kuondoka na kwenda chooni. Chooni aliifichua tena ile barua na kuirejea...(uk.24).

Kwa mujibu wa Fincham na Cui (2011), vijana wanapokua hujipata wakikabiliwa na msukumo wa hisia za mapenzi na kujiingiza katika uhusiano wa mapema. Athari ya mapenzi inabainika katika hadithi ya "Kusoma na Kupenda" (Salim, 1970). Zubeda na Abdu wanashindwa kustahamili hisia za mapenzi hadi kupigana busu shuleni. Wanapatikana na kusemwa na Rama,

mlinzi wa shule kwa mwalimu mkuu. Abdu na Zubeda wanaonywa na kutengana kwa muda lakini hisia za mapenzi zinawazidia na kurudiana tena.

> ...Zubeda na Abdu walirejeana tena kwa kasi zaidi, na sasa mapenzi yalikuwa ya moto moto. Naam, mambo hayakukosa kujulikana na haukupita muda kabla Zubeda na Abdu kuitwa tena... (uk. 43).

Ben katika hadithi, "Maisha Yalimwendea Kombo" (Isaakwisa, 1970) anadhihirisha mapenzi ya kweli kwa Ruth ambaye hathamini penzi la Ben. Ben anafanya jukumu la kusafiri kutoka kijijini hadi mjini alikohamia Ruth mpenzi wake, ili amjulie hali na wapange mipango ya ndoa.

> ...Ben alimwandikia Ruth barua ya kumwarifu kwamba angekuwa mgeni wake siku ya Jumamosi. Ruth alipoipokea ile barua, aliifungua na kabla ya kumaliza kuisoma alitupa macho mwisho wa barua, alipoona jina la Ben, aliichanachana... (uk. 38).

Hadithi ya "Sina Rafiki" (Wahab, 1970) inawasilisha maudhui ya athari ya mapenzi. Bi. Asha analia baada ya mumewe Hasan kufariki kwa sababu anahisi uchungu. Mumewe alikuwa mwenye bidii katika maisha, anawacha pesa ambazo licha ya kuzitafuta kwa bidii hajafaidika nazo. Bi. Asha anadhihirisha mapenzi kwa mumewe kwa sababu wanawake wengine wanaweza kufurahi baada ya mume kufariki ili wafaidi mali aliyowacha.

> ...Mapesa yote haya! Masikini mume wangu, hata hajawahi kuzifaidi! Hapo alijipweteka chini, machozi yakimtiririka. Hakuwa na haja ya kuzihesabu, kwani marehemu alikwisha mwambia kuwa akiba yake ilikuwa shilingi sitini elfu... (uk. 7).

Msimulizi anachaguliwa wanawake wengi wa kuoa na wazazi wake lakini moyo wake unamridhia Aziza katika hadithi, "Mke Wangu" (Muhammed, 1970). Mapenzi yake kwa Aziza yanazidi kubainika kwa sababu lengo la msimulizi ni kumtunza mkewe hadi avutie zaidi.

> ...Mke niliyechaguliwa na wazee wangu alikuwa ndiye niliyemwelekeza rohoni mwangu. Aziza nilimteua mwenyewe baina ya wengi niliotajiwa kwa majina nami nikawaweka kando...nilitaka mke mtoto mbichi nimvumbike mwenyewe mpaka aive. Na Aziza nilimwelekeza atakuwa hivyo... (uk. 48).

Mapenzi ni mojawapo ya maudhui ambayo ni nadra kukosekana katika kazi za fasihi kwa sababu mapenzi ni sehemu ya maisha ya mwanadamu. Tofauti na Lewis (2008), tahakiki ya hadithi ya "Siku ya Arobaini" (Mohamed, 1970) inathibitisha kuwa suala la uzinzi ni tabia ya mtu tu. Mwanamke anaweza kuwa anawajibika na anampenda mumewe lakini mumewe akawa na hulka ya uzinzi. Hadithi fupi teule ziliwasilisha maudhui ambayo katika kipindi hiki cha mwamko mpya bado yanadhihirika. Hivyo basi, ubora wa hadithi fupi unatokana na hadithi kulenga maudhui yenye umuhimu kwa kizazi cha wakati huo, kizazi cha sasa na kizazi cha baadaye.

4.5 Athari za Tamaa

Tamaa ni hamu kubwa inayomsukuma mtu kutumia juhudi zozote zile kupata kitu (Green, 2011). Sadiki ni mhusika mwenye tamaa kupita kiasi kwa wanawake wengine licha ya kuwa na mke wake halali Bahati. Sadiki katika hadithi, "Siku ya Arobaini" (Mohamed, 1970) anakua mwenye tamaa kwa wanawake wengine hadi kuishia kuwa mzinzi.

> ...Sadiki alikuwa ni kijana anayependa sana wanawake. Alikuwa na njaa isiyo na mipaka, na ijapokuwa alikuwa na mke, hakutosheka na mmoja wala mia moja... (uk. 25).

Maudhui ya tamaa yanaendelezwa katika hadithi ya "Maisha Yalimwendea Kombo" (Isaakwisa, 1970). Ruth anaingiwa na tamaa ya kutoka kijijini na

kwenda mjini ili akafanye starehe za densi na pombe. Tamaa yake ya anasa hii inamfanya kupoteza pesa anazopata badala ya kujijenga kiuchumi.

> ...Basi akaamua kuhamia mjini na akaanza kujiingiza katika starehe kama dansi na kuchapa mtindi...mambo haya yote ya starehe yalimfanya Ruth kusahau kabisa mipango ya kugawanya mali... (uk. 38).

Mzee Khamis anakua na tabia ya ulafi kutokana na tamaa yake ya kuhudhuria sherehe mbalimbali bila hata mwaliko maalumu. Katika hadithi, "Mzee Khamis, Leo Wapi?" (Said, 1971), Mzee Khamis ananusurika kifo kwa sababu ya tamaa yake inayomfanya kuogelea ili asikose wali wa Tumbatu anapokosa mtumbwi wa kumvusha baharini.

> ...Bahati mbaya hapakuwa na mtumbwi wa kumvusha mpaka Tumbatu...Wasiwasi wa kukosa wali ukamjaa. Akakumbuka taabu yake ya mwendo. Moyo ukamshawishi... pale tu, si mbali ati. Haya jitose...alikuwa na tamaa ya kufuzu... (uk. 6).

Tamaa ni ujumbe mkuu unaofafanuliwa katika hadithi ya "Sina Rafiki" (Wahab, 1977). Athari ya tamaa inabainika kupitia mhusika Hasan ambaye anamuua rafiki yake Karama ili amiliki mali ya Karama. Aidha, Hasan anahukumiwa kufungwa maisha gerezani baada ya idara ya polisi ya upelelezi kugundua kuwa Hasan ndiye mhusika mkuu katika kifo cha Karama na baadaye pia anamuua mke wa Karama, Bi. Asha.

> ...Alimkuta Bi. Asha amejitupa chini yumo katika kutanga, akaanza kumrushia mateke, ondoka mwizi we! Niambie pesa umezificha wapi, ziko wapi? Bi.Asha alifunua jicho moja, akajikaza na kusema, kumbe kweli umemuua rafiki yako kwa pesa... (uk. 11).

Zigon (2008) anaeleza kuwa athari ya tamaa husababisha wanadamu kutenda matendo ya ajabu, kikatili na kishetani. Ubora wa maudhui haya ni kuwa

yanaelekeza wanajamii kwa sababu mojawapo wa upungufu wa baadhi ya wanajamii ni kuwa na tamaa. Hivyo basi, hadithi fupi teule ziliwasilisha maudhui yenye ubora maana bado ni maudhui faafu katika jamii ya sasa.

4.6 Nafasi ya Mwanamke katika Jamii

Kwa mujibu wa UNESCO (2017), mwanamke bado anapewa nafasi duni katika jamii ingawa muda unavyozidi kusonga ndivyo anazidi kujikwamua katika kupewa nafasi duni. Katika hadithi, "Siku ya Arobaini" (Mohamed, 1970) mwanamke anachukuliwa kama kivutio na chombo cha kumstarehesha mwanamume. Sadiki anapokea barua iliyoandikwa na mwanamke anayetaka waonane ufuoni wa *People's Beach*. Anadhani barua hiyo imetoka kwa jirani yake Saida.

> ...Sadiki aliegemea mlango wa kwake kuvuta fikira. Isijekuwa Saida, yule kisura anayemkuta dirishani siku zote aendapo kazini. Na ikiwa ndiye yule basi Sadiki aliona kaokota hazina ya uzuri... (uk. 23).

Katika hadithi ya "Ajuta Majuto ya Mjukuu" (Somba, 1970) mwanamke anaelezwa kama anayethamini mali badala ya maisha ya wanawe. Mamake Kamene anajaribu kumshawishi bintiye Kamene akubali kuolewa na mzee Kitonga kwa sababu ingawa Kitonga ni mzee ana mali.

> ...mara akakumbuka maneno aliyoambiwa na mama yake siku moja, mwanangu Kamene, Kitonga ni mtu anayeheshimiwa sana. Ana mali na wake wengi... (uk. 8).

Nafasi ya mwanamke katika jamii inadhihirisha kuwa mwanamke ni mpenda anasa. Ruth katika hadithi, "Maisha Yalimwendea Kombo" (Isaakwisa, 1970)

anapata ajali akiwa mlevi huku ameandamana na John ambaye licha ya kuwa na mke na watoto anafanya starehe na Ruth.

> ...Ruth hakujali chochote bali alizidi kuponda ile rasilimali pamoja na John hata nyumbani kwao ikawa vigumu kufika japokuwa alikuwa na gari. Siku moja John na Ruth walitoka dansini, walikuwa wameuchapa mtindi kweli kweli. Ruth alikuwa akiendesha gari yake. Bahati mbaya...gari ikagonga ukuta wa nyumba ya Bwana Maina. Gari hiyo ilipondeka pondeka vibaya... (uk. 40).

Ijapokuwa inasemekana kuwa mwanamke amepewa nafasi duni katika jamii, baadhi ya sababu za kudunishwa kwa mwanamke zinasababishwa na wanawake wengine au mwanamke mwenyewe. Tathmini ya hadithi fupi teule inaonyesha kuwa uamuzi mwingine wa kudunishwa kwa wanawake umetokana na matendo yao wenyewe kama vile tamaa ya pesa na anasa. Vilevile, jamii inaendelea kumtetea mwanamke pamoja wa watoto wa kike jambo ambalo limefanya jamii kuwasahau wanaume na watoto wa kiume. Tofauti na wakati huo ambapo hadithi hizi ziliwasilishwa, nafasi ya mwanamke katika jamii ya sasa imeimarika kwa asilimia kubwa (GaaG, 2014).

4.7 Athari ya Utabaka

Bottero (2005) anaeleza utabaka kama mfumo wa kuwagawanya watu kwa misingi ya tofauti za uwezo wa kumiliki mali na kutawala njia za uzalishaji mali. Athari ya utabaka inajitokeza katika hadithi ya “Kusoma na Kupenda” (salim, 1970). Abdu anaonekana hapo awali akiwa kwao Mombasa akisomea kwenye shule yenye hadhi ya juu inayowakilisha watu wa tabaka la juu kuliko shule anayojiunga nayo hapo Unguja inayowakilisha watu wa tabaka la chini.

> ...kwa hakika shule ile haikuwa nadhifu kama ile aliyokuwa ametoka. Deski zake zilikuwa kuukuuu na kuta zake chafu kidogo... (uk. 41).

Maudhui ya athari ya utabaka yanaendelezwa katika hadithi, "Mzee Khamis, Leo Wapi?" (Mohamed, 1971). Mzee Khamis anawakilisha watu wa tabaka la chini. Anaposikia mahali kuna sherehe, afadhali atembee mwendo mrefu lakini awahi wali. Vilevile, Mzee khamis hana uwezo wa kuabiri gari ili kufika aendapo. Tofauti na Mzee Khamis, watu wa tabaka la juu wanamiliki magari na wengine wana uwezo wa kulipa nauli.

> ...Gari zilianza kumpita na yeye alijitahidi kuzisimamisha zimsaidie. Jawabu alizopata kutokana na watu waliojaa humo pomoni wakienda maulidini ni Mzee Khamis, Leo wapi?... (uk.10).

Athari ya utabaka inabainika katika hadithi ya "Mke wangu" (Muhammed, 1977). Aziza anakashifu tabia ya watu wa tabaka la juu kujiona bora, Aziza ni mtetezi wa watu wa tabaka la chini kwa sababu anamwita bazazi wa madafu apande juu ghorofani wanakokaa. Msimulizi ambaye ametoka tabaka la juu anaonekana kutoridhika na hatua ya Aziza kumwita bazazi wa madafu kuingia kwao.

> ...Aziza hakukasiri. Hapo hapo alikwenda mbio mpaka dirishani, akaita kwa kelele, Bwana mwenye madafu! Tuletee madafu manne huku juu! Nilishituka ikanitoka, Aziza wee! Unamwita aje huku juu?...sasa ulikuwa hutaki aje huku juu? Nilimsikia akisema kabwela yule, aliendelea haijuzu kuingia nyumbani kwa kabaila... (uk. 55).

Mzee Miraji anawakilisha watu wa tabaka la chini katika hadithi, "Malipo Duniani Hesabu Ahera" (Said, 1971). Nyumba ya Mzee Miraji inadhihirisha kuwa ametoka katika tabaka la chini kutokana na mabati anayoezeka.

Anawakilisha hali ngumu ya maisha ambayo watu wa tabaka la chini hupitia, hasa mazingira wanayoishi.

> ...nyumba yao ilikuwa ya rangi ya manjano iliyoezekwa kwa madebe ya samli waliyoyanunua kwa mwenye madebe mabovu...Ilikuwa na madirisha mapana makubwa manne lakini hayakufaulu kuleta mwangaza wa kutosha... (uk. 12).

Tathmini ya maudhui ya athari ya utabaka inadhihirisha kuwa suala la utabaka bado ni changamoto kubwa sana hata kwa jamii ya sasa. Utabaka ndio husababisha kuwepo kwa siasa mbaya na migogoro ya kila mara miongoni mwa wananchi. Kutokana na haya, maudhui haya bado ni faafu kwa kuelekeza jamii ya sasa ili kujenga jamii yenye umoja na kuboresha uchumi wa wananchi na jamii kwa jumla.

4.8 Mila na Desturi katika Utamaduni

Mila ni mambo yanayofanywa na jamii fulani yanayolingana na asili na mazingira ya jamii hiyo. Kalman (2009) anaeleza utamaduni kama namna wanajamii wanavyoishi, lugha wanayoongea, vyakula wanavyokula, nguo wanazovaa, hadithi wanazosimulia na namna wanavyosherekea sherehe mbalimbali. Utamaduni uliopitwa na wakati ambao unaruhusu ndoa ya mapema na lazima miongoni mwa wasichana wadogo unakashifiwa katika hadithi, “Ajuta Majuto ya Mjukuu” (Somba, 1970). Wazazi wa Kamene wanahifadhi mila na desturi zao wakati wanamwozesha mtoto wao Kamene kwa Kitonga, mzee mwenye wake wawili.

> ...mwanangu una bahati sana, una baba mwenye hekima...anayekutafutia mtu mwenye nafasi akuoe maana nawajua mababa wengi wasiojishughulisha juu ya mambo ya ndoa za binti zao hata kidogo. Huwaacha wasichana wao kutafuta mchumba yeyote yule anayempenda...sidhani kama ni jambo zuri mwanangu; hasa katika kuhifadhi mila na desturi zetu... (uk. 9).

Maudhui ya mila na desturi katika utamaduni yanajitokeza katika hadithi ya "Malipo Duniani Hesabu Ahera" (Said, 1971). Utamaduni wa Mwafrika huhusisha imani kuwa maovu ambayo mtu huwatendea wengine huwa ni lazima mtu alipwe papa hapa duniani. Imani hii inadhihirika katika methali, "malipo ni duniani ahera kwenda hesabu" (Wamitila, 2001). Methali hii imetumika kuipa hadithi kichwa chake. Katika kukua kwa Kombo, anamsumbua babake Mzee Miraji kwa utukutu wake na baadaye anapokua na kuoa anajaliwa mtoto kwa jina Miraji. Miraji, anaibuka kuwa mtukutu zaidi ya Kombo alivyokuwa akiwa mdogo. Utamaduni wa Mwafrika unajitokeza maana wanajamii wanaamini Kombo anapata malipo yake papa hapa duniani. Malipo ya usumbufu na utukutu aliokua nao.

> ...Kombo alipata mtoto mwanamume. akampa jina la marehemu babaye, yaani Miraji. Vitendo vya Miraji alipokuwa mkubwa havielezeki kwa mdomo; mradi mpaka uvione kwa macho...wengine wanasema ati Kombo amekosa radhi za mzee wake, na mwenyewe Subhana anamlipa hapa hapa duniani kwa kumbarikia Miraji... (uk. 14).

Katika hadithi, "Mke Wangu" (Muhammed, 1977), maudhui ya utamaduni wa jamii ya Waswahili wa eneo la pwani yanaelezwa. Utamaduni ambao unaeleza mila na desturi za jamii ya Waswahili katika suala la ndoa. Mila na desturi ambazo zinawaruhusu wazazi kuwa na jukumu la kumchagulia mwanamume mke.

> ...mke niliyechaguliwa na wazee wangu alikuwa ndiye niliyemwelekeza rohoni mwangu... (uk. 48).

Ubora wa maudhui ya mila na desturi katika utamaduni wa wanajamii unatokana na ukweli kuwa Mwafrika hawezi kutenganishwa na utamaduni wake hata kidogo. Aidha, maudhui haya yanafaa kwa sababu yalielimisha jamii ya wakati huo kuhusu tamaduni mbalimbali za Kiafrika, bado yanatuelimisha na yataelimisha vizazi vijavyo. Wamitila (2003) anaeleza kuwa mojawapo ya jukumu la fasihi ni kuhifadhi mila na desturi za utamaduni wa wanajamii.

4.9 Umuhimu wa Bidii

Bidii ni hali ya kufanya jambo kwa juhudi ili kupata ufanisi (Crews, 2004). Bahati katika hadithi ya "Siku ya Arobaini" (Mohamed, 1970) anafanya juhudi za kumpeleleza mumewe Sadiki ili kupata ukweli wa tabia ya Sadiki ya uzinzi. Bidii inadhihirika kupitia kwa Bahati anapojituma kuandika barua na kuteua maneno barabara. Maneno yanayomkutanisha na Sadiki katika ufuo wa *People's Beach*. Sadiki anaingia mtegoni maana anajipeleka katika ufuo wa *People's Beach* kama ujumbe wa barua unavyokusudia. Kufika kwa Sadiki inakuwa ni hakikisho kwa Bahati kuwa Sadiki ni mzinzi na anafanikiwa kujua ukweli wa tabia yake kutokana na bidii yake ya upelelezi kupitia kwa barua.

> Ni mapenzi peke yake yaliyonifanya nikuombe tuonane hapo *People's Beach*, mnamo saa mbili za usiku kesho... (uk. 23).

Umuhimu wa bidii unabainika katika hadithi, "Kusoma na Kupenda" (Salim, 1970). Abdu anafanya jitihada katika masomo yake na kufanikiwa kupata alama nzuri pamoja na kuwa mwanafunzi bora darasani. Bidii ya Abdu

inamwezesha kumshinda Zubeda ambaye hapo awali alikuwa akiongoza darasani.

> Zubeda aligundua kuwa Abdu alikuwa kijana mwenye fahamu nzuri na mwepesi wa kuelewa. Siku zilipita na mtihani ulipokaribia alihofu kuwa huenda Abdu akamnyang'anya cheo chake alichokuwa nacho katika darasa lile. Mtihani ulipofanywa, naam, kweli Abu alizikongoa maki nyingi kuwapita wote mle darasani na hata kumfyeka Zubeda pia. (uk. 42).

Mhusika Joyce anafanya kazi kwa bidii ili kutekeleza majukumu yake kama kijakazi katika hadithi ya "Maisha Yalimwendea Kombo" (Isaakwisa, 1970). Ruth anakosa kumshughulikia mchumba wake Ben anayekuja kumtembelea na kufanya uamuzi wa kwenda kukesha vilabuni. Joyce anajituma kwa kumpikia Ben na kumwonyesha mahali pa kulala.

> Ruth hakujali...Joyce akaenda jikoni na kushughulika kupika chakula cha Ben. Baada ya chakula, Joyce akamwonyesha Ben mahali pa kulala, wakaagana. (uk. 40).

Bidii inabainika kutokana na juhudi alizonazo Mzee Khamis za kuwahi wali. Mzee Khamis anajikakamua kutembea mwendo mrefu ili awahi wali katika hadithi, "Mzee Khamis, Leo Wapi?"(Mohamed, 1971). Anafikia uamuzi wa kutembea baada ya kukosa nauli na kama ilivyo desturi kwake lazima afanye bidii afike kunakoliwa wali.

> Maulidi mengine makubwa yalikuwa Kisiwa cha Tumbatu. Ilivyokuwa pesa za kupandia gari hana, Mzee Khamis aliona bora aamke asubuhi na mapema aanze kuutwanga. Njiani jamaa walipomwona hawakuacha kucheka. (uk. 10).

Mhusika Kombo anafanikisha maudhui ya bidii katika hadithi ya "Malipo Duniani Hesabu Ahera" (Said, 1971). Anafanya bidii katika masomo yake na

kupita vyema. Ufanisi wake ni kuwa anapata ufadhili wa kwenda Uingereza kusomea udaktari.

> Baada ya mwaka mmoja wa kujitahidi, Kombo alifika kwa urahisi darasa la nane, na hatimaye aliingia sekondari. Huko alijitahidi kikwelikweli naye akawa mwanafunzi wa kupigiwa mfano...anasoma kwa bidii na huku anamwangalia mama yake na Fatuma ambaye kwa wakati huo alikuwa amekwisha olewa. Kombo akapata bahati ya kuchaguliwa kwenda Uingereza kusomea udaktari. (uk. 14).

Umuhimu wa bidii unasisitizwa katika hadithi, "Mke Wangu" (Muhammed, 1977). Aziza anamkasirikia mumewe na hafurahishwi na ndoa yao kwa sababu mumewe anakosa kufanya bidii ya kufanya kazi hata ya kujiajiri. Msimulizi anaamini anastahili kuajiriwa kwa sababu amesoma tofauti na Aziza anayeamini mtu anaweza kujiajiri mwenyewe kwa kufanya kilimo au kuchoma mihogo akauza. Aziza anafurahishwa na bidii ya bazazi wa madafu na kusema anatamani angeolewa na mume kama bazazi wa madafu maana ana bidii.

> Huyu ni mwanamume, hafikiri kukaa akachana nywele, akatembee; hana nafasi ya upuzi huo. Yeye daima anafikiri kazi tu, maana kazi ndiyo maisha bora...huyu- au mtu kama huyu- ndiye mume wangu kifu yangu. Wewe, bwana, tumekaa kwa kuwa umenioa tu, lakini si mume wangu... (uk. 57).

Kuendelea kwa mtu au jamii hutokana na juhudi za kujituma kwa hali na mali. Hivyo basi, hadithi fupi teule zinasisitiza umuhimu wa bidii; suala ambalo lina uzito mkubwa katika kuchangia maendeleo ya jamii. Ubora wa maudhui haya ndio ulizifanya hadithi kusomwa hewani katika idhaa ya redio na hatimaye kuchapishwa kwa sababu maudhui bado yanatufaa katika kipindi hiki cha mwamko mpya.

4.10 Ukatili katika Jamii

Kwa mujibu wa Hulsey na Frost (2004), ukatili ni matendo maovu ambayo huwa katika jamii na hivyo kusababisha kuwepo kwa idara za usalama na sheria. Maudhui ya ukatili yanabainika katika hadithi ya "Ajuta Majuto ya Mjukuu" (Somba, 1970). Wayua anavamiwa na watu wenye nguvu wanapokuwa mtoni na dadake Kamene. Anashikwa kwa lazima na kubebwa kuelekea kwa Kyalo anakoenda kuolewa kama mke wa nne wa mzee Kyalo. Wayua anafanyiwa ukatili wa kulazimishwa katika ndoa licha ya kuwa bado ni msichana ambaye hajafikia umri wa kuolewa.

> ...alijiangusha chini lakini wale watu wakaanza kumburura kwa nguvu. Kwa kadiri alivyokuwa akijigaragaza chini na kupiga piga mateke huku akiwakwaruza wale watu kwa kucha za mikono yake ndivyo wale watu walivyozidi kumshika kwa nguvu na kwenda naye. (uk. 6).

Dereva wa teksi katika hadithi, "Maisha Yalimwendea Kombo" (Isaakwisa, 1970) anaendeleza maudhui ya ukatili. Ruth anapokutana na dereva wa teksi Dar es Salaam anamwamini na kumpenda kama mpenzi wake. Ruth anamweleza kiwango chake cha fedha na nia yake ya kununua vyombo vya nyumbani. Anafanikiwa kununua vyombo lakini anapokuwa kazini dereva wa teksi anamwibia kila kitu licha ya kuwa wanaishi wote. Dereva wa teksi ni katili kwa sababu anamwibia Ruth ambaye ni mpenzi wake. Anamwibia kila kitu ikiwemo nguo zake.

> ...akakusanya kila kitu hata sanduku la Ruth, akabana mlango, huyoo! Akaenda zake. Akawaambia majirani wamweleze Ruth kwamba alikuwa amefukuzwa pale kwa sababu ya kutolipa kodi ya nyumba... (uk. 43).

Ukatili unajitokeza katika hadithi ya “Sina Rafiki” (Wahab, 1977). Hasan anahusika katika kifo cha Karama licha ya kuwa Karama ni rafiki yake. Anamuua ili aweze kumiliki pesa za Karama. Vilevile, Hasan anapandwa na hamaki na kumpiga Bi. Asha mateke baada ya kukosa pesa ambazo anadhani Bi.Asha amewachiwa na mumewe, marehemu Karama. Anampiga Bi. Asha bila huruma yoyote ingawa Bi. Asha anaugua hadi kumuua.

> Alimkuta Bi. Asha amejitupa chini yumo katika kutanga, akaanza kumrushia mateke, ondoka mwizi we! Niambie pesa umezificha wapi, ziko wapi? (uk. 11).

Jukumu kubwa la maudhui yanayoelezwa katika hadithi fupi teule ni kukashifu matendo ya kikatili katika jamii. Maudhui haya yana umuhimu wa kukuza jamii bora yenye utu. Ubora wa maudhui haya ndio unafanikisha ubora wa hadithi fupi teule.

4.11 Athari ya Utamaushi

Beck na Alford (2009) wanaeleza utamaushi kama ukosefu wa kuwa na matumaini. Utamaushi unajitokeza kupitia kwa mhusika Abdu katika hadithi, “Kusoma na Kupenda” (Salim, 1970). Abdu anachukua hatua ya kuacha shule baada ya kupatikana na kosa la kuchumbiana na Zubeda wakiwa shuleni. Kanuni za shule zinapinga wanafunzi kujihusisha na mapenzi. Hii ndiyo sababu inamfanya mwalimu mkuu kuwatuma nyumbani wanafunzi wanaokiuka sheria za shule.

> ...Abdu alimwomba Zubeda amfikishie barua yake ya kuacha shule pamoja na vitabu kwa mwalimu mkubwa kwani yeye alikuwa anarejea kwao Mombasa pamoja na wazee wake na kwa hivyo hapakuwa na haja tena ya kumpeleka mzee wake... (uk.44).

Ben anatamauka na kuamua kuvunja uhusiano wake na Ruth katika hadithi ya "Ajuta Majuto ya Mjukuu" (Somba, 1970). Ben anasafiri kutoka kijijini hadi mjini ili kumtembelea mchumba wake Ruth ndiposa wapange mambo ya ndoa yao. Aidha, Ruth anampuuza Ben na kwenda kufanya starehe za dansi usiku kucha na John. Anasusia kurudi kwake kwa siku mbili hadi Ben anapokosa matumaini na kuamua kuvunja mapenzi yao yanayoyumbayumba.

> ...Ruth hakurudi nyumbani. Baada ya dansi alikata shauri kwenda kulala kwa John mpaka chee! Na siku ya pili yote akashinda kule kule. Bila kusita, Ben akaona heri arejee nyumbani...akaondoka bila kuacha taarifa yoyote... (uk. 40).

Utamaushi ni mojawapo ya changamoto ambazo huwakabili wanajamii na kuwasababishia maisha ya huzuni, upweke na matatizo mengine ya kisaikolojia (WHO, 2020). Kutokana na ukweli huu, maudhui haya ni muhimu katika kuelekeza wanajamii ili kupunguza athari za kutamauka ambazo wakati mwengine husababisha mauti.

4.12 Athari za Kisasi

Abuhaimed (2019) anaeleza kuwa kisasi husababisha watu kutekeleza mauti. Athari ya kisasi inadhihirika katika hadithi, "Ajuta Majuto ya Mjukuu" (Somba, 1970). Kamene anaamua kuweka sumu kwa pombe na kumuua babake, Kitonga na wageni wanaoandamana na Kitonga. Mahsusi ya Kamene kuwaua ni kutokana na kusitisha ndoa ya lazima anayopangiwa ili aolewe na Kitonga ndiposa anaamua kuwalipa kwa kisasi cha kuwaua.

> Ya nini Kamene kwenda kumua baba yake na yule mchumba wake. Laiti angalikataa katu katu, asingalilazimishwa... (uk. 11).

Vilevile, athari ya kisasi inaelezwa katika hadithi ya “Sina Rafiki” (Wahab, 1977). Hasan anafanya uamuzi wa kumuua rafiki yake Karama lengo lake ikiwa arithi mali ya Karama hasa baada ya kumuoa mke wa Karama Bi. Asha. Tamaa inamtawala na anaamua atasubiri Bi. Asha augue maradhi ambayo humtatiza hasa msimu wa joto. Anasusia kumletea Bi. Asha dawa na maradhi yanapomzidi Bi. Asha anaamua kutafuta pesa katika madebe. Anapogundua Bi. Asha ashatumia pesa alizotarajia kupata, analipiza kisasi kwa kumpiga mateke licha ya kuwa Bi. Asha anaugua. Hatimaye Hasan anamuua Bi. Asha.

> Kumbe kweli umemuua rafiki yako kwa pesa, lo! na sasa unataka kuniua mimi. Rafiki gani? Sina rafiki mimi! Niambie pesa umezipeleka wapi! Huzipati ng’o! Habithi mkubwa we! Hapo Hasan alimuongeza mateke... (uk. 11).

Tathmini ya maudhui ya athari ya kisasi inaonyesha kuwa maudhui haya bado yana uzito katika kipindi hiki cha mwamko mpya kwa sababu kisasi bado ni mojawapo ya changamoto inayokumba wanajamii. Kutokana na hoja hii, hadithi fupi teule ziliwasilisha maudhui yenye uzito na kuzifanya kuwa na ubora wa kusomwa hewani katika idhaa ya redio ya BBC.

4.13 Nafasi ya Dini katika Jamii

Fasihi hutumiwa kama nyenzo ya kueleza dini ya wanajamii kwa sababu dini ni mojawapo ya sehemu ya utamaduni wa wanajamii (Detweiler na Jasper, 2000). Hadithi ya “Mzee Khamis, Leo Wapi?” (Mohamed, 1971) inaendeleza maudhui ya dini. Imani ya dini ya Islamu inaelezwa kupitia baadhi ya sherehe za dini kama vile maulidi. Sherehe ambazo hutokea katika kila mwaka. Mzee

Khamis anajulikana na wengi kwa sababu hakosi katika sherehe za maulidi ambako huenda kuwahi wali.

> ...Maulidi hayo safari hii yalikuwa kwa Bin Barak...ilipopigwa Bismillahi yeye alikuwa ameshaifuta robo ya sinia... (uk. 8).

Bi. Asha anaendeleza maudhui ya dini katika hadithi, "Sina Rafiki" (Wahab, 1977). Imani ya dini ya Kiislamu inafafanuliwa kupitia kwa Bi. Asha baada ya kifo cha mume wake Karama. Katika dini ya Islamu, mwanamke anastahili kumwomboleza mume wake kwa siku arobaini.

> "...Baada ya kumalizika arobaini, Bi. Asha aliona bora apange vitu vya mumewe marehemu. Lilikuwepo sanduku kubwa lililochukua upana wa nyumba..." (uk. 7).

Nafasi ya dini imedhihirika na kuelezwa kutokana na hadithi fupi hizi teule. Ubora wa hadithi fupi hizi unatokana na hadithi kuwasilisha maudhui ambayo bado yana uzito hata katika kizazi cha sasa na kizazi cha baadaye. Dini ni sehemu kuu ya maisha ya jamii yoyote ile na kuelewa dini ya wanajamii ni kuelewa utamaduni wa wanajamii. Maudhui kama haya ndiyo yalifanya hadithi fupi hizi kufikia kiwango cha ubora wa kusomwa hewani katika idhaa ya redio ya Kiswahili ya BBC.

4.14 Hitimisho

Sura hii imeangazia maudhui ya hadithi fupi teule zilizowasilishwa katika *British Broadcasting Corporation* (BBC). Maudhui yameteuliwa kwa kuzingatia kigezo cha maudhui ambayo yanajitokeza katika kazi ya fasihi ya kipindi hiki cha mwamko mpya. Aidha, tahakiki ya maudhui imetokana na mhimili wa nadharia ya mtindo unaoshikilia kuwa maudhui ni kipengele

muhimu katika utathmini wa ubora wa kazi yoyote ya fasihi (Wamitila, 2003). Masuala yaliyojadiliwa bado yanadhihirika katika jamii tunamoishi. Hivyo basi, ubora wa maudhui umesaidia katika kutathmini ubora wa hadithi fupi teule ambazo zilisomwa katika idhaa ya redio ya Kiswahili ya BBC na hatimaye kuchapishwa katika mikusanyiko: *Mapenzi ni Kikohozi* (1970), *Vituko Duniani* (1970), *Pavumapo Palilie* (1971) na *Kinywa Jumba la Maneno* (1977). Sura inayofuata itahitimisha tasnifu hii kwa kushughulikia muhtasari wa sura za tasnifu, matokeo ya utafiti, matatizo ya utafiti, mchango wa utafiti, hitimisho la utafiti na mapendekezo ya utafiti.

SURA YA TANO

HITIMISHO

5.1 Utangulizi

Sura hii inashughulikia hitimisho la utafiti. Yanayoelezwa ni: muhtasari wa uafiti, matokeo ya utafiti, mchango wa utafiti, matatizo ya utafiti, hitimisho la utafiti na mapendekezo ya utafiti huu.

5.2 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu ulilenga kutathmini hadithi fupi teule zilizowasilishwa katika BBC (*British Broadcasting corporation*) kwa kuzingatia mtazamo wa Poe (1842; 1846) na Leech (1969). Utafiti umetimiza lengo hili kwa kuzingatia hadithi fupi teule za mikusanyiko ifuatayo: *Mapenzi ni Kikohozi* (1970), *Vituko Duniani* (1970), *Pavumapo Palilie* (1971) na *Kinywa Jumba la Maneno* (1977). Malengo makuu katika utafiti huu yalikuwa: Kwanza, kuchanganua muundo wa hadithi fupi teule zilizowasilishwa na BBC. Pili, kueleza dhana ya usawiri wa wahusika katika hadithi fupi teule zilizowasilishwa katika BBC. Tatu, kubainisha maudhui katika hadithi fupi zilizowasilishwa na BBC.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia mseto: nadharia ya hadithi fupi iliyoasisiwa na Poe (1842; 1846) na nadharia ya mtindo iliyoasisiwa na Leech (1969). Nadharia ya hadithi fupi hushikilia mihimili ya muundo wa hadithi fupi. Aidha, nadharia ya mtindo hutumia mihimili inayotathmini vipengele vya fani na maudhui katika hadithi fupi. Utafiti huu umetumia nadharia mbili kwa sababu nadharia ya hadithi fupi inaeleza misingi ya kimuundo. Kufidia

upungufu wa nadharia ya hadithi fupi, nadharia ya mtindo inaeleza misingi ya fani na maudhui.

Sura ya kwanza ya utafiti huu imeeleza kuhusu usuli wa mada ya utafiti, suala la utafiti, maswali na malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia za utafiti na mbinu za utafiti.

Sura ya pili imetathmini muundo wa hadithi fupi teule zilizowasilishwa katika BBC kwa kuzingatia mtazamo wa Edgar Allan Poe. Hadithi fupi teule zilizohakikiwa zimo katika mikusanyiko: *Mapenzi ni Kikohozi* (1970), *Vituko Duniani* (1970), *Pavumapo Palilie* (1971) na *Kinywa Jumba la Maneno* (1977). Muundo wa ubora wa hadithi fupi kupitia mihimili iliyowekwa na Poe (1842; 1846) umedhihirika katika hadithi fupi teule.

Sura ya tatu imeshughulikia dhana ya usawiri wa wahusika katika hadithi fupi teule. Uhakiki umezingatia vipengele vifuatavyo: aina ya wahusika, idadi ya wahusika pamoja na jukumu lao, uthabiti wa wahusika, mshabaha wa lugha ya wahusika na ile ya hadhira lengwa na kusadikika kwa wahusika kutokana na matendo yao. Uhakiki wa kimtindo umethibitisha ubora wa hadithi fupi teule kutokana na hadithi fupi teule zilizohakikiwa kuzingatia kanuni za vipengele hivi.

Sura ya nne imeangazia maudhui ambayo yaliwasilishwa katika hadithi fupi teule zilizowasilishwa katika idhaa ya redio ya Kiswahili ya BBC. Maudhui haya ni kama vile: elimu, ndoa, mapenzi, tamaa, nafasi ya mwanamke katika jamii, utabaka, utamaduni, bidii, ukatili, utamaushi, uzinzi, kisasi na dini. Tathmini ya maudhui imebainisha kuwa maudhui haya bado ni faafu katika kipindi hiki cha mwamko mpya.

5.3 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kutimiza malengo matatu. Kwanza, kuchanganua muundo wa hadithi fupi zilizowasilishwa katika BBC. Lengo hili liliafikiwa kutokana na kutathmini muundo wa hadithi fupi teule kwa kuzingatia misingi ya hadithi fupi iliyowekwa na Poe. Hadithi zimedhihirisha kuwa na mtiririko bora wa mawazo ambayo yanasomeka katika kikao kimoja, zinajenga tukio moja katika uwasilishaji wa dhamira na maudhui, utatuzi mzuri wa mgogoro na matumizi ya lugha yenye mvuto kwa hadhira kwa kutumia mbinu mbalimbali za lugha kama vile; taswira, chuku, misemo na mbinu nyinginezo zilizochanganuliwa katika utafiti huu. Aidha, utanzu huu umeendelea ukikua zaidi kwa sababu hadithi za sasa zimedhihirisha matumizi ya tanzu nyinginezo kama ushairi na mbinu za sanaa kama vile barua katika kusanii hadithi fupi.

Lengo la pili ni kueleza usawiri wa wahusika katika hadithi fupi zilizowasilishwa na BBC. Usawiri wa wahusika katika hadithi fupi teule umetathminiwa kwa kuzingatia vigezo vya ubora tulivyotaja awali katika sura ya tatu. Vigezo hivi vimebainisha ubora wa hadithi fupi teule. Ubora wa

hadithi unatokana na mojawapo ya hadithi kama “Mke Wangu” (Muhammed, 1977) iliyoko katika mkusanyiko wa *Kinywa Jumba la Maneno* (1977) kuchapishwa katika mkusanyiko wa *Damu Nyeusi* (2007).

Katika lengo la tatu, maudhui katika hadithi fupi zilizowasilishwa na BBC yamebainishwa. Imebainika kuwa, maudhui kama vile: elimu, ndoa, mapenzi, tamaa, nafasi ya mwanamke katika jamii, utabaka, utamaduni, bidii, ukatili, utamaushi, uzinzi, kisasi na dini bado yanafaa katika kipindi hiki cha mwamko mpya. Ufaafu wake unatokana na maudhui yaya haya kuwasilishwa katika kazi za sasa za fasihi kwa sababu bado ni masuala ibuka katika jamii tunamoishi. Hivyo basi, hadithi fupi teule zinawasilisha ujumbe unaoelekeza jamii kama mojawapo ya dhima ya fasihi (Matei, 2011).

5.4 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu umetathmini ubora wa hadithi fupi ambazo ziliwasilishwa katika idhaa ya redio ya Kiswahili ya BBC na hatimaye kuchapishwa. Ubora wa hadithi fupi hizi teule utawafaidi wapenzi wa fasihi ya Kiswahili hususani wapenzi wa hadithi fupi kwa njia zifuatazo: Kwanza, utafiti utawafaa wasomi wa hadithi fupi ili waelewe historia na maendeleo ya utanzu wa hadithi fupi hapa Afrika Mashariki kwa sababu tathmini ya ubora wa hadithi fupi imefanyiwa mikusanyiko ya awali zaidi kuchapishwa.

Pili, utafiti utawafaa waandishi chipukizi katika kusanii kazi zenye ubora wa muundo, mtindo, mtiririko, mshikamano, mvuto na maudhui yenye ubora wa kuifaa jamii ya sasa na kizazi cha baadaye.

Tatu, hadithi fupi teule zimechangia katika kusarifu na kusanifu muundo wa hadithi fupi ya Kiswahili kutokana na baadhi ya hadithi kudhihirisha dhana ya mwingiliano tanzu ambayo Poe hakugusia. Hadithi kama vile; "Siku ya Arobaini" (Mohamed, 1970) ambayo ndani yake kuna matumizi ya barua na hadithi, "Sina Rafiki" (Wahab, 1977) yenye sajili ya redio ndani yake.

Nne, hadithi fupi teule zimeonyesha kwamba maudhui ambayo hapo awali yalikuwa yakiwasilishwa katika nyimbo, ushairi na riwaya vilevile yanaweza kuwasilishwa katika hadithi fupi. Maudhui haya ni kama vile; changamoto katika ndoa, athari za mapenzi na uzinzi, athari za tamaa, nafasi ya mwanamke katika jamii, athari ya utabaka, mila na desturi katika jamii, umuhimu wa bidii, ukatili katika jamii na nafasi ya dini katika jamii.

Tano, kwa kuchangia katika kueleza vigezo vya kutathmini ubora wa hadithi fupi ya Kiswahili; hadithi hizi zimeinukia kuwa za kirasimi. Vigezo hivi ni kama vile: mtiririko bora wa mawazo yanayosomeka katika kikao kimoja, ujenzi wa tukio moja katika kuwasilisha maudhui lengwa kwa kujikita katika mgogoro mmoja tu, ujenzi wa ploti bora kutokana na utatuzi mzuri wa mgogoro, matumizi ya lugha yenye mvuto ili kunasa hisia za msomaji au

msikilizaji na usawiri bora wa kipengele cha usawiri wa wahusika na uhusika wao katika hadithi fupi.

Sita, tathmini ya hadithi fupi teule imebainisha kuwa uchoraji wa picha katika hadithi fupi una athari katika kuvuta makini ya msomaji wa hadithi fupi suala ambalo Poe hakufafanua. Baadhi ya hadithi fupi zilizotathminiwa zimetumia uchoraji wa picha kuboresha uwasilishaji wa dhamira katika hadithi. Hadithi zilizotumia picha ni nne kati ya nane zilizotathminiwa: Hadithi ya "Ajuta Majuto ya Mjukuu" (Somba, 1970), "Maisha Yalimwendea Kombo" (Isaakwisa, 1970), "Sina Rafiki" (Wahab, 1977) na "Mke Wangu" (Muhammed, 1977). Hall (1990) anaeleza kuwa picha ni muhimu katika fasihi ya watoto na vilevile fasihi wa watu wazima ili kuvuta makini ya msomaji, kueleza muhtasari wa hadithi na kuwasilisha ujumbe kwa haraka.

5.5 Matatizo ya Utafiti

Utafiti ulikumbwa na vikwazo kama vile: kwanza, kupatikana kwa mikusanyiko hii ilikuwa changamoto kubwa. Muda wa miezi saba ndio ulitumika ili kupata mikusanyiko yote. Mkusanyiko wa *Kinywa Jumba la Maneno* (1977) ulipatikana Tanga, Tanzania kwa bei ya juu sana maana ulinunuliwa kutoka kwa maktaba ya mtu binafsi (elfu ishirini za Tanzania). Ifahamike kuwa bei hii ni kando na ada ya kusafirisha kitabu kutoka Tanga hadi Mombasa.

5.6 Mapendekezo

Utafiti huu ulitathmini hadithi fupi teule zilizowasilishwa katika BBC kwa mtazamo wa Edgar Allan Poe na Leech (1969). Utafiti ulihusisha uhakiki wa mikusanyiko minne ya awali zaidi kuchapishwa hapa Afrika Mashariki. Muundo wa hadithi fupi teule, dhana ya usawiri wa wahusika na ubainishaji wa maudhui umejadiliwa kwa kuzingatia upeo na mipaka ya utafiti. Utafiti zaidi unaweza kufanywa kuzingatia yafuatayo:

Kwanza, kurejelea hadithi fupi ambazo huchapishwa katika uwanja wa TEKNOHAMA wa magazeti kama vile *Taifa Leo.*

Pili, tathmini ya hadithi fupi teule tulizohakiki inaweza kufanywa kwa kuzingatia mtazamo wa Nathaniel Hawthorne (1804-1864) tofauti na utafiti huu ambao umejikita na mtazamo wa Edgar Allan Poe (1809-1849) na Leech (1969).

Tatu, utafiti mwingine unaweza kutathmini muundo wa kazi za waandishi wengine wa hadithi fupi za awali kusomwa hewani baada ya kipindi cha mashindano ya hadithi fupi cha BBC kusitishwa miaka ya 1970. Waandishi kama vile Ali Abdulla Ali ambao hadithi zao zilisomwa hewani katika Idhaa ya Kiswahili ya Sauti ya Ujerumani na bado wanachapisha kazi zao katika kipindi hiki cha mwamko mpya.

Kwa kufanya hivyo, fasihi andishi ya Kiswahili itaendelea kukua kwa kasi na kwa ubora wa hali ya juu.

5.7 Hitimisho

Kutokana na utafiti huu, tathmini ya hadithi fupi teule zilizowasilishwa katika BBC kwa mtazamo wa Edgar Allan Poe na Leech (1969) imeonyesha kuwa hadithi hizi zilifikia kiwango cha ubora. Kiwango cha ubora kimetokana na tathmini ya muundo wa hadithi fupi teule, usawiri wa wahusika na uhusika wao katika hadithi na uwasilishaji wa maudhui yenye uhalisia kwa jamii. Aidha, imebainika kuwa baadhi ya wasanii wa hadithi fupi teule tulizotathmini bado wanachapisha kazi zao katika kipindi hiki cha mwamko mpya kutokana na ubora wa kazi zao. Kwa mfano; Said Ahmed Mohamed amechapisha mikusanyiko ya *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine* (2005) na *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine* (2005). Vilevile, waandishi wengine bado wamechapisha kazi za riwaya kando na hadithi fupi kama vile Zainab Burhani aliyechapisha *Kipimo cha Mizani* (2004). Hivyo basi, tathmini hii inabainisha wazi kuwa endapo kanuni za utunzi wa hadithi fupi zitazingatiwa basi mashirika makuu ya uchapishaji hayatakosa kung'ang'ania kazi kama hizo. Hata hivyo, mikusanyiko ya awali zaidi kuchapishwa hapa Afrika Mashariki ilichochea waandishi wengine kuibuka kutokana na kuweka misingi ya kusarifu na kusanifu hadithi fupi ya Kiswahili. Kwa njia hii, ubora wa hadithi fupi zilizowasilishwa katika BBC umechangia kukuza utanzu huu wa hadithi fupi ya fasihi andishi.

MAREJELEO

Abuhaimed, S. (2019). *Crime and Revenge*. Seattle: Kindle Direct Publishing.

Atiyya, A.M. (1991). "Naguib Mahfouz and The Short Story". In, Gassick, T. (Ed.). *Critical Perspectives on Naguib Mahfouz*. Washington: Three Continents Press. (pgs. 10-21).

Barger, A. (2008). *Edgar Allan Poe: Annotated and Illustrated Entire Stories and Poems*. Tennessee: Bottletree Books.

BBC (2017). *Historia ya Idhaa ya Kiswahili ya BBC*. https://www.bbc.com/swahili/habari-40404261. (Juni 26, 2017).

Beck, A.T. & Alford, B.A. (2009). *Depression: Causes and Treatment*: Philadelphia:University of Pennsylvania.

Behrman, J.R. & Stacey, N. (1997). *The Social Benefits of Education*. Michigan: University of Michigan Press.

Bertoncini, E.Z. (1998). "Palm Oil With Which Swahili Words are Eaten: Use of Proverbs in Modern Swahili Literature". In, Makward, E. Ravellpinto, T. na Songolo, A. (Eds.). *The Growth of African Literature: Twenty Five Years After Dakar and Fourah Bay*. Asmara: Africa World Press, inc. (pgs.1-5).

Bloch, B. (1953). "Linguistic Structure and Linguistic Analysis ". In, Lang, B. (Ed.). *The Concept of Style*. New York: Cornell University Press. (pgs.46-205).

Bottero, W. (2005). *Stratification: Social Division and Inequality*. New York: Routledge Publishers.

Bramah, E. (2016). *Ultimate Collection: 20+ Novels & Short Stories*. New York: Amazon Publishers.

Burhani, Z. (2004). *Kipimo cha Mizani*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Burke, C. (1999). *Covenanted Happiness, Love and Commitment in Marriage (2nd Edition)*. New Jersey: Screptree Publishers.

Chandra, S.S. & Sharma, R.K. (2004). *Sociology of Education*. New Delhi: Atlantic Publishers.

Chokocho, A. na Kayanda, D. (Wahr) (2016). *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Longhorn Publishers Limited.

Crews, M. (2004). *Hard Work: Success Made Easy*. Escondido: SDG Press.

Crystal, D. & Davy, D. (1969). *Investigating English Style*. London: Longman Group.

Coombes, H. (1953). *Literature and Criticism*. London: Penguin Books.

Detweiler, R. & Jasper, D. (2000). *Religion and Literature*. Louisville: Westminster John Knox Press.

Esenwein, B. J. (1909). *Writing the Short Story: A Practical Handbook on the Rise, Structure, Writing and Sale of the Modern Short-Story.* Pennsylvania: Hinds, Nobe and Eldredge.

Fincham, F.D. & Cui, M. (2011). *Romantic Relationships in Emerding Adulthood*. Cambridge: Cambridge University Press.

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa.* Nairobi: Oxford University Press.

Forster, E.M. (1927). *Aspects of the Novel*. Cambridge: Edward Arnold.

Frow, J. (2014). *Character and Person*. Oxford: Oxford University Press.

Fullan, M. (2016). *The New Meaning of Education Change*. New York: Teacher College Press.

GaaG, N.V.D. (2014). *Feminism & Men*. London: Zed Books Ltd.

Goyet, F. (2017). *The Classic Short Story, 1870-1925: Theory of a Genre*. Cambridge: Open Book Publishers.

Green, J.B. (2011). *Dictionary of Scripture and Ethics*. Michigan: Baker Academic.

Habwe, J. (Mhr) (2010). *Mizungu ya Manabii na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Oxford University Press.

Hall, S. (1990). *Using Picture Storybooks to Teach Literary Devices: Recommended Books for Children and Young Adults*. California: Greenwood Publishing Group.

Henry, G. (2018). "Mchango wa Tanzu za Asili Katika Riwaya ya Kiswahili: Uchunguzi Kifani wa Riwaya ya *Uhuru wa Watumwa*". Katika *Mulika* Na. 33. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (kur. 58-67).

Hills, R. (2000). *Writing in General and the Short Story in Particular*. New York: Houghton Mifflin Harcourt Company.

Hulsey, T.L. & Frost, C.J. (2004). *Moral Cruelty: A Meaning and The Justification of Harm*. New York: University Press of America.

Iribemwangi, P.I. (Mhr) (2007). *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine.* Nairobi: East African Educational Publishers Limited.

Iribemwangi, P.I. (Mhr) (2011). *Kunani Marekani na Hadithi Nyingine.* Nairobi: Target Publications Limited.

Kairu, W.M. (2005). "Uhalisi na Mtindo wa Ken Walibora Katika Fasihi ya Watoto". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Kalman, B. (2009). *What is Culture?*. New York: Crabtree Publishing Company.

Kaui, T.M. (2011). "Tathmini ya Usimilisho wa Riwaya na Hadithi Fupi kwa Wanafunzi wa Sekondari Nchini Kenya". Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

King'ei, G.K. na Wafula, R.M. (1997). *Pendo la Heba na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Chama cha Waandishi Kenya.

Lavanya, S. (2013). *Conflict*. https://www.booksoarus.com. (Oktoba 10, 2019).

Leech, G.N. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman Group Ltd.

Leech, G.N. (2013). *Language in Literature: Style and Foregrounding*. London: Routledge.

Leech, G.N. & Short, M. (1981). *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to English Fictional Prose (2nd Edition*). Harlow: Longman Group Ltd.

Lewis, A. (2008). *Adultery Pandemic: Healing Ourselves and Restoring Marriage*. Michigan: Zondervan Publishing.

Longman (1970). *Mapenzi ni Kikohozi*. Nairobi: Longman Ltd.

Longman (1970). *Vituko Duniani*. Nairobi: Longman Ltd.

Longman (1971). *Pavumapo Palilie*. Nairobi: Longman Ltd.

Longman (1977). *Kinywa Jumba la Maneno*. Nairobi: Longman Ltd.

Lyon, E. (2014). *A Writer's Guide to Fiction: A Concise Practicle Guide for Novelists and Short – Story Writers*. New York: The Berkley Publishing Group.

Makena, E. A. (2018). "Uwasilishaji Maudhui katika Hadithi Fupi za Said A. Mohamed". Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Matei, A. (2011). *Fani ya Fasihi Simulizi*. Nairobi: Oxford University Press.

May, C. E. (2002). *The Short Story: The Reality of Artifice*. London: Routlege Publishers.

Mazrui, A. (2007). *Swahili Beyond the Boundaries: Literature, Language and Identity*. Ohio: Ohio University Press.

Mbatiah, A.M. (Mhr) (2000). *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundations.

Mbiti, J.S. (1991). *Introduction to African Religion*. Nairobi: East African Educational Publishers.

McCarthy, T. (2000). *Teaching Literature Elements With Short Stories*. London: Penguin Publishers.

McKinney, M.J. (2005). *Grammardog Guide to Poe Short Stories*. Christoval: Grammardog Publishers.

McOnyango, O. (2006). *Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Focus Publishers.

Mohamed, B. (2008). "Usemezano kama Mkakati wa Kufahamu Riwaya za *Babu Alipofufuka* (2001), *Bina-Adamu!* (2002) na Mkusanyiko wa Hadithi Fupi wa *Sadiki Ukipenda* (2002)".Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Mohamed, S.A. (1978). *Si Wazimu Si Shetani*. Nairobi: Longman Publishers.

Mohamed, S.A. (1980). *Utengano*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mohamed, S.A. (1988). *Kiza Katika Nuru*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mohamed, S.A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Riwaya, Tamthiliya na Hadithi Fupi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mohamed, S.A. (2001). *Babu Alipofufuka*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Mohamed, S.A. (2002). *Sadiki Ukipenda na Hadithi Nyingine*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Mohamed, S.A. (2005). *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Longman Publishers.

Mohamed, S.A. (2005). *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Mohamed, M.S. (1976). *Nyota ya Rehema.* Nairobi: Oxford University Press.

Mohamed, M.S. (1978). *Kicheko cha Ushindi.* Nairobi: Shungwaya Publishers.

Mohochi, E.S. (1995). "Fani Katika Hadithi Fupi za Kiswahili". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Egerton. (Haijachapishwa).

Mohochi, E.S. (2018). "Hadithi Fupi: Utanzu Uliopuuzwa." Katika *Mulika* Juz. 24. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Momanyi, C. (2006). *Tumaini.* Nairobi: Vide~Muwa.

Momanyi, C. na Timammy, S.R. (Wahr) (2011). *Takrima Nono na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Longman.

Moses, O. (2014). *Out of Character: Modernism, Vitalism, Psychic Life*. Stanford: Stanford University Press.

Msokile, M. (1992). *Misingi ya Hadithi Fupi*. Dar Es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mukopi, L.M. (2005). "Hadithi Fupi za Kisasa za Kiswahili kama Utanzu Mahuluti". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Musili, L.M. (2015). "Athari ya Mbinu Rejeshi Katika Hadithi Fupi za Kiswahili". Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Muusya, J.K. (2012). "Mandhari Katika Hadithi Fupi: Ulinganishaji wa Diwani za *Pendo la Heba na hadithi nyingine* (1997) na *Mizungu ya Manabii na hadithi Nyingine* (2010)". Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Nasser, G.A. (2007). *An Anthology of Short Fiction: With a Study Aid Essay*. Cairo: The Anglo-Egyptian Bookshop.

Naude, B. & Others (2009). "FCS Integrated English for First Additional Language L3". In, Naude, B. (Ed.). *Characteristics of Short Stories*. London: Pearson Education. (pgs. 295-296).

Nayef, M. (2013). *How to Write a Short Story according to Edgar Allan Poe*. https://www.darkmediaonline.com/happybirthdayedgarallanpoe/. (January 19, 2018).

Ngara, E. (1982). *Stylistics Criticism of the African Novel*. London: Heinmann.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nyamu, M.M. (2015). "Usawiri wa Mandhari Katika hadithi Fupi na Umuhimu wake Katika Kuendeleza Vitushi Katika Hadithi Fupi". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Mount Kenya. (Haijachapishwa).

Omar, B. (Mhr) (2010). *Kopo la Mwisho na Hadithi Nyingine*. Nairobi: EAEP.

Onchangu, R.N. (2013). "Mtindo Katika riwaya na hadithi Fupi za Clara Momanyi". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Oriedo, H.E. (2007). *Istilahi za Fasihi ya Kiswahili*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Paris, B.J. (1997). *Imagined Human Beings: Psychological Approach to Character and Conflict in Literature*. New York: New York University Press.

Pelayo, R. (2001). *Critical Companions to Popular Contemporary Writers: Gabriel Gracia Marquez*. London: Greenwood Press.

Pitlor, H. (2011). *The Best American Short Stories*. New York: Houghton Mifflin Harcourt Company.

Poe, E.A. (1842). “Review of Twice-Told Tales”. In, Carlson, E.W. (Ed.). *A Companion to Poe Studies.* London: Greenwood Press. (pgs.285-286).

Poe, E.A. (1846). “The Philosophy of Composition”. In, Lippmann, B. (Ed.). *Edgar Allan Poe- The Philosophy of Composition*. Norderstedt: GRIN Verlag. (pgs.1-8).

Poe, E.A. (1938). *The Complete Tales and Poems*. New York: Random Housen Inc.

Potter, S.J. (2012). *Broadcasting Empire: The BBC and the British World, 1922-1970.* Oxford: Oxford University Press.

Reid, I. (1977). *The Short Stort*. London: Methuen & Co. Ltd.

Robert, S. (1951). *Kusadikika.* Nairobi: Thomas Nelson and sons Ltd.

Robert, S. (1968). *Utubora Mkulima*. Nairobi: Thomas Nelson and sons Ltd.

Ruhumbika, G. (1974). P*arapanda na Hadithi Nyingine.* Dar es salaam: East African Literature Bureau.

Simpson, P. (2004). *Stylistics: A Resource Book for Students.* London: Routledge.

Stokes, P. & Wall, T. (2014). *Research Methods*. New York: Palgrave.

Sundararaj, A. (2011). *How to Tell a Great Story*. New York: Lean Marketing Press.

Swain, D.V. (2008). *Creating Characters: How to Build Story People*. Oklahoma: University of Oklahoma Press.

Tanui, S.C. (2018). “Usawiri wa Maudhui Yenye Kufunza Wanafunzi wa Vyuo Maadili Mema: Tathmini ya *Alidhani Kapata* (2007) na *Damu Nyeusi* (2007)”. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Tolstoy, L. N. (1960). *What is Art? Translated by Almyer Mande*. New York: Macmillan.

UNESCO (2017). *Cracking the Code: Girls’ and Womens’ Education in Science, Technology, Engineering and Mathematics (STEM)*. Paris: UNESCO.

Wafula, C.N. (2015). “Mgongano wa Tamaduni Katika Hadithi Fupi za Kiswahili”. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Walibora, K.W. (1996). *Siku Njema*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.

Walibora, K.W. na Mohamed, S. (2007). *Kiti cha Moyoni na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Oxford University press.

Walibora, K.W. na Mohamed, S. (Wahr) (2007). *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Oxford University press.

Wamitila, K.W. (2001). *Kamusi ya Methali*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Wamitila, K.W. (2002). *Bina-Adamu!* Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K.W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi.* Nairobi: Focus Publication Ltd.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publication Ltd.

Wamitila, K.W. (Mhr) (2004). *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Focus publishers.

Wamitila, K.W. (2006). *Kamusi ya Misemo na Nahau*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Wamitila, K.W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers.

Wanga, E. (Mhr) (2017). *Orodha Gani na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Evangel Publishing House.

WHO (2020). *Depression*. https://www.who.int. (January 30, 2020).

Zigon, J. (2008). *Morality: An Anthropological Perspective*. New York: Berg Publishing.